Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 15 Agosti, 2006**

*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Nyumba la Taifa kwa Mwaka 2003/2004 *[The Annual Report and Accounts of the National Housing Corporation for the Year 2003/2004]*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Taarifa ya Mwaka ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa Mwaka 2004/2005 *[The Annual Report of the National Social Security Fund for the year 2004/2005]*

**WAZIRI WA FEDHA:** Hati za Uhamishaji Fedha Na. 1 na Na. 2 za Mwaka 2005/*2006 [Statements of Reallocation Warrant No. 1 and No. 2 of 2005/2006]*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 406

**Barabara ya Makoka – Kibangu**

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY (K.n.y. MHE. MHE. HALIMA J. MDEE** ) aliuliza:

Kwa kuwa, wakazi wa Kata ya Makuburi (Mtaa wa Kibangu na Makoka) wanaozidi elfu tano wanategemea barabara ya Makoka – Kibangu kupitia pembezoni mwa mto Gide kwa kuendeshea maisha yao ya kila siku na kwa kuwa, barabara hiyo iko katika hali mbaya sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia barabara hiyo matengenezo ili iweze kukidhi mahitaji ya wakazi wa maeneo hayo?

(b) Kwa kuwa barabara hiyo iko pembezoni mwa mto, Je Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara mbadala na kuifunga hiyo iliyopo sasa?

(c) Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea Kata husika kushuhudia uharibifu huo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Manispaa ya Kinondoni imekuwa ikizifanyia matengenezo ya mara kwa mara barabara katika Kata ya Makuburi na kuzifanya zipitike kwa kipindi cha mwaka mzima. Manispaa ilifanya matengenezo kwa Barabara za Kara ya Makuburi zenye urefu wa kilomita 11.3 kwa mwezi Julai 2006 na barabara ya Makoka – Kibangu ikiwa mojawapo. Kazi hiyo iliigharimu Manispaa jumla ya shilingi 3,793,500/=. Orodha ya barabara zilizofanyiwa matengenezo ni zifuatazo:-

- External – JWTZ Mabibo - km. 2.3;
- JWTZ Mabibo – *Mandela Road* kupitia *SAS* - km. 1.7;
- Makoka – Kibangu - km. 3.7;
- Makoka – Uwanjani - km. 1.3; na
- *International School – River Side* - km. 11.3.

Matengenezo haya hayakuhusisha sehemu iliyomomonyoka kutokana na sehemu hiyo kuhitaji gharama kubwa kwa ajili ya matengenezo.

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Manispaa ilifanya tathmini ya gharama za kuzuia mmomonyoko huo ambapo ulibaini kuwa zilihitajika shilingi 68,000,000/=. Hivi sasa inakadiriwa kuwa itagharimu shilingi 250,000,000/= kutokana na ongezeko la korongo linalotokana na uharibifu mkubwa wa mvua za mwaka 2005/2006. Manispaa

imelazimika kuifunga barabara ya Makoka – Kibangu ili kunusuru maisha ya watu na mali zao.

Sehemu mbadala ya kupitisha barabara hiyo (*Alternative Route*) imeainsihwa. Sehemu iliyoainishwa ina nyumba za watu zipatazo 7 hivyo nyumba hizo zinafanyiwa tathmini ili zilipwe fidia. Baada ya tathmini kukamilika, gharama za kubomoa nyumba hizo na kutengeneza barabara zitajulikana na Halmashauri itaangalia uwezekano wa kutengeneza barabara hiyo kwa kufawa upya vipaumbele vyake.

(c) Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Manispaa walitembelea barabara ya Makoka – Kibangu eneo hilo na wananchi wanaonyesha dhamira ya kufidiwa nyumba zao ili njia mbadala ambayo ipo umbali wa mita 100 kutoka eneo lililoharibika ili iweze kupitika kwa haraka. Aidha, naukubali mwaliko wa Mheshimiwa Mbunge hivyo niko tayari kutembelea Kata ya Makuburi ili kushuhudia uharibifu uliojitokeza.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara aliyozungumzia Naibu Waziri ya Ubungo – Makoka hadi Makoka Shuleni ni barabara ambayo imefanyiwa matengenezo miezi miwili iliyopita, matengenezo hayo hayajakidhi hata kidogo matengenezo ya barabara hiyo.

Baada ya mwezi mmoja barabara hiyo tayari haipitiki na tayari imeshaharibika.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ananihakikishia vipi kwamba wakazi wa Ubungo - Makoka watatengenezewa barabara hiyo angalau katika kiwango cha changarawe?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Blandes, kama ifuatavyo:-

Barabara ya Makoka – Kibangu kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba kuna sehemu ambayo imemomonyoka na haiwezi ikatengenezwa kwa urahisi kwa sababu uharibifu wake ni mkubwa. Kwa sasa hivi wananchi wa sehemu hiyo wanapita barabara mbadala badala ya barabara hiyo ya Makoka – Kibangu, Serikali ilichofanya ni kuhakikisha kwamba wanaifunga ile barabara ili yasije yakatokea madhara.

Pili, Serikali kwa sasa inafanya tathmini ya kuangalia je watengeneze lile korongo ambalo limeharibika au watengeneze *alternative route* na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba *alternative route* ina kiasi cha shilingi milioni 250 kwa sasa hivi tunaangalia pia kama *alternative route* nyingine ya kubomoa nyumba za watu ili waweze kufidiwa ili barabara hii iweze kutengenezwa.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi tunaangalia kwanza hizo *alternative route* ili tujipange upya kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. Kwa sasa wananchi wanazunguka katika barabara ya *International School.*

Na. 407

**Regional Consultative Committee (RCC)**

**MHE. ZITTO KABWE ZUBERI** aliuliza:

Kwa kuwa, *Regional Consultative Committee (RCC)* ni kiungo mihumu sana katika gazi ya Mkoa katika kuimarisha uwajibikaji.

(a) Je, tangu Kamati hiyo iundwe mwaka 1997 kuna matatizo gani ya kiutendaji?

(b) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati muafaka wa kuwa na *Semi – Legislative* badala ya *Regional Consultative Committee (RCC)* ili kuongeza uwajibikaji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zuberi, Mbunge wa Kigoma Kaskazini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria za Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997, Kamati ya Ushauri ya Mkoa yaani *(Regional Consultative Committee*) iliundwa kwa ajili ya kutoa ushauri fasaha ambao utamsaidia Mkuu wa Mkoa kutoa mwongozo wa utekelezaji Mkoani pamoja na kujadili mambo yote ya Mkoa na kutoa fursa nzuri zaidi ya kushauriana na kuratibu mipango ya maendeleo na utekelezaji wake katika Mkoa husika. Aidha, Kamati hii ina jukumu la kutoa ushauri kwa Halmashauri zilizopo chini ya Mkoa husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya ushauri ya Mkoa ni wafuatao:-

(i) Mkuu wa Mkoa ni Mwenyekiti;
(ii) Wakuu wa Wilaya wote katika Mkoa;
(iii) Wakurugenzi wa Halmashauri wote katika Mkoa;
(iv) Wabunge wote wa kuchaguliwa katika Mkoa;
(v) Wabunge wa kuteuliwa/Viti Maalum kutoka Mkoa husika; na

(vi) Katibu Tawala wa Mkoa ni Katibu wa Kamati ya ushauri ya Mkoa.

Matatizo ya kiutendaji yanayozikabili Kamati za ushari za Mkoa ni ya kawaida na hasa yale yanayohusu:-

(i) Uhaba wa fedha za kuendeshea vikao.
(ii) Ukosefu wa Wataalam wa kutosha katika Sekretarieti za Mikoa kuweza kuzishauri Kamati ipasavyo.
(iii) Ukosefu wa vitendea kazi kuwezesha Wataalam wa Sektretarieti kufanya maandalizi mazuri ya vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa.

Ofisi yangu inapitia upya Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya 1997 ili kuboresha utendaji kazi wa Sekretarieti za Mikoa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu ya Kamati ya ushauri ya Mkoa kama yaliyvoainishwa katika Sheria ya Tawala za Mikoa Na 19 ya mwaka 1997, hakuna umuhimu wa kuwa na *Semi – Legislative* katika ngazi ya Mkoa badala ya *Regional Consultative Committee (RCC).* Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri) kwa muundo wa majukumu yake zina *Semi – Legislative Powers* kupitia Madiwani ambazo zinawapa Mamlaka ya kutunga Sheria ndogondogo kuhusu mambo mbalimbali kwa lengo la utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Halmashauri husika.

**MHE. ZITTO KABWE ZUBERI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya sasa *RCC* zinakuwa hazina meno kwa sababu ushauri unapotokea kwamba kuna tatizo la kiubadhilifu ni vigumu kwa Wajumbe wa *RCC* kuweza kuchukuka hatua zozote kwa sababu mtaambiwa kwamba ni ushauri tu.

Je, ni lini Serikali italeta Muswada Bungeni kuweza kurekebisha Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997 ili kuzipa nguvu *RCC?*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zuberi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Ofisi yangu inapitia upya Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997 ili kuboresha utendaji katika kazi katika Sekretarieti za mikoa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Sheria hiyo inaletwa hivi karibuni katika Bunge lako Tukufu ili kuifanyia *Amendment* mbalimbali. (*Makofi*)

Lakini, hata hivyo, *RCC* bado zina meno na bado zina nguvu ni kwamba Sheria ile ikitekelezwa vizuri bado *RCC* ina nguvu ya kushauri na pia kuchukua hatua mbalimbali kwa wale ambao wanaleta ubadhilifu au wanaleta matatizo katika Halmashauri za Wilaya. (*Makofi*)

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kikao hiki cha *RCC* ni kikao muhimu sana Mkoani na kwa kuwa kinafanyika mara moja kwa mwaka je, Serikali haioni kwamba kwa wakati huu wa kasi mpya inafaa viongezwe vikao kuliko kufanya mara moja kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Laizer M. Lekule kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *RCC* kwa mujibu wa Sheria inatakiwa kukaa mara mbili kwa mwaka na siyo mara moja tu labda ni kwa sababu tu ya ukosefu wa fedha ndiyo maana sehemu nyingine wanakaa mara moja lakini inatakiwa ikae mara mbili kwa mwaka. (*Makofi*)

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Sheria hiyo Namba 19 ya mwaka 1997 inafanyiwa marekebisho na sisi tutaangalia kwamba je ni vema ikaongezewa vikao vikawa 2 au 3 na kuendelea au vikabie vikao vikao 2. Napokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutaufanyia kazi na ninaomba wengine ambao wana mapendekezo mbalimbali wanaweza wakatuletea ili tuweze kuyajumuisha katika *Amendment* ya Sheria hii.

**MHE. MANJU SALUM OMAR MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amesema Wajumbe wa *RCC* miongoni mwao ni pamoja na Wabunge wa Majimbo na Wabunge wa Viti Maalum. Je, ushiriki wa Wajumbe hawa una tofauti kati ya Mkoa na Mkoa? Kwa sababu kwa Mkoa wa Kigoma Wajumbe wale ambao ni Wabunge wa Viti Maalum wanapohudhuria vikao hivi hawalipwi posho kama wanavyolipwa Wajumbe wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Manju Msambya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu mimi na Sheria inavyosema kwamba Wajumbe wote ni sawa, hakuna Mjumbe ambaye anatakiwa alipwe na Mjumbe ambaye hatakiwi kulipwa. Mimi nafikiri ni utaratibu tu wa Mikoa ambao wanafanya hivyo, lakini kisheria kila Mjumbe anatakiwa alipwe kama kukosa Wajumbe wote wakose kutokana na kutokuwa na fedha. Kwa hiyo, natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa kwamba *Regional Consertative Committee*, *Members* wote ni sawa na wanatakiwa walipwe sawa na kama hakuna posho basi wakose wote. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Kamati hizi za Mashauriano zimeonekana kufaa sana na kuunganisha Mawazo ya Mkoa kwa maana ya Wilaya katika Mkoa na hivyo kuunganisha hata mawazo ya kimaendeleo.

Je, Naibu Waziri au Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kutunga kanuni ambazo zitaelekeza hizi Kamati muhimu zifanye kazi zao zote kama sawa kwa Taifa zima ili kuondoa hizi dosari ndogondogo. Vilevile kwa kuwa Sheria inakuja kurekebishwa je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuweka fungu maalum ili sasa kazi za Kamati hizi zisiwe ni hisani ya Mkuu wa Mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalila nyongeza la Mheshimiwa William Shellukindo kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya nyongeza kwamba kwa sasa hivi tunafanyia *amendment* hiyo ya Sheria mtu yeyote au Mjumbe yeyote ambaye ana mawazo mazuri kama ya Mheshimiwa William Shellukindo atuletee ili tuyaingize katika *amendment* ya Sheria hiyo.

Kwa hiyo, napokea ushauri wako na tutaufanyia kazi. (*Makofi*)

Na. 408

**Kuondoa Umaskini**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA (K.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI)** aliuliza:

Kwa kuwa, lengo la Serikali la kuanzisha Wizara hii ni kutoa faraja kwa Watanzania wote katika nyanja ya kuondoa umaskini, lakini mpaka sasa mikopo iliyotolewa bado ina masharti magumu.

(a) Je, Mfuko wa *SELF* unasaidiaje katika kuondoa umskini?

(b) Ni kwa kiasi gani umaskini utaondolewa wakati ambapo kundi kubwa la watu hawajaelimika juu ya elimu ya kawaida na hata ile ya kuondoa umaskini?

(c) Je, ni kwa kiwango gani umaskini umepungua tangu Wizara hii ianzishwe tofauti na iliyokuwa kabla?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami kama ifuatavyo:-

Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami Mbunge wa Nkasi, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Jitihada za Serikali za kupiga vita umaskini zilianza tangu tulipopata uhuru mwaka 1961, tulipotangaza vita dhidi ya maadui wakuu watatu yaani Umaskini, Ujinga na Maradhi. Katika mwaka 1995 Serikali ilianzisha Idara ya Kuondoa Umaskini wakati huo ikiwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa lengo la kuratibu, kufuatilia na kuboresha juhudi za kupambana na umaskini.

Jitihada za kutoa mikopo kwa wananchi ni njia mojawapo ya kuwapatia mitaji katika kuwawezesha kufanya biashara mbalimbali. Nakubaliana na Mheshimiwa Nyami kuwa mikopo itolewayo bado ina masharti magumu. Hii inatokana na uchache wa Asasi na Benki zikopeshazo ambazo zimejiwekea masharti hayo ili kuthibiti urudishaji wa mikopo na kupata faida itakayowezesha kuendesha Asasi hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilianzisha miradi wa kutoa mikopo midogo *Small Entepreneurs Loan Facility (SELF)* ikiwa ni hatua mojawapo ya kutekeleza mkakati wa kupunguza umaskini wa kipato. Kwa kupitia Asasi za Kifedha, mradi hutoa mikopo midogo kwa wananchi wenye vipato vidogo ili waitumie mikopo hiyo kufanyia biashara na hatimaye kujiongezea kipato, kipato kikiongezeka ni rahisi kumudu mahitaji muhimu. Huduma hii ya mikopo ya *SLF* ipo katika mikoa 14 ambayo ni pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mtwara, Lindi, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Mwanza, Iringa, Mbeya na Ruvuma.

Aidha, mradi wa *SELF* pia unatoa huduma katika mikoa yote ya Zanzibar. Mpaka kufikia mwishoni mwa Juni 2006, Mfuko wa *SELF* ulikwishatoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 7.105 kwa Asasi 114 katika maeneo ya mradi. Mikopo hii imewafikia walengwa wapatao 37,364 ambao kati yao wanawake ni asilimia 62. Matarajio ya serikali ni kupanua huduma hii ya mikopo kufikia Mikoa yote ya Tanzania.

*(b) SELF* hutoa mafunzo kwa lengo la kuzijengea uwezo Asasi shiriki ili ziweze kutoa mikopo na huduma nyingine kwa walengwa kwa ufanisi zaidi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya Asasi zinazotoa huduma ya kifedha kwa wananchi zina

mapungufu kama vile kutokuwa na watendaji wenye uwezo, uwezo mdogo wa kuandaa mipango ya biashara, vitendea kazi kama usafiri wa kuwafikia walengwa walioko vijijini, kutoa mafunzo kwa walengwa kabla ya kuwapatia mikopo na kadhalika.

Hadi kufikia Juni 2006, *SELF* imetoa mafunzo kwa watendaji 1,491 wa asasi mbalimbali ikiwa ni pamoja na *SACCOS*, *CBOs* na *NGOs*.

Aidha, *SELF* pia inazifadhili asasi shiriki kugharamia mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa ambapo walengwa wapatao 3,175 wameshapatiwa mafunzo hayo.

(c) Kwa jumla uchambuzi wa utafiti wa Hali ya Kipato na Matumizi katika Kaya (*Household Budget Survey (HBS*) uliofanyika kuanzia mwezi Mei, 2000 hadi Aprili, 2001 ulionyesha kuwa umaskini unapungua ingawaje siyo kwa kasi inayotarajiwa. Utafiti unaonyesha kuwa idadi ya watu wanaoishi katika umaskini (Kutokukidhi Mahitaji muhimu – *basic needs*) ilipungua kutoka 38.6 katika mwaka 1991/1992 kufikia asilimia 35.3 katika mwaka 2000/2001.

Aidha, idadi ya wanaoishi katika umaskini uliokithiri (kutoweza kupata mahitaji ya chakula) ilipungua kutoka asilimia 21.6 katika mwaka 1991/1992 hadi 17.7 katika mwaka 2000/2001. Pamoja na mafanikio hayo, viwango vya umaskini mijini na vijijini bado ni vikubwa na hasa vijijini, tuendelee kufanya juhudi kupunguza umaskini nchini.

Baada ya utafiti wa 1991/1992 na wa 2000/2001, utafiti mwingine utafanyika mwaka 2006/2007. Utafiti huu utatuwezesha kujua hadi wakati huu 2006/2007 umaskini utakuwa umepungua kwa kiwango gani. Kwa upande wa takwimu zinazopima umaskini usio wa kipato (elimu, afya, maji na kadhalika) ni rahisi kupima kwa kuwa kila mwaka takwimu hizo hukusanywa. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba mikopo mingi ya aina hii imekuwa ikitolewa mijini zaidi kuliko vijijini?

Pili, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kuwa jana Serikali imefanya kitendo cha kimapinduzi cha kuweza kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kuondoa umaskini vijijini kwa ajili kutoa mikopo katika Sekta mbalimbali ikiwemo kilimo.

Je, Serikali sasa inaweza ikaziekeleza Benki zikapunguza urasimu na muda mrefu wa kutoa mikopo? Na muda uwe mwisho kabisa siku saba (7) mtu awe amepata mkopo wake?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Christant Majiyastanga Mzindakaya, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu mikopo hii ya *SELF* kwenda zaidi mijini kuliko vijijini nakubaliana naye kwa sehemu fulani kwamba mikopo imekuwa ikipelekwa zaidi mijini, lakini tumekuwa sasa tunawaagiza *SELF* kwamba sasa waelekeze mikopo yao vijijini na katika miwili au mitatu ya nyuma kunaonekana maendeleo kuliko ilivyokuwa pale mwanzo.

Kuhusu urasimu katika mabenki, ni kweli kuna urasimu na Serikali imekuwa ikiwasiliana na Benki zote za Biashara nchini kuhakikisha kwamba urasimu huu unapunguzwa na sasa hivi kutokana na hizi fedha za wastani wa bilioni moja ambazo zitakwenda Mikoani. Tumekubaliana na *NMB CRDB* kwamba urasimu upunguzwe kabisa.

Vilevile mambo kama vile *fees* kwa ajili ya kufanya *application* na kadhalika yote haya nayo yameondolewa, kwa hiyo matumaini ya Serikali ni kwamba kutokana na maelekezo haya ya Serikali na kwa ushirikiano na mabenki haya, urasimu katika kushughulikia Mfuko wa Uwezeshaji kule vijijini utapungua. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nilikuwa naomba Serikali itufahamishe ni lini itaweza kushawishi mabenki kuweza kupunguza riba kwa wananchi ili jitihada zote wanazofanya katika biashara fedha zisiishie kulipia riba kubwa inayotozwa na mabenki haya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kama nilivyosema pale mwanzoni wakati namjibu Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kwamba tunafanya jitihada, tunawasiliana na Benki kuhusu suala la kupunguza riba.

Lakini kwa fedha hizi za uwezeshaji ambazo zitakuwa bilioni 1 kwa kila Mkoa. Tumekubaliana na mabenki kwamba riba itakuwa asilimia 10 tu, jambo ambalo halijawahi kutokea. Kwa sababu huko nyuma benki hizi zilikuwa zina-*charge* riba kwa asilimia kati 16 mpaka asilimia 25. Kwa *Macro-Finance Institutions* mpaka asilimia 36. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatua za awali zimeanza kuchukuliwa na ni matumaini ya Serikali kwamba tutaendelea kuwasiliana na mabenki kwa kweli kuendelea kupunguza riba ili wananchi wengi zaidi wapate fursa ya kukopa.

**MHE. ELIATTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ni nia nzuri ya Serikali kuhakikisha kwamba mikopo inawafikia

wanajiji wote nchi nzima. Je, lini *SELF* itafika katika Mkoa Rukwa ambako wanavijiji wengi hawajapata mikopo tangu tupate uhuru? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, *SELF* ilianzishwa kwa awamu kama ambavyo nilijibu katika swali langu la msingi. Mwaka 2004 tulianzisha *SELF* katika Mikoa sita, lakini mwaka 2004 tuliongezea Mikoa mingine minne. Ni matumaini yetu kwamba katika Awamu inayokuja sasa Mikoa yote itakuwa *covered* ukiwemo Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Na. 409

**Kiwanda cha Kusindika Nyama Cha Dar es Salaam**

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED (K.n.y. MHE. LUCY F. OWENYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa mojawapo ya sababu za kubinafsisha Mashirika ya Umma ni kuongeza ufanisi/tija:-

Je, ni lini kiwanda cha kusindika nyama (*Tanganyika Parkers*) cha Dar es Salaam kitaanza uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kampuni ya kusindika nyama ya *Tanganyika Parkers Limited (TPL)* ilianzisha uzalishaji na usindikaji wa nyama katika kiwanda cha Kawe mwaka 1951. Mara baada ya Uhuru Serikali iliingia mkataba wa uendeshaji na kampuni ya *Brooke bond Liebig (BBL)* ya Uingereza ambapo Serikali ilikuwa na hisa asilimia 51 na kampuni hiyo kubakia na asilimia 49.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *Tanganyika Packers Limited* kilitaifishwa mnamo mwaka 1974 na kuendeshwa kama Shirika chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma. Kutokana na kutaifishwa kwake Kampuni ya *TPL* ilipoteza cheti cha ubora wa nyama (*Sanitary Certificate*) kilichokuwa kinatolewa na Serikali ya Uingereza.

Kampuni ya *Brooke Bond Liebig* nayo ikafuta mkataba wake wa kununua nyama kutoka *TPL*. Kukosekana na soko la nje la nyama kuliikosesha *TPL* mapato na hivyo kuingia kwenye matatizo ya kifedha na kiuendeshaji na kuwa na madeni makubwa. Kampuni ilisimamisha uendeshaji na uzalishaji wa nyama mwaka 1984 na kiwanda hatimaye kikafungwa mwaka 1993.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha kusindika nyama kilichopo Kawe *(TPL)* kilibinafsishwa kwa Mwekezaj*i (M/S Al – Ghurair* wa Falme za Kiarabu (*United Arab*

*Emirates*) ambapo mwekezaji huyo alikabidhiwa eneo la kiwanda tarehe 23 Aprili, 2002 ili aliendeleze kulingana na mpango aliowasilisha Serikalini. Hata hivyo, kwa kuwa kiwanda hiki kilikuwa kimekaa kwa takriban miaka 20 bila kufanya kazi, baadhi ya mitambo na mashine zake zilikuwa zimechakaa mno kuweza kufanya kazi.

Aidha, kutokana na eneo hilo kusongwa na makazi ya watu ilionekana halifai tena kuweka kiwanda cha kusindika nyama. Hivyo mwekezaji alipendekeza mpango mbadala wa kukitumia kiwanda hiki na eneo lake. Kutokana na sababu hizo Serikali ilikubali matumizi mbadala.

Mheshimiwa Spika, katika mpango mbadala wa awali wa kuendeleza eneo hilo mwekezaji huyo alionyesha kuwa angejenga maduka makubwa (*Shopping Malls*). Hata hivyo mwaka 2003 aliwasilisha Serikali ombi la kujenga shule ya kimataifa na viwanja vya kisasa vya michezo badala ya kujenga maduka makubwa. Baada ya Serikali kutafakari Serikali ililiridhia ombi hilo. Mwekezaji huyo ameanza kuwekeza kwa kujenga ukuta kuzungushia eneo hilo. Hivyo hatutarajii kuona uzalishaji wa nyama pale Kawe, badala yake tunatarajia kuona shule na viwanja vya michezo kulingana na mpango mpya wa mwekezaji.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, napenda niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Naibu Waziri amekiri kwamba kuna mabadiliko makubwa ya mwekezaji wetu katika kiwanda cha *Tanganyika Packers Limited* na wamebadilisha matumizi yake kuwa masuala ya shule. Je, Kiwanda chetu cha Shinyanga Serikali ina mkakati gani basi kukifufua kiwanda hicho kiweze kutumika badala ya *Tanganyika Packers Limited*?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga na Kiwanda cha Nyama cha Mbeya kwa sasa hivi viko katika mpango wa kubinafsishwa, na kwa hiyo viko chini ya *PSRC* na mwezi Mei, mwaka huu viwanda vyote viwili zabuni ya kutafuta wawekezaji ilitangazwa. Zabuni hiyo inafikia mwisho tarehe 25 Agosti, 2006. Kwa hiyo, tunatarajia wawekezaji watajitokeza wa kuvinunua viwanda hivyo kwa ajili ya usindikaji wa nyama. *(Makofi)*

Na. 410

**Mfumo wa Elimu Mjumuisho**

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iko katika hatua ya kuweka Mfumo wa Elimu Mjumuisho, ambayo itajumuisha wanafunzi wenye hali tofauti za kimaumbile kama vile Wasioona, Albino, Wasiosikia, na Walemavu wote wa aina zote watatakiwa kusoma katika darasa moja na wale wasio na ulemavu wowote chini ya Mwalimu mmoja na kwa kuwa mfumo huo unahitaji maandalizi ya kutosha kama vile shule, Vyuo vinavyomwezesha mlemavu kufikia huduma za masomo, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa vitabu vyenye maandishi makubwa '*large print'* na vitabu vya *braille* kwa wasioona:-

(a) Je, Serikali imefanya utafiti kuona kama kweli mfumo huo utajumuisha makusudio yote kwa vijana wetu kupata elimu kwa viwango vinavyotakiwa na vilivyo sawa kwa makundi yote?

(b) Je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na changamoto hizo kwa vitendo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu imefanya utafiti kwa kushirikiana na Mashirika na Taasisi zisizo za Kiserikali ili kubaini idadi na mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu. Mashirika na Taasisi zilizohusika ni pamoja na Kituo cha Habari juu ya Ulemavu, Chama kwa ajili ya Wenye Ulemavu wa Akili Tanzania na Huduma ya Watoto na Vijana Walemavu katika jamii.

Mheshimiwa Spika, utafiti umebaini kuwa:- - Watoto wengi wenye ulemavu hawajapatiwa nafasi katika shule zetu, kutokana na uhaba wa shule za vitengo maalum.

- Wapo wanafunzi wenye ulemavu katika baadhi ya shule za kawaida lakini hawahudumiwi ipasavyo kutokana na uhaba wa walimu waliopatiwa mafunzo na upungufu wa vifaa maalum vya kufundishia na kujifunzia.

- Kupitia tafiti hizo mapendekezo mbalimbali ya kuboresha utoaji wa Elimu kwa kundi maalum la wenye ulemavu yametolewa na yamezingatiwa katika maandalizi ya utoaji wa Elimu Jumuishi.

(b) Mheshimiwa Spika, mkakati wa kukabaliana na changamoto za uanzishaji wa Elimu Jumuishi umewekwa kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

- Kuendesha mafunzo ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Elimu Jumuishi kwa walimu, Waratibu Elimu Kata, Wakaguzi wa Shule na Maafisa Elimu wa Wilaya nchini kote. Mpaka sasa Halmashauri 37 zimepatiwa mafunzo hayo.

- Kusambaza michoro maalum ya majengo ya shule inayozingatia mahitaji ya wenye ulemavu.

- Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya wanafunzi wenye ulemavu pamoja na mtambo wa kisasa wa kuchapisha vitabu vya wasioona.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa

kuwa, Naibu Waziri amekubali kwamba katika suala la Elimu Maalum Walimu wote wapatiwa Taaluma ya Elimu ya Watoto wasiojiweza. Sasa je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia watoto wenye uwezo wa kusoma ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwafikisha mashuleni na kurudisha kutokana na ulemavu wao waliokuwa nao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, shule hizi ziko za aina mbili. Shule za msingi ziko chini ya Halmashauri kwa maana ya Tawala za Mikoa na Serikalil za Mitaa. Shule za Sekondari zinamilikiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Pamoja na hayo tunashirikiana katika utoaji wa taaluma na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Tatizo la wanafunzi wenye ulemavu ambao hawawezi kufika shuleni. Naomba lijadiliwe kwenye Halmashauri na kwa pamoja wanaweza wakapata suluhisho. Si rahisi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuweza kutatua matatizo haya ambayo kimsingi yapo chini sana kwenye jamii na Wizara iko mbali. Kwa hiyo, naomba Halmashauri na Kata zetu zijadili hili na zipate ufumbuzi. Sisi tutaendelea kutoa msaada kila itakapowezekana. *(Makofi)*

Na. 411

**Ujenzi wa Madarasa na Ununuzi wa Vifaa Muhimu vya Elimu**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. HERBERT J. MNTANGI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali Kuu imekuwa ikipata misaada mikubwa ya kuboresha Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu kutoka kwa wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Dini na watu binafsi na kwa kuwa, kwa kutambua umuhimu wao, Serikali ilikubali kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wadau hao gharama katika ujenzi wa madarasa na vifaa muhimu vya elimu:-

(a) Je, kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 na 2005/2006 Serikali imesaidia wadau gani katika Sekta ya Elimu ya Msingi na Sekondari na kwa kiasi gani cha fedha?

(b) Je, Serikali imesaidia watoto yatima wangapi wanaosoma katika shule za wadau hao au sekta binafsi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), iliahidi kusaidia shule zisizo za Serikali ambazo

haziendeshwi kibiashara na sio Seminari kwa kutoa Ruzuku ya Uendeshaji. Katika mwaka 2004/2005 na 2005/2006 haikutoa Ruzuku hiyo kwa sababu taratibu za kutoa ruzuku hiyo zilikuwa hazijakamilika na pia fedha zilizopatikana hazikutosha.

Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Serikali inaangalia uwezekano wa kutoa Ruzuku hiyo kwa kutegemea uwezo wa fedha utakaokuwepo. Aidha, Serikali imeendelea kusaidia Sekta binafsi zinazoendesha shule kwa kuandaa walimu wanaoajiriwa na sekta hiyo; ukaguzi wa shule na kutoa ruzuku ya kufidia gharama za Mitihani ya Kitaifa sawa na shule za Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *Girls Secondary Education Support (GSES)* wanafunzi wasichana 145 kutoka familia zenye kipato duni bila kulenga watoto yatima pekee wanagharimiwa elimu yao ya sekondari. Wanafunzi hao wanasoma katika shule mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali. Aidha, Serikali kupitia Mpango wa MMES inawagharimia wanafunzi wa aina hiyo Elimu ya Sekondari wanafunzi 45,000 wa Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Nne. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninalo swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Naibu Waziri ametaja Mpango wa MMES; na kwa kuwa Mpango wa MMES umeegemea zaidi kwenye misaada ya Wahisani. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kufanya maandalizi kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 ya kuweka Mfuko Maalum wa aina ya *Thinking Fund* ili wahisani hao wasitishapo misaada yao tufanye mradi huo uwe endelevu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, wazo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitoa la kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya kusaidia Elimu ya Sekondari ni wazo nzuri. Kwa sababu litaiwezesha Serikali kuwa na mpango wake wa ndani ili kuendesha Elimu hii ya Sekondari bila kutegemea wahisani. Hata hivyo, Wizara italitafakari na kuona uwezekano wa kuweza kufanya jambo la namna hiyo.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ningependa kuongezea tu kwa kifupi taarifa kutokana na swali la nyongeza la Mheshimiwa William Shellukindo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa MMES ulianzishwa kusaidia Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, lakini si kwamba ulikuwa unategemea wafadhili tu. Tumekuwa tukirudi kila wakati humu Bungeni kwamba ili Mpango huu uwe endelevu lazima utegemee nguvu za wananchi.

Pamoja na kwamba ni wazo nzuri la kuanzisha Mfuko Maalum na kadhalika, lakini bado kwa sehemu kubwa ili Mpango huu uwe endelevu itabidi hasa utumie nguvu za wananchi.

Kwa msingi huo namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote tusaidieni kuhimiza nguvu za wananchi kwa sababu mpango utakuwa endelevu tu ukitegemea nguvu za wananchi. Halafu Serikali isaidie pale ambapo inabidi kusaidia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ni nchi ya Kijamaa na kwa kuwa nchi zote za Kijamaa, jambo moja la msingi ambalo huwa zinafanya ni kuhakikisha kwanza Elimu ya Msingi ni *Universal Primary Education* kwa wote, Elimu ya Sekondari ni *Universal Secondary Education* kwa wote na ni lini Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakubali na kuanzisha Elimu ya Sekondari ambayo ni bure kwa kila mtoto wa Kitanzania? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, hata sisi nchi yetu ingefurahi sana kama tungefikia hatua ya kutoa Elimu ya Sekondari kuwa bure kwa wote. Ni jambo ambalo mimi naamini kabisa sisi wote humu tungependa kufikia hatua hiyo. Lakini ili tufikie hatua hiyo itabidi tujenge uwezo taratibu.

Ukiangalia hata matamshi ambayo ameyatoa Mheshimiwa Rais hivi karibuni ni kwamba lengo letu angalau mwaka kesho tusichukue chini ya asilimia 60 ya vijana wanaofaulu kuingia Kidato cha Kwanza. Kwa msingi huo tunaelekea huko. Cha msingi ni kama nilivyosema tuendelee kuhamasisha nguvu ya wananchi na Serikali isaidie ili hatimaye tujenge uwezo wa kuchukua vijana wote waingie katika Elimu ya Sekondari. Lakini naamini kabisa wazo ni nzuri likizingatiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kwa kunipa kibali cha kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa majibu haya yanayotolewa na Serikali hapa yamewahi kutolewa kwa muda mrefu. Nakumbuka Mheshimiwa Joseph Mungai alipokuwa Waziri wa Elimu na Utamaduni alikuwa akisema kwamba Serikali itaangalia uwezekano wa kusaidia Mashirika yanayoisaidia Serikali na kwa kuwa, kwa kweli jukumu la msingi ni la Serikali yenyewe na kuna Mashirika ya Dini. Kwangu mimi ninayo KKKT, nina *Vistation Secondary School* na kadhalika.

Je, Serikali haioni angalau kwamba kuna haja sasa ya kuanza kusaidia mathalan kulipia mishahara ya walimu na watumishi wengine wakati tunauangalia huo mpango unaozungumzwa hapa ili kuweza kuwasomesha watoto wengi zaidi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri ni vizuri tu kwamba Serikali ina nia ya kusaidia shule zisizo za Serikali ili nazo zisaidie pia kusaidia vijana wetu katika kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba hapo awali Serikali ilikuwa imefunga milango kidogo kwa watu binafsi kuanzisha shule.

Lakini baada ya kuona kwamba mzigo wa kuwaelimisha vijana ni mkubwa basi ikatoa wito kwa watu wote, Mashirika na Taasisi mbalimbali zichangie katika kutoa elimu nchini. Kwa msingi huo, Serikali ilitoa wito kwa kujua kwamba uwezo wake si mkubwa kiasi hicho cha kuweza kukidhi mahitaji ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge anapoomba kwamba Serikali isaidie kulipa mishahara ni sawa, lakini kama alivyojibu Naibu Waziri kwamba kila Serikali inapokuwa na uwezo itafanya hivyo, lakini kwa Taasisi ambazo haziendeshwi kidini na pia hazitozi ada kubwa. *(Makofi)*

Lakini mwaka huu wa fedha kama Mheshimiwa Mbunge alivyosikia kwenye hotuba ni kwamba tumeishatenga kiasi cha bilioni 250 kusaidia shule ambazo si za Serikali, lakini haziendeshwi kidini na wakati huo hazitozi ada kubwa sana. Mheshimiwa Mbunge kama anavyojua tayari tuna tatizo la shule nyingine zinatoza ada kubwa sana hasa itakuwa ni kichekesho hao wanaotoza ada kubwa sana, halafu Serikali tena inawaongezea. Kwa hiyo, ni wazo nzuri lakini linatakiwa liendeshwe kwa utaratibu wakati huo kuzingatia uwezo wa Serikali.

Na. 412

**Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya kero kubwa sana inayowasumbua wananchi ni msongamano wa wafungwa na mahabusu kwenye Magereza yetu nchini:-

(a) Je, hali halisi ya msongamano iko vipi kwa sasa?

(b) Je, ni makosa gani yanayowapeleka wahalifu wengi Magerezani?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza msongamano huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uwezo wa magereza yetu ni kuhifadhi wahalifu 22,699, lakini wahalifu waliokuwepo magerezani hadi kufikia tarehe 1 Juni, 2006 walikuwa ni

44,565 ambapo kati yao 23,829 walikuwa ni wafungwa na 20,420 walikuwa mahabusu. Takwimu hizi zinaonyesha ukubwa wa tatizo la msongamano wa wahalifu Magerezani. Msongamano huo ni mkubwa mara mbili kuliko uwezo wa magereza yetu.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 1 Juni 2006, makosa ya wizi, Unyang'anyi, mauaji, ubakaji pamoja na kuvunja na kuiba ndiyo yanayowapeleka wahalifu wengi yaani wafungwa na mahabusu zaidi magerezani. Aidha, wingi wa mahabusu nao unachochea na kuzidisha mno tatizo la msongamano magerezani, kwa mfano takwimu za tarehe 1 Juni, 2006 zinaonyesha kati ya watu 44,565 waliokuwepo magerezani 20,420 au asilimia 45.8 ya wote walikuwa mahabusu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kukabiliana na tatizo hili kama vile kutumia Kamati za Kusukuma Kesi Mahakamani (*Case Flow Management Committees*). Kukarabati na kujenga Magereza mapya, kuboresha uwezo wa Polisi katika kupeleleza makosa, kuimarisha Idara ya Mahakama kiutendaji hasa kuondoa upungufu wa Mahakimu na Majaji, kuendesha kampeni zinazolenga kupunguza uhalifu nchini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mbinu nyingine za kupunguza msongamano Magerezani ni pamoja na kuwaachilia wafungwa kwa kifungocha nje, kuwarekebisha wafungwa ndani ya jamii kwa kutumia Sheria ya Huduma kwa Jamii ya mwaka 2002 (*The Community Service Act. No.*2 *of the year 2002),* pamoja na msamaha wa wafungwa chini ya Sheria ya Bodi ya *Parole* ya mwaka 1994 *(Act. No. 25 of the year 1994)* pia kwa kutumia misamaha ya Rais.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia, Wizara ya Sheria na Katiba pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kutekeleza mikakati iliyotajwa hapo juu katika kukabiliana na kulimaliza tatizo la msongamano wa wafungwa Magerezani. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Ukienda kuangalia Magerezani hali ni mbaya sana. Kwa mfano, Magereza ya Mkoa wa Kigoma yana wafungwa takriban 1,486 na nusu ya wafungwa hao ni mahabusu na ndani ya hao wafungwa kuna mahabusu ambao ni wakimbizi na pia wafungwa wengine ni wakimbizi. Sasa nataka kujua ni kwa nini wakimbizi hawa ambao ni wahalifu tunaendelea kuwalisha, wanajaza msongamano kwenye magereza yetu. Kwa nini utaratibu usiwepo wa kuwarudisha kwao? Hilo la kwanza.

La pili, ningependa kujua ni makosa gani mengi zaidi yanawapeleka watu wengi Magerezani ili sasa kuwe na mkakati wa ku-*make sure* tunayapunguza hayo makosa?

**NAIBU WAZIRI WA WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna wakimbizi wasiopungua 1,077 kwenye Magereza ya Mkoa wa Kigoma. Lakini Itifaki ya Geneva yaani *the Geneva Conversation* ya mwaka 1951 inazikataza nchi zinazopokea wakimbizi kuwafukuza na kuwaondoa mpaka watu hao

wenyewe kwa hiari yao watakapoamua kurudi makwao baada ya hali ya usalama katika nchi hizo kupatikana.

Kwa hiyo, pamoja na nia ya kuondoa msongamano wa wafungwa katika magereza ya Kigoma, lakini bado Serikali yetu inabanwa na *Geneva Conversation* au kama nilivyosema Itifaki ya Geneva ya mwaka 1951 na sisi tulisaini mkataba huo.

Kuhusu suala la makosa yanayowapeleka wafungwa wengi Magerezani kama tulivyosema kwenye swali la msingi, makosa mengi sana ambayo yanawapeleka watu wengi Magerezani. Kwanza ni wizi ambapo tuna wafungwa zaidi 7,649, unyang'anyi wa kawaida tuna wafungwa na mahabusu wasiopungua 7,262, halafu mauaji wako wafungwa 6,828, kuvunja na kuiba wafungwa 6,200, kujamiiana wafungwa 3,856, kujeruhi wafungwa 2,313 na madawa ya kulevya ni wafungwa 1,427.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Waziri Chilligati ambaye alinikaribisha siku ya Jumapili kuambatana naye kwenda Isanga kusali pamoja na wafungwa wa kike na kiume.

Aidha, niipongeze Serikali ya Tanzania ya Awamu ya Nne kwa kweli kwa kuweza kupeleka vitu kama *TV* ambavyo nilishuhudia vikiwepo kwenye Magereza yetu, redio na magodoro nikiamini na vitanda vinapelekwa.

Lakini naomba kusema tu katika mahabusu waliokuwepo wanawake robo tatu ya wale wanawake walikuwa ni vichaa ambao wengine tangu mwaka 1999 wamepelekwa mara moja tu Mahakamani na hawajapelekwa tena na hawaelekei kutoka leo au kesho kwa sababu hata ukiwahoji walikuwa bado ni vichaa. Sasa nilikuwa najaribu kuuliza Serikali haioni sababu ya kuweza kufungua au wodi ya Mirembe kwa ajili ya watu hao. Maana yake kwa kuwaweka Magerezani wanaweka *conjunction* au kuwaachia warudi makwao.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya Wizara yangu nipokee pongezi alizotoa kwa juhudi alizoziona tunazofanya kuboresha hali ya Magereza yote nchini. Inatupa moyo na tutaendelea na programu ya kuboresha hali ya Magereza.

Kuhusu wagonjwa wa akili aliowaona pale Magereza juzi. Alivyosema ni sahihi na mimi nilikuwepo niliona. Niliongea na Mkuu wa Gereza pale kwa nini hawa wagonjwa wako pale kwenye Gereza badala ya kwenda kwenye Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Akasema alikuwa bado anasubiri nyaraka mbalimbali zitakazomwezesha kuwapeleka huko. Kwa hiyo, pale pale nilitoa maagizo ndani ya wiki hii hizo nyaraka zipatikane zinapotoka katika Magereza walikotoka na wiki hii hii waende hospitali kwa sababu mgonjwa mahali pake ni hospitali sio Gerezani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Nitoboe siri tu leo nilikuwa natoa nyongeza nyingi nyingi kwa sababu kesho nilikuwa sina maswali.

Kwa hiyo, haya yaliyosalia ndiyo maswali ya kesho. Mbinu hii inaitwa kubabiababia. *(Makofi)*

Sasa ninayo matangazo kwa furaha kubwa naomba niwatambue wageni kutoka Jamhuri ya Gambia. Wapo watatu hawa ni Watendaji Waandamizi wa Mfuko wa Hifadhi kama vile *NSSF* kwetu hapa Tanzania. Wanaongozwa na Ndugu Gabriel Mendi, Meneja Mwandamizi wa Mfuko wa Hifadhi wa Gambia. Pia Ndugu Sidi Kanji Meneja wa Mfuko huo na mwenyeji wao ambao ni Mkurugenzi Mkuu wa *Local Authority Provident Fund (LAPF)* Ndugu Bura yule pale. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wenzetu hawa Wagambia katika ule uelewa wa *Pan Africanism* walipata fununu kwamba jengo hili la Bunge limejengwa kutokana na fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwa hiyo, wamekuja kama wageni wa Katibu wa Bunge kujifunza ili na wao waweze kujenga ukumbi kule Gambia sijui kama utalingana na huu lakini tunawatakia kheri. *You are warmly welcome from the Sister Republic of Gambia. We are so happy to see you, we wish you well. I hope you have a very pleasant visit. Thank you very much.* Naomba kutambua kwa kuwepo kwa Bibi Ben Membe, mkewe Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Yule pale. Yule amevaa nguo yenye rangi nzuri. (*Makofi)*

Waheshimiwa Ndassa na Sakila wameniomba na Mheshimiwa Sakila huko safarini lakini wanawasiliana kwa karibu na mwezake kutoka Kwimba wameniomba nitangaze kuwapo kwa Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ambao wanaongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo anaitwa Anthony Nswabi na Katibu Mary Kapunda wale pale kwenye *Speaker's Gallery.* Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana Dodoma tunashukuru mmekuja kutuona hapa ukumbini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalillo ana wageni wake ambao ni Mheshimiwa Mussa Nkuyage Diwani wa Liwale Mjini ambaye pia ndiye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale na Msaidizi wake wa Mbunge. Katika ukumbi pia upande wangu wa kushoto tunao wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi ya Kikuyu Mjini Dodoma. Naomba msimame. Ahsante sana mara kwa mara nimesema tunawashukuru sana walimu mnafanya vyema kuwaleta vijana kuweza kuona jinsi demokrasia inavyoendeshwa ndani ya nchi yao. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lawrence Masha ameniomba nimtambulishe Bwana Juvenalis Matangili ambaye ni Mratibu wa Chama cha Wavuvi wa Tanzania *(TAFU)* yule pale. Karibu sana. (*Makofi)*

Sasa pale *VIP Gallery* mtaona kuna maua pale. Vijana wetu Mabinti wa Miss Utalii Tanzania kutoka Mikoa mbalimbali Pwani, Kilimanjaro, Ilala nyingine ni Wilaya nazitaja Kinondoni, wenyeji wa hapa Dodoma pamoja na Mratibu wa Miss Utalii anaitwa Azizi Chonya naomba asimame. Pia mpiga picha Halifa Mgeta na Rais wa Miss Utalii Tanzania Gideon Chipungahelo huyu ni maarufu sana huyu, yule pale. Naomba Ma-*miss* wote msimame ili Wabunge waweze kuwaona. Karibuni sana, karibuni sana tunawatakia mafanikio katika kuiwakilisha nchi yetu na wale ambao mtabahatika kwenda mbele ya

safari huko nje basi mkumbuke kwamba mnazingatia maadili mema pamoja na kuipa sifa nchi yetu ya Tanzania. Ahsante na hongera kwa ushindi mlioupata mpaka sasa. Ahsante sana. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kikao cha kwanza cha Kamati Kuu ya *CPA* Tawi la Tanzania kinafanyika leo saa 5.00 asubuhi Mwenyekiti mpya wa Tawi Dr. Raphael Chegeni tunaendelea kumpongeza. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hii ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya sio tu iko Serikalini hawa wamechaguliwa juzi leo tayari kuna kikao. Wajumbe wote Ukumbi Na. 227 Kamati Kuu ya *CPA* Tawi la Tanzania. Mheshimiwa Mohamed Missanga Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ameniomba nitangaze kuwa leo saa 5.00 asubuhi kwenye ukumbi Namba 231 Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu mkutane kwa kikao kifupi.

Mwisho, lakini sio mwisho kwa umuhimu Wajumbe wote wa Kamati ya Sherehe ya jana, ile sherehe kabambe wanaombwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama kukutana kwenye kikao choa wanakiita wao Kikao cha Tathmini ya Shughuli zao saa 7.00 mchana. Kulingana na hali halisi ya mafanikio ya hafla ya jana Mheshimiwa Spika ameamua ataungana nao kwenye kikao hicho ili kuweza kusema moja kwa moja maneno ya shukrani kwa niaba ya Wabunge wote. Nadhani wale ambao jana hawakuja hawakutokea pale walivyosimuliwa nadhani wamejisikia vibaya sana. Kwa sababu wamekosa mengi. Lakini kikubwa zaidi imeonyesha kwamba ndani ya Bunge hili tuna vipaji vya kila namna. Kumbe si suala la uwezo tu wa kushinda Uchaguzi lakini nani alimtazamia Mama Mahiza kuwa ni mwimbaji mahiri. Natoa mfano tu. Au Waziri Muhammed Seif Khatib anaimba utadhani hiyo ndiyo jadi yake kabisa. (*Makofi/Kicheko)*

Nashukuru kwa hayo. Baada ya matangazo hayo sasa tunaendelea na *Order Paper.* Katibu endelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2006/2007 Wizara ya Fedha

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. KILONSTI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii iliyoko mbele yetu kama mchangiaji wa mwisho katika Bajeti hii. Naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Spika. Lakini nikupongeze sana kwa jinsi ulivyoendesha vikao vya Bunge letu la Bajeti toka mwezi Juni mpaka sasa nafikiri tunastahili wote Wabunge kukupongeza sana kwa jinsi ulivyoliendesha kwa *Speed and Standard. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri wote pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii, wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana katika Wizara hii. Nawapongeza sana na mimi naunga hoja mkono. Lakini pia ninawapongeza *TRA* kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya. Kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato ya nchi

hii ambayo sasa yamefikia zaidi ya shilingi bilioni 220. Tunastahili kuwapongeza sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inao uwezo mkubwa wa kukusanya kodi kubwa na mimi najua huko ndiko tunakokwenda maana tukilinganisha nchi yetu na nchi kama Uganda bado sisi tuna nafasi kubwa ya kukusanya kodi kubwa zaidi kuliko hata Kenya. Mimi nina imani uchumi wetu umekuwa ukienda vizuri, nina imani uchumi huu utakwenda vizuri na utaendelea vizuri na hatimaye tutaona yale mapungufu ambayo yamejitokeza ndani ya uchumi huu yataanza kujirekebisha pole pole na ufanisi tutaanza kuuona vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze neno moja jana Waheshimwa Wabunge walipokuwa wanachangia hoja hii wako wengine walichangia hoja ya ukosefu wa vyombo vya fedha katika sehemu zao za uwakilishi. Mimi hili naliunga mkono kwa sababu mimi natoka Manyovu, Wilaya ya Kasulu, na kutoka Manyovu mpaka Kasulu ni karibu kilomita 40. Hili ni eneo la ujambazi mkubwa sana, wafanyabiashara wanapotoka Manyovu wanapeleka fedha Kasulu, wengi wao wamekuwa wanatekwa, mabasi yale yamekuwa yanatekwa njiani. Wamekuwa wananyang'anywa mali zao, wengine wanapeleka fedha Benki, wengine wanakwenda kununua vifaa kufanya biashara, kununua biashara mjini wanatekwa na fedha zao zinaibiwa na kupata hasara kubwa.

Kwa hiyo, vyombo vya fedha kama tungeweza kuwekewa Benki basi ukosefu unaojitokeza au upungufu unaojitokeza wa watu wetu kunyang'anya mali zao usingejitokeza. Lakini kingine ni kwamba hatuwezi kuweka ulinzi kila mahali maana Polisi hawatoshi na kwa hiyo ni vizuri kama hizi huduma zingeweza kusogezwa karibu na watu. Hilo ni eneo moja ambalo nilifikiri nilitaje tu kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ninalotaka kulizungumzia ni juu ya mwenendo mzima wa uchumi wa nchi yetu. Tumekuwa tunazungumza juu ya riba kubwa katika Mabenki. Lakini tumekuwa tukizungumzia pia gharama nyingi zinazotozwa na Mabenki kiasi kwamba mtu anaogopa kuwekeza fedha zake ndani ya Benki. *Commission* mteja anazotozwa ndani ya Benki na riba inayokulipa Benki ni vitu ambavyo havina uwiano. Mimi nafikiri ni wakati muafaka wa Serikali kujielekeza kwenye tatizo hili na kuanza kuziangalia hizi gharama ambazo wateja wanaopeleka fedha zao Benki wanazotozwa na Mabenki. Hata *interest* ukilipwa, *interest* ya shilingi 50 nayo inatozwa kodi.

Ukipeleka fedha ukaziweka ndani ya Benki leo labda shilingi 2,000 lakini ukatoa *cheque* ya shilingi 1,000 iko kodi inatozwa. Ukifanya sijui kitu gani upeleke pale iko *commission* Benki inakutoza kwa kufanya hilo jambo kwa kukufanyia wewe shughuli hiyo tena shughuli ya gharama ndogo sana. Sasa haya yote ni gharama kwa mteja na mteja hawi *motivated* kuweka fedha zake ndani ya Benki.

Sasa hili suala la *interest rate* ambalo kwanza ni bado *rate* ziko juu. Ni kweli zimeshuka lakini badoziko juu na mimi ningeomba ziteremke zaidi. Maana *economy* ambazo zinatuzunguka zote *interests* zao ziko chini. Kenya kwa wale wanaoweza ku-*negotiate* na wale wanaochukua fedha nyingi *interests rate* zao zimeshashuka chini ya

7%. Lakini sisi bado Mbunge ambaye anajulikana yeye ndiye ana kazi nzuri, ana kazi ambayo anaweza kukatwa fedha kwa mara moja na wakafanya faida bila jasho kubwa ndiye anasema 16%. *(Makofi)*

Lakini ukienda wewe kama mfanyabiashara mdogo mdogo unayetaka kuongeza juhudi yako ya kufanya kazi unaambiwa 18% mpaka 20% bado inafika. Sasa kiwango hiki kingepungua *in order to motivate* wafanyabiashara wadogo wadogo waweze kuchukua fedha ndani ya Benki na wafanye kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Ukienda kwenye *NGO's it is worse*. *It is Microfinance Organizations* ni mbaya zaidi kwa sababu utaratibu wao pia ni mbaya, hauwezi kumfanya huyu mfanyabiashara mdogo mdogo siku moja aje a-*graduate into a business operator* mzuri, haiwezekani. Kwa sababu ya riba anayotozwa kwenye *Microfinance Operations* zote zinazofanyika nchini. Kwa hiyo, mimi ningeomba riba zote ziangaliwe.

Mheshimiwa Spika, la tatu ninalotaka kuzungumzia ni kazi za madini. Migodi yote hapa nchini inaendeshwa na *foreigners*. Kazi zote za ununuzi wa vito hawa *foreigners* wanafanya wenyewe. Wewe mtu mdogo ukianzisha mgodi na uka-*employ technical staff* unalipa *withholding tax*. Hawa wakubwa hawalipi *withholding tax. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanachofanya ni kwamba wanaleta *staff* wao kutoka nje hata wanaokuja kufanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na watu wetu Watanzania. Matokeo yake ni kwamba *operations* zinazofanywa ndani ya viwanda kwanza hatuzijui na hatuwezi kufuatilia maana hatujui kinachoendelea. *(Makofi)*

Lakini tatu ni kwamba kodi hatuwatozi na ni vizuri utaratibu huu ukachunguzwa vizuri zaidi tukajua ni namna gani tunaweza tukarekebisha baadhi ya mambo katika sekta ya madini ili Serikali iweze kupata kodi zaidi, iweze kupata fedha zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua zipo sehemu ambazo nchi ingeweza kufanya vizuri zaidi. Sisi ndio *the only producers* wa *Tanzanite* katika dunia hii. Tungekuwa tunataka kuwa *proud* na hii *Tanzanite* tungeiangalia vizuri, mikataba tunayosaini na wawekezaji wanaokuja kwenye hii kitu *Tanzanite* tungekuwa *very carefull* nayo na hapa ndipo tuna uwezo wa kuongeza bei kwenye *Tanzanite*. Maana hatuna mshindani dunia nzima. Kwa hiyo, tungepata fedha zaidi kwenye *Tanzanite*. *(Makofi)*

Lakini huko nje mimi nimekwenda *South Africa* nimekuta inauzwa si kama zao la Tanzania ni kama zao la ile Kampuni ya *Afrigem* ya *South Africa*. Nimekwenda Brazil nimeikuta inauzwa kama zao la Afrika ya Kusini maana zile *invoice* zinatoka Afrika ya Kusini ndiyo zinakwenda Brazil. Nilifikiri hili niliseme. Silisemi hili kwa maana ya Tanzania kutotaka kuwa *competitive,* tunataka kuwe *competitive* hata kwenye sekta ya madini. Lakini kuna *avenue* nzuri ambayo nchi hii inaweza ikapata fedha vizuri zaidi na ikafanya kazi nzuri zaidi bila ya uwezo wake wa ku-*compete* nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, la nne, ubinafsishaji. Kaka yangu Dr. Juma Ngasongwa alitueleza vizuri utaratibu wake ni mzuri sana unaofanywa. Lakini naomba nizungumzie tu kidogo ubinafishaji wa *NIC. NIC* hivi sasa inabinafsisha hatujaliona tamko.

Lakini maneno yaliyoko ni kwamba *preferred candidate* katika wale waliotenda kununua au kuchukua *NIC* ni mtu aliye tenda shilingi bilioni 3. Lakini kama hii ni kweli mafao ya wafanyakazi wa *NIC* peke yao yanafika shilingi bilioni 5.

Wewe unataka kuibinafsisha kwa shilingi bilioni 3**.** *Assets* za *NIC* ni zaidi ya shilingi bilioni 23. Nyumba mojawapo ya *NIC* majengo ya *NIC* ni shilingi bilioni 11 *valuation* yake iliyofanywa na wataalam. Leo unataka kutoa Shirika lote na majumba yote kwa shilingi bilioni 3. Hii hatutaelewa, wala hatutakubali ndani ya Bunge hili. Kama wanashindwa kupata mwekezaji mimi ninayo hoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mnisikilize vizuri. Hoja yangu mimi naomba sisi Wabunge na Bunge lenyewe tutende kununua *NIC.* Nataka tuombe kununua *NIC* tuichukue. Kisha baadaye tuta-*float shares,* watu wanunue *shares*, Watanzania watanunua *shares. (Makofi)*

Uwezo wa *NIC* kuzalisha ni mpaka shilingi 96 bilioni kwa mwaka *in premiums* wanazopata, biashara wanayofanya kwa mwaka. Inawezekana matumizi yake ni makubwa, lakini sio kiasi cha kuitupa kiasi hicho. Ninamwunga mkono yule mtu aliyesema jana kwamba *ATC* wamechukua Wazungu tuna ubia nao. *(Makofi)*

Lakini bado kuna hasara kubwa inayotokea pale tunachukua fedha tunawapa. *NIC* ni Waswahili na mbona hatuwapi hata senti tano. Hoja hii naomba ifanyiwe kazi. Waheshimiwa Wabunge tuombe kuchukua *NIC* sisi Wabunge kwa pamoja. Mimi najua tutakubali kisha tuta-*float shares* wanaohitaji tutaungana nao *NIC* na tutaajiri wataalamu wako duniani, teknolojia ni kitu kinachonunuliwa na sisi tunaweza kukinunua popote duniani. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawili ya mwisho ni yale yanayohusu wafanyakazi wa *Community.* Mfanyakazi wa *Community* jamani hii kelele mbona imekuwa nyingi na kubwa sana? Tupate maelezo sahihi kwa nini hawalipwi? Tuliletewa mpango hapa wa *phasing* ya malipo wanayostahili kupata, leo bado machungu ni yale yale kuna ambao hawajalipwa mpaka leo. Wastaafu nao wa nchi hii wananung'unika, *Treasury* nayo haiwafanyii haki. Ebu tupate maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameandikiwa barua na wastaafu wa Dodoma. Ebu tuelezwe hawa wazee ndio hazina ya Taifa hili, lakini leo hawa wazee inaonekana hatuwajali wanasema tunanyanyaswa, tunadhalilishwa, hatusikilizwi tuwajali hawa wazee ndio hazina ya Taifa hili na sisi wote tulioko humu huko ndiko tunakokwenda. Tuwajali jamani hawa wazee wetu. (*Makofi)*

Juzi nilisoma kwenye gazeti mtu ameenda Hazina kudai hela yake amefia pale pale. Jamani hatuoni hata huruma? Kama nchi tuone haya wenzao wameshalipwa miaka

20 iliyopita. Leo bado sijui waliokufa ni wangapi, lakini ni wengi ambao wamekufa, wamepoteza maisha yao *they have not enjoyed the benefit of their labour.*

Mheshimiwa Spika, niliona niyaseme haya ili kusudi Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atupe majibu, atueleze wastaafu wetu kwa nini wanung'unike akazungumze nao hawa watu wa *Community* atoe maelezo sahihi. Najua fedha zimetengwa, lakini zimetengwa kwa kiwango gani wote watapata au hawatapata yako matatizo gani. Atueleze yako matatizo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye ufafanuzi mzuri kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo: -

(i) Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya huduma za kiuchumi na kijamii ambazo ni barabara, maji, elimu ya msingi, sekondari na vyuo, pia ujenzi wa nyumba za walimu uzingatiwe.

(ii) Pamoja na kwamba *TRA* wanafanya kazi nzuri ya kukusanya mapato, juhudi iongezwe ili kukusanya mapato ya kutosha ili Serikali iweze kutekeleza miradi ya maendeleo bila kukwama. Pia mazingira ya kufanyia kazi yaboreshwe.

(iii) Pamoja na kwamba kima cha chini cha mshahara kimepanda, bado kima hicho ni kidogo, Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi hasa wa kima cha chini kwani gharama ya maisha imepanda.

(iv) Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua kali kwa wale wote wanaokwepa kulipa kodi. Je, katika mwaka wa fedha 2005/2006 ni watu/wafanyabiashara wangapi walikwepa kulipa kodi na hatua gani zilichukuliwa?

(v) Kwa kuwa Halmashauri nyingi zinafunga mahesabu kwa kuchelewa na hii inasababishwa na upungufu mkubwa wa wahasibu, je, Serikali imeweka mikakati gani ya kusomesha wahasibu wengi na kuwapeleka katika Halmashauri hizo ili kuboresha udhibiti wa fedha katika Halmashauri.

(vi) Je, Serikali ina mipango gani ya kuwaendeleza wahasibu waliopo kitaaluma ili kufikia kiwango cha *CPA* kuliko hali ilivyo sasa?

(vii) Misamaha ya kodi idhibitiwe ili kuongeza mapato Serikalini.

(viii) Kwa kuwa kulikuwa na mpango wa kujenga ofisi ya *TRA* Wilaya ya Mpwapwa na kiwanja kilikwishaandaliwa, je, ni sababu gani za msingi zinazofanya ofisi hiyo isijengwe hadi sasa?

(ix) Kwa kuwa mikopo ni haki ya wananchi katika vyombo vya fedha, je, Serikali itakubaliana nami kwamba masharti na riba kubwa ni kikwazo kikubwa cha kupata mikopo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, kuna adha na matatizo wanayopata watumishi wanaofanya kazi walioko vijijini mfano:-

(i) Maafisa Ugani wanaofanyia kazi kwenye vijiji vya Ngwala (Chunya) umbali wa kilometa 215 ili waje kwenye tawi la Benki Chunya hutumia siku 12 kwenda na kurudi kituoni.

(ii) Walimu kwenye vituo katika vijiji vya Namkukwe, Magamba na Gua umbali wa wastani wa kilometa 120 mpaka 200 hadi Chunya. Nusu mwezi hutumika kufuata mishahara.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iwapunguzie adha hiyo inayowapata watumishi hao angalau kwa kuanzisha *Mobile Bank.*

Mheshimiwa Spika, posho ya maafisa wastaafu hasa wale waliostaafu miaka kabla ya 2000 ni ndogo sana, nashauri Wizara iliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la upatikanaji wa malipo ya pensheni wakati wanapostaafu. Wanahangaika sana, wengine huchukua miaka miwili kabla hawajalipwa malipo hayo. Mfano kwenye majeshi na upande wa walimu, malipo yao hucheleweshwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya bima, katika Wilaya ya Chunya walimu hawajalipwa tangu bima hizo ziive miaka miwili iliyopita. Inadaiwa fedha zilimalizika kabla walimu wa Wilaya za Ileje na Chunya hawajafikiwa. Nashauri Wizara iwalipe bima zao walimu hao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, awali nimpongeze Mheshimiwa Zakia Meghji na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Abdisaalam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Ndugu Mgonja kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya tangu awamu ya tatu.

Pili, napenda kuchangia katika maeneo mawili, kwanza ni *TRA* na mfumo wa mapato ya Serikali na pili Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* kuwa Chuo Kikuu kamili.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na *TRA,* naipongeza sana Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa kuongeza makusanyo ya kodi. Kwa miaka ya karibuni *TRA* imekuwa ikiongeza ukusanyaji wa kodi mwezi hadi mwezi. Katika kipindi cha miezi michache iliyopita, *TRA* imeongeza mapato toka 160 bilioni kwa mwezi hadi zaidi ya 200 bilioni kwa mwezi Juni 2006 na taarifa za vyombo vya habari ni kuwa mwezi Julai, 2006 makusanyo yamefikia 220 bilioni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado *TRA* inaweza kukusanya zaidi ya makusanyo ya sasa kwani, kuvuka malengo mwaka hadi mwaka kwa miaka minne mfululizo ni dalili kwamba malengo yako chini. Nchi nyingi za jirani, zenye uchumi kama wetu zinakusanya zaidi na kuna mianya kadhaa ya ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya misamaha ya kodi bado ni makubwa, yaweza kuwa ni kwa kuzidiwa ujanja na wenzetu, hasa wanaoomba *exemptions* kwenye *projects* au kwa makusudi katika msingi mzima wa ufisadi.

Mheshimiwa Spika, hivyo kuna mambo mawili ninayopanga kuyasema kuhusu *TRA* yakiwemo wigo mdogo wa kodi na mfumo wa kodi unaomkandamiza mfanyakazi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba *TRA* iangalie jinsi ya kutatua tatizo la wigo mdogo wa kodi unaojikita katika sekta iliyo rasmi pekee, yaani *investment business and employment incomes,* unaosababisha *disincentives on voluntary compliance* wafanyabiashara wanaamini kukwepa kodi ni kuongeza faida, hivyo kila siku wamekuwa wakitafuta mbinu mpya za kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, *unfair distribution of the tax burden,* wananchi wa kawaida hasa waajiriwa katika sekta rasmi wanalipa kodi kubwa sana kuliko wengine katika nchi *PAYE* iko juu, lakini pia wanalipa *VAT* kama sehemu ya *Indirect tax, High tax rates PAYE* na *VAT rates* ziko juu kuliko nchi nyingi jirani.

Mheshimiwa Spika, kodi kwenye *basic inputs* kama mafuta inaongeza gharama za uzalishaji hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa sekta nzima ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linaloisibu *TRA* na Mapato ya Serikali kwa ujumla ni mianya kadhaa ya ukwepaji kodi. Naomba *TRA* irekebishe mianya katika maeneo yafuatayo:-

(i) Wafanyakazi Watanzania wanaofanya ofisi za kibalozi hawalipi kodi kwa mtindo wa *PAYE.*

(ii) Serikali haina rekodi sahihi, kwani hakuna vitambulisho vya uraia ambavyo vingeweza kusaidia kujua nani yuko wapi!! Wengi hawalipi kodi! (Zaidi ya shilingi 500 milioni ziada kwa mwezi inaweza kukufanya toka chanzo hiki).

(iii) Watanzania wengi walioko nje ya nchi, Serikali haina utaratibu wa kuwa *trace* na kujua mapato yao.

(iv) Vitambulisho vya uraia (zaidi ya shilingi bilioni moja kwa mwezi inaweza kukusanya toka chanzo hiki).

(v) Utaratibu wa ku-*trace* mapato yote ya mtu, hasa *secondary empoyment arrangement* haifanyi kazi.

(vi) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa unamtaka mwajiriwa amjulishe mwajiri wake ajira zingine alizonazo na mapato anayopata. Utaratibu huu ni hafifu sana, kwani waajiriwa wengi hawafanyi hivyo, waajiriwa wengi hawataji mapato yao sahihi ya ajira zao za pili na utaratibu wa *TIN* ungesaidia (zaidi ya shilingi 300 milioni ziada kwa mwezi inaweza kukusanywa toka chanzo hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kuhusu *TRA* naomba kuishauri *TRA* katika kuongeza wigo wa kodi, iangalie maeneo mapya ya kodi. Kwa kuwa *TRA* inawataalamu, mimi natoa kama *hints* ili wazifanyie kazi, hata hivyo, niko tayari kushirikiana na *TRA* kujadili na kuweka mkakati wa namna ya kuyafikia maeneo hayo *of course on consultative basis.*

Mheshimiwa Spika, tatizo letu kubwa katika mapato ni udhaifu katika matumizi ya utambuzi wa walipa kodi na idadi ndogo ya watu waliojiandikisha kama walipa kodi yaani wenye *TIN,* wajasiriamali wengi hawana *DJs, MCs,* wapambaji kwenye sherehe na kadhalika wengi wao hawajaandikishwa kibiashara na hivyo mapato yao hayalipiwi kodi. (Kuna zaidi ya shilingi 100 milioni ziada kwa mwezi toka chanzo hiki).

Mheshimiwa Spika, pia kutoka kwa wasanii muziki wa kizazi kipya, muziki wa injili, waigizaji (Kuna zaidi ya 15 bilioni kwa mwaka ziada toka chanzo hiki) *TRA* inatakiwa udhibiti uingizaji wa *empty music storage devices, production and distribution of CD, VCD, DVD, Audio tapes* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutoka kwa wanamichezo, mashindano ya ulimbwende (kuna zaidi ya shilingi 500 milioni kwa mwaka ziada toka chanzo hiki).

Mheshimiwa Spika, wamachinga na mamalishe hawajawekewa utaratibu wa kuwafanya waeleweke na walipe kodi, japo kidogo kwa kila mmoja, lakini kwa kuzingatia wingi wao, kodi kubwa inaweza kupatikana kwenye eneo hili. (Mfano, Dar es Salaam pekee inakisiwa kuwa na machinga zaidi ya 100,000, kama kila mmoja atalipa shilingi 10,000 kwa mwezi, kodi ingekuwa shilingi 1,000,000,000 kwa mwezi)!

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ninalotaka kuchangia ni kuhusu Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* kuwa Chuo Kikuu kamili. Chuo hiki kilianzishwa kwa

Sheria ya Bunge ya mwaka 1972. Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na jitihada za kukifanya chuo hiki kuwa Chuo Kikuu kamili. Lakini jitihada hizi ambazo kwa kiasi kikubwa ni msukumo wa wadau na uongozi wa chuo pekee, Serikali kwa maana ya Wizara imekuwa kikwazo. Haijakamilisha utaratibu wa kuleta Muswada Bungeni wa kubadili sheria ya Chuo hicho, sijui tatizo ni nini.

Ningependa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alishughulikie tatizo hili kwani linavunja moo sana wahadhiri na wengi wao wamekuwa wakihama chuo hicho baada ya kumaliza masomo ambayo wamekuwa wakisomeshwa na Chuo, hasa *Ph.D.* katika jitihada za chuo na wahadhiri wake kupata sifa za kuwa chuo kikuu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja, nampongeza sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu akiwemo Joyce Mapunjo kwa usimamizi mzuri wa Wizara pamoja na asasi zilizo chini ya Wizara. Sisi Wabunge tunamuunga mkono Mheshimiwa Waziri, hivyo tunawaomba wasaidizi mlio chini yake kumsaidia Waziri kwa manufaa ya nchi yetu.

Najua Mheshimiwa Waziri ni mtu makini, ni mwanamke aliyetulia, mwenye msimamo, anayeweka maslahi ya nchi mbele, lakini namwomba awe makini katika kutekeleza majukumu yaliyoko mbele yake, dude hilo (Wizara) ni kubwa, lina mambo mengi, kuna wajanja wengi hivyo Waziri usipokuwa makini, wajanja watakuzunguka kwani macho yao yote ya fedha yako Wizara yako.

Naomba nami niungane na Watanzania kwa kuwapongeza sana *TRA* kwa kuitikia ombi la Mheshimiwa Rais la kukusanya zaidi ya bilioni 200, nawapongeza sana. Nawatia shime waongeze bidii ili wakusanye bilioni 300 kwa mwezi, wakiamua wanaweza hii ni kutokana na timu ya *TRA* inayoongozwa na Kamishna Mkuu Ndugu Kitilya.

Mheshimiwa Spika, bila pesa hakuna maendeleo, yale yote tuliyoyaahidi kwenye Uchaguzi Mkuu (Ilani) bila makusanyo ya kutosha ni kazi bure, hakuna kitakachotekelezwa. Naomba Serikali, wakubwa kutoiingilia *TRA* kwa maana ya kuandika vi-*note* na maagizo ya simu msaidieni huyo ni ndugu yetu, tukifanya hivyo tunakuwa tunawakatisha Tamaa. Tuwaache huru ili tuwahoji kwa kushindwa kufikia lengo.

Naiomba Serikali imalize tatizo la wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pia pale Wizarani huwa kunakuwa na mrundikano wa wazee jengo la Mhasibu Mkuu, itafutwe njia mbadala.

Naiomba *TRA* inisaidie na kunihakikishia kuhusu uhalali wa kupewa mradi wa leseni ya udereva kutumia *computer* iliyopewa Kampuni ya *Face Technologies* ya Afrika Kusini Mkataba uliotiwa saini tarehe 17 Januari, 2006 wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 6.27, je, kampuni hiyo inao uwezo? Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba thamani ya mradi itakuwa dola za Marekani milioni 6.27? Je,

tumejiandaa vipi ili yasije yakatokea kama yale ya Uganda na Zambia? Je, Watanzania wametayarishwa vipi, ikiwa ni pamoja na kupewa mafunzo ya kutosha?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara imeshafanya utafiti wa kutosha kama bado isingekuwa busara mradi huu ukasimamishwa ili kuwashirikisha wadau?

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni nzuri sana nampongeza, naomba utekelezaji wa yale yote yaliyoainishwa kwenye kitabu. Naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara ya Fedha baada ya Waziri kuwasilisha hotuba ya bajeti hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi yanayohusu wastaafu wa mikoani kwamba wamekuwa wakihangaika kupata malipo yao kutokana na kukosa nauli ya kufuata malipo hayo Dar es Salaam kwamba hata wanapofanikiwa kupata nafasi ya kufika Wizarani na *Section* ya *Pension*, wamekuwa wakihangaika na wakati mwingine kulazimika kurudi bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba watu wenye madai ya namna hiyo ni wengi kiasi kwamba hawawezi kuhudumiwa mara moja. Nashauri Wizara ipange utaratibu wa kuwa wakiandaa malipo na kuyatuma Mikaoni (Makao Makuu), mahali ambapo itakuwa ni rahisi kwa watumishi hao kupata huduma hiyo bila kukopa nauli za kuwafikisha Dar es Salaam. Athari ambazo zimekuwa zikiwapata ni kukopa nauli pamoja na adha ya kuishi kwenye nyumba za kulala wageni.

Mheshimiwa Spika, kwa kutatua hilo tatizo la wastaafu litafurahiwa na wastaafu wengi na kuiepushia lawama Wizara ambayo kwa hakika inajitahidi kwa kiasi kikubwa kuwahudumia watu wa aina hiyo. Baada ya kutoa ushauri huo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana Wizara kwa kazi ngumu za kila siku. Naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, urasimu wa malipo ya fedha za watumishi wastaafu uondolewe mara moja na pili, mapunjo ya watumishi wastaafu yalipwe.

Mheshimiwa Spika, tatu, utaratibu wa kulipa kila baada ya miezi sita utazamwe upya ili angalau iwe kila mwezi ama mara nne kwa mwaka.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia machache kuhusu Wizara hii na hasa yanayolenga Jimbo langu la Bukene. Awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri, kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye majimbo mengine Tanzania nzima nina wastaafu waliokuwa wanafanyakazi Shirika la Reli, wengine wako hai wengine

wamefariki na warithi wao wanasubiri kulipwa kwa muda mrefu sana sasa. Hawa ni wafanyakazi wa Reli, Stesheni ya Bukene, Mahene, Igusule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, majina yametoka kwenye magazeti yapo, wamefuatilia Tabora na wengine Shinyanga, *in vain*. Naomba wafikiriwe na walipwe mapema iwezekanavyo ili nao wajikwamue katika umaskini uliokithiri. Safari za kwenda Tabora/Shinyanga ni gharama sana kwani kila kukicha nauli zinapanda. Hivyo basi, naomba wapunguziwe ugumu wa maisha kwa kulipwa haki yao.

Mheshimiwa Spika, kuna wafanyakazi wa idara zingine mbalimbali yaani Idara ya Mahakama, Idara ya Maji na kadhalika, naomba sana walipwe. Wengine wamekwisha kufa, hivyo naomba walipwe warithi wao ili ziwasaidie. Sasa alipokuwa hai aliweza kudunduliza watoto na mama yao wakala. Sasa hayupo amefariki, waliobaki ni kama wanapewa adhabu mara mbili yaani kufiwa na kuchelewa kulipa haki yao ya mirathi.

Mheshimiwa Spika, chonde chonde naomba walipwe ipasavyo. Kama tulivyoambiwa tulete majina yao, basi nami nitakukabidhi majina yao au wakati Bunge la Novemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoambiwa tulete majina basi nami kama wenzangu naomba kukaribisha taasisi za fedha katika jimbo langu la Bukene.

Mheshimiwa Spika, taasisi hizi za fedha kama *CRDB Bank*, imejikita sana katika makao makuu ya Mkoa. Kwa misingi hiyo naomba ifike Makao Makuu ya Majimbo yetu kama Bukene. Benki kama *NMB* zinaishia Wilayani, kwa misingi ile ile naomba zifike kwa Makao Makuu ya Majimbo kama Bukene.

Mheshimiwa Spika, nakaribisha taasisi hizi na zingine za fedha sababu ninazo, mtiririko wa fedha upo hasa wakati huu wa mauzo/manunuzi ya biashara ya mpunga/mchele, tumbaku, pamba, karibuni sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho lakini katika umuhimu naomba ushirika ufanye kazi ipasavyo ni jambo la kushangaza wananchi wangu wa Jimbo la Bukene wamefuatilia wee ili waanzishe *SACCOS*, lakini idara ya Ushiriki wa Nzega, ni mangimeza hawaendi na inasikitisha kuona nia ipo lakini hakuna *SACCOS,* hivi hawa wenzetu wanakwendaje sio ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya kwa nini? Wako nchi gani au dunia ipi? Kwa kupitia kwako naomba wabadilike waende kuanzisha *SACCOS*. Mimi nimekwishahamisha wanachohitaji ni bwana/bibi ushirika kuwapa semina na kuwaandikisha ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo hapo juu naunga mkono mia kwa mia hoja iliyoko mbele yetu.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na ninaupongeza uongozi wa Wizara hii wote kwa hoja nzuri.

Kusudi langu ni kuomba mambo mawili, kwanza, kusogeza huduma za benki karibu na Wilayani ili watumishi waweze kupokea fedha zao benki ili kutimiza azma ya kupokelea mishahara benki. Wilaya zingine hazina benki kama Wilaya ya Ruangwa, Mkoani Lindi haina benki, utaikuta Wilaya ya Nachingwea kilometa 40. Wizi utatokea na uporaji na pili ni kuhusu *SACCOS*. Wilaya zingine zinahitaji kupewa semina za kuanzisha *SACCOS*. Elimu hii ya *SACCOS* baadhi ya Wilaya hazijui. Tunahitaji waelimishwe kwa njia ya semina elimu ya *SACCOS* ni muhimu kwanza kabla ya kuanzisha *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, narudia tena ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Zakia Meghji, kwanza kwa kuwa mwanamke wa kwanza kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha, lakini pia kuwa kwa kazi nzuri anayoifanya tokea ateuliwe kuwa Waziri wa Fedha. Nawapongeza pia Naibu Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa Mkullo, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Serikali kwa kurudisha malipo ya pensheni kwa watumishi waliochukua pensheni ya mkupuo, pensheni yenyewe kwa maana ya viwango vya sasa vya pensheni ni vidogo yaani shilingi 20,000/= kwa mwezi. Naiomba Serikali iboreshe kiwango cha chini cha pensheni kwani kilichopo kimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu ilifanya kazi nzuri ya kuwalipa baadhi ya wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba baadhi bado wanalalamika hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, malalamiko yaliyopo ni kuwa Serikali kutoyapa mafao thamani yake halisi *(Real Value)* wakati wa kuyalipa na Serikali haikulipa madai ya pensheni ya ziada/nyongeza *(Additional Penshen).*

Kimsingi baada ya kukubaliana kutoa kesi Mahakamani, Serikali ilipaswa kuwalipa wastaafu kulingana na *Deed of Settlement (DEED)* jambo ambalo halikufanyika, kulingana na madai yao.

Mheshimiwa Spika, hawa wastaafu wamefanya kazi kwa uadilifu na uaminifu hivyo wanastahili kutendewa mema.

Mheshimiwa Spika, hivyo naomba Wizara chini ya Waziri mahiri na wasaidizi wake mahiri wafike mahali wamalize tatizo hili la wastaafu wa *Community.* Sifa ya Serikali ya CCM ni kuwaondolea kero wananchi pamoja na wastaafu hawa. Hivyo Wizara ifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanaza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wake na watendaji wengine kwa kuandaa bajeti nzuri na kuiwasilisha vizuri na jinsi mnavyoendesha Wizara kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *TRA* kwa jitihada kubwa za makusanyo na jinsi yalivyoongezeka, pia nawapongeza kwa mabadiliko yanayofanywa kutumia sera ya *IT (computerisation).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Idara hii iongezewe uwezo ili *Audits* zisichelewe sana kwani ni za msaada zinapokuwa mapema na idara iwe na timu ya kutosha na *well trained*. Kiukaguzi uendelee kuwa wa kufaa na wa kina zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa *Pension Funds,* Wizara iweke taratibu nzuri za kusimamia *Pension Fund* zile ambazo ziko chini ya Wizara. Kwa sasa yako mengi yametokea na yanasemwa juu ya *Pension Funds* zetu zilizo chini ya Wizara zikisimamiwa vizuri itapunguza maneno.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kufuta kodi za adha kwa wananchi (kodi hizo zilikuwa kero) na naishukuru Serikali kwa kutoa ruzuku kufidia mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Songea baada ya kufutwa kwa kodi za adha kwa wananchi ilibaki na chanzo kikuu cha mapato yake ya undani ambacho kila mwaka kiliingizwa katika bajeti ya Halmashauri (Chanzo hicho ni ushuru wa zao la mahindi) kutoka kwa wafanyabiashara. Kupitia chanzo hicho Halmashauri iliweza kukidhi kutimiza shughuli za kiuendeshaji kwa kiasi fulani kupitia mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia kitengo cha hifadhi ya chakula mkoani Ruvuma wamekuwa ndio wanunuzi wa zao hilo huko huko vijijini na kupelekea ushuru huo kutokulipwa tena.

Mheshimiwa Spika, matokeo, kwa kuwa halmashauri kwa kipindi cha miakamitatu 2003 - 2005 imeshindwa kupata mapato hayo kwa takribani kiasi cha shilingi 47,457,785/= kwa mwaka. Kwa kuwa pengo hilo linaendelea, tunaomba Wizara itupe fidia ya shilingi 80,000,000/= kwa mwaka 2006/2007 ili kufidia pengo hilo. (Angalia kiambatisho cha barua yangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema kuwa *National Audit Office* ni idara inayojitegemea. Hata hivyo kwa utaratibu uliopo, bajeti ya idara hii huwasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha. Nashauri kuwa utaratibu huu

uachwe na bajeti ya idara hii ijitegemee, hii ni kwa sababu *National Audit Office* ipo kwa mujibu wa Katiba ambayo ni sheria mama. Pia kujitegemea kwa idara hii kutaongeza *confidence* na hivyo kuogeza *efficiency* katika kudhibiti hesabu za Serikali. Pia kudhibiti na Mkaguzi Mkuu sasa hivi ana kaimu kwa muda mrefu mno. Nashauri athibitishwe kazini au kama ana mapungufu basi ateuliwe mwingine yote haya katika uongeza *confidence* yake akiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, kubadilisha leseni za udereva, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeingia mkataba na kampuni inayoitwa *Face Technologies (PTY) Ltd.* ya Afrika ya Kusini kwa kubadili leseni za udereva. Mkataba huu ni wa miaka mitatu na utagharimu shilingi bilioni 6.3. Kwa kuwa mkataba huu ni wa aina ya *BOT,* Serikali iwe makini sana maana inawezekana fedha zitakazopatikana zikawa nyingi ziadi ya hapo.

Kampuni ya *Face Technologies (PTY) Ltd.* imepata mikataba kama hiyo huko Uganda na Zambia. Katika nchi hizo utendaji wake umekuwa na walakini mpaka Mabunge ya nchi hizo yameingilia.

Nashauri Wizara iwe makini sana na utendaji wa kampuni hii na ikibidi iombe ushauri huko Uganda na Zambia. Nashauri hivi ili Wizara isije ikapata matatizo kama yaliyotolewa na *Net Group Solutions.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nimeombwa na wazee wastaafu wa Dodoma kuwasemea kuhusu matatizo katika pensheni yao na nakuambatanishia barua yao.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wanalalamika kuwa Serikali haifuati sheria katika kuwalipa pensheni yao. Ukishapata hoja ya wazee hawa nitaomba kurejeshewa *documents* hizi. Naomba Waziri ajitahidi kujibu suala hili.

Mheshimiwa Spika, ni mimi mtiifu wako, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu pamoja na viongozi woe kwa kazi nzuri. Pongezi za pekee kwa *Commissioner General* wa *TRA*, kwa kuvuka lengo la makusanyo. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Posta, inaendelea kuboresha huduma zake ila ipo haja ya kuongezewa mtaji ili iweze kuwafikia wananchi wengi vijijini kwa kufungua matawi yake. Benki hii iendelee kushirikiana kwa dhati na kwa karibu na shirika la posta ili huduma zao ziwafikiwe vijijini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa *(NIC),* hivi liko hai, mbona hivi sasa liko kimya na halijitangazi? Wateja wengi hawana uhakika wa kukata bima *NIC*. Je, *PSRC* tunarekebisha nini *NIC really?*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na udhibiti wa ununuzi wa umma. Sheria inayosimamia manunuzi inahitaji kupitiwa upya ina taratibu za manunuzi zimekuwa ndefu na kuchukua muda. Mafunzo yatolewe kwa wafanyakazi mbalimbali wa maeneo hili katika Mawizara *(Supplies Officers).*

Mheshimiwa Spika, mrundikano wa magari yasiyolipiwa Bandari ya Dar es Salaam. Ipo haja kwa *TRA* kuwa na eneo lake nje ya bandari ya Dar es Salaam ili ihifadhi magari na mizigo inayoshindwa kulipiwa na kubaki bandarini kwa miaka kadhaa hata kuozea hapo. Uchunguzi ufanywa kwa vile magari yanayonadiwa kufanyiwa *valuation* na kuwekwa bei kubwa sana kiasi ambacho watu hushindwa kununua na kubaki bandarini na kuongeza *congestion*. *TRA* ishirikiane na *TPA* kutafuta namna bora ta kurahisisha mizigo ya nchi jirani zikiwemo gari ziweze kuwa *cleared* mapema na ziwefikie wenyewe mapema bila kujaribu jina la *TPA*.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa mwanzo mzuri, asikate tamaa. Juhudi zake tunazielewa. Si kila mtu atamfurahia ila wananchi wakiridhika na huduma zake ni *blessing* kwa Serikali.

**MHE. EMMENUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara ya Fedha kwa kuandaa hotuba na kuiwasilisha Bungeni leo.

Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Naibu Gavana Ndugu Reli kwa kuwezesha Mabenki hasa *NMB* wakubali kwenda kufungua tawi Bukombe. Nasema hivyo kwa sababu tayari wameshafika Bukombe kutafuta sehemu ya kufungua Benki, nasema Mungu abariki utumishi wenu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kuchangia hotuba hii mambo yafuatayo hasa ikilinganishwa na Wilaya ya Bukombe.

Kuhusu *flow of OC from Treasurery to OC departments at Bukombe 2005/2006.*Wizara ya Fedha ndiyo wanaoidhinisha bajeti hii lakini mtiririko wako unavyoletwa Majimboni kwetu inashangaza.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti mwaka 2005/2006 Bukombe tuliidhinishiwa shilingi 1,647,457,200/= kati ya hizi hadi Juni tumepokea shilingi 1,207,673,400/= tukabaki tunadai Hazina shilingi 439,583,800/= zinazotokana na Idara ya Kilimo upungufu wa shilingi 14,885,900/=, Elimu upungufu wa shilingi 291,170,700/=, Afya upungufu wa shilingi 126,119,500/=, Barabara upungufu wa shilingi 3,426,700/= na Maji upungufu wa shilingi 3,981,000/= inayoleta jumla ya shilingi 439,583,800/=.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze hatma ya hela hizi ni nini? Je, tutazipata au ndiyo imetoka?

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Utumishi na Uongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe mwezi Julai niliona hela nyingi sana zimebaki Hazina ambazo ni sehemu ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atusaidie, naamini tatizo hili lipo sehemu mbalimbali, mbona hatuletewi hela zetu zote kama bajeti ilivyoainisha na kuidhinishwa?

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu madai ya Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe toka Hazina mwaka 2004. Wilaya ya Bukombe inawadai Hazina jumla ya shilingi 37,467,474.65/= za mishahara ya walimu na watumishi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu imekuwa ikiandika barua Hazina na hatupati majibu wala maelekezo ya upungufu huu, tufanye nini ili tupate hela hii ya watumishi? Je, kwa utaratibu huu tunawatia moyo watumishi au tunawavunja moyo?

Mheshimiwa Spika, madai haya yapo katika barua zifuatazo ambazo tayari zimeshatumwa kwa Katibu Mkuu Hazina yenye kumbukumbu Namba F.20/11/vol. 11/115 ya tarehe 21/06/2004 na yenye kumbukumbu Namba F.20/11/vol. 11/118 ya tarehe 02/07/2004 zenye madai ya jumla ya shilingi 37,467,474.65.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze ni lini Serikali ilitoa majibu ya madai hayo na hatma yake ni nini? Tunaletewa hela hizi au tunasamehe kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi zinazotolewa na Wizara, kwa mwaka 2003/2004 aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha kipindi hicho Dr. Festus Limbu, alipotembelea Wilaya ya Bukombe kwa ajili ya Harambee ya ujenzi wa jengo la CCM Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Bukombe alifurahishwa na akaahidi kuwapatia Bukombe shilingi 30,000,000/= ambazo hadi leo hazijatoletwa.

Mheshimiwa Spika, tuseme Serikali ina uwezo wa kutoa ahadi za uongo au hela itazipata lini? Kwa kuwa Serikali ni hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya michango hiyo natamka kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangia suala la wastaafu, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa kauli yake aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 02/08/06 akiagiza Waheshimiwa Wabunge tukaorodheshe majina ya wote wanaodai mirathi halafu tuyalete Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba wastaafu wetu na wale wanaotafuta mirathi wanahangaika mno.

Mheshimiwa Spika, tatizo la watumishi kupata ulemavu kazini sijui hatma yao ni nini.

Mheshimiwa Spika, mfano katika Jimbo la Bukombe yupo mfanyakazi Ndugu John Nuhu aliyeajiriwa Idara ya Afya tangu tarehe 15 Februari, 1971 na tarehe 25 Februari, 2003 alipofuka macho yaani haoni kabisa akiwa kazini na tarehe 07/01/2006 ilibidi astaafu kutokana na ulemavu na tarehe 08/02/2006 alipata mafao yake ambayo ni shilingi 1,426,000/=. Je, hali hii ndiyo ataishi nayo huyu mtu katika maisha yake?

Mheshimiwa Spika, mtu huyu amepata ulemavu ndani ya Serikali napenda kutoa ushauri Serikali iangalie namna ya kumpatia/kuwapatia posh ili waweze kuishi angalau kwa muda uliobaki wa uhai wao.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mtu kama huyu hana uwezo wa kufanya kazi yoyote.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mchango mdogo kwa Waziri wa Fedha kuhusu uchakavu wa sarafu za shilingi 100 na shilingi 50.

Mheshimiwa Spika, huko vijijini wafanyabiashara wengi hivi sasa wanazikataa sarafu ambazo sura au nembo zake zimechakaa kwa kuanza kufutika. Suala hili ni adha kubwa kwa wananchi vijijini, linaathiri biashara ndogo ndogo ambazo zimeshamiri vijijini. Namwomba Waziri wa Fedha atoe tamko la Serikali kuwathibitishia kuwa sarafu zilizochakaa bado ni fedha halali na zikubaliwe na wafanyabiashara bila wasiwasi.

Zaidi ya hao namwomba Mheshimiwa Waziri azihimize Benki za Biashara zilizoko Wilayani na wananchi kwa ujumla wakazibadili sarafu chakavu kwa sarafu mpya ambazo Benki Kuu kupitia Gavana aliiarifu Kamati ya Fedha na Uchumi kwua zipo nyingi katika akiba yao.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hoja zilizojitokeza ni nyingi, mimi nitafafanua chache na kama ulivyosema Naibu Waziri mwenzangu na mtoa hoja watakamilisha zitakazo baki. *(Makofi)*

Hoja ya kwanza iliyojitokeza inahusu kuondoa *VAT* kwenye mafuta ya taa na kupunguza kodi ya ushuru kwa bidhaa. Pamoja na kuondoa *VAT* kwenye mafuta ya taa Serikali pia ilipunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye mafuta hayo kutoka shilingi 122/= kwa lita hadi shilingi 51/= kwa lita ili kuhamisisha wananchi kutumia mafuta ya taa badala ya mkaa kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kulinda mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bei ya mafuta ya taa kwa wateja haikuteremka kwa kiwango ambacho Serikali ilitarajia. Aidha, imeelezwa pia kuwa kumekuwa na uhaba wa mafuta hayo. Sababu zinazoweza kuwa zimechangia kuwepo kwa uhaba huo wa mafuta ya taa na hivyo kutopungua kwa bei kwa viwango vilivyotegemewa ni pamoja na kuongeza kwa matumizi hayo kwa ajili ya kuchanganya kwenye *diesel* yaani *fuel alteration. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Bureau of Standards* inatembelea vituo vya mafuta kuona ni vituo gani vinaendesha biashara hii ambayo inaleta athari kwa vyombo vinavyotumia hayo mafuta na pale itakapo baina kuwepo kwa udanganyifu huu vituo hivyo vitachukuliwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilihusu Wabunge walilalamika kwamba bajeti haina maelezo ya kina. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Waheshimiwa Wabunge hupewa maelezo ya kina kuhusu bajeti na hushirikishwa katika utayarishaji wa bajeti kama ifuatavyo:-

(a) Tukianza na hatua ya awali, Waheshimiwa Wabunge pia wameshiriki na kuchangia kikamilifu katika utayarishji wa dira ya nchi, yaani *vision* ya nchi 2025. Wabunge pia wameshirikishwa katika uandaaji wa MKUKUTA.

(b) Wameshirikishwa katika vikao vya mwaka vya *Performance Evaluation Review* yaani *Annual Concentrative Meetings* ambavyo vinahudhuriwa na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kujadili mapitio ya bajeti yaliyotekelezwa na malengo ya bajeti ijayo.

(c) Kwa kupitia Kamati za Kisekta zinazochambua bajeti, vitabu vya maelezo ya kina yaani *MTEF documents* huwasilishwa kwenye Kamati na kukuonyesha:-

(i) Majukumu ya Wizara ambayo yanatekelezwa na Idara za Wizara.

(ii) Kuonyesha malengo yanayotekelezwa na Idara za Wizara.

(iii) Kuonyesha shughuli zinazotekelezwa kwa kila Idara.

(iv) Kuonyesha kiasi kilichotengwa kutekeleza shughuli hizo.

(d) Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani katika Halmashauri zao. Hivyo wanategemewa kuchambua na kuidhinisha bajeti za Halmashauri zao.

(e) Pamoja na maelezo hayo hapo juu, Wizara yangu imeamua kuandaa Semina kwa Wabunge wote juu ya mchakato wa kutayarisha na kutekeleza na kusimamia bajeti ya Serikali hapo baadaye. Ili kufafanu mambo yaliyojitokeza katika kupitia bajeti ya Wizara mbalimbali. Semina hii tunategemea kwamba itaandaliwa kabla ya Kikao cha Bajeti cha mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo niliyoyaeleza hapo juu ni dhahiri kuwa Waheshimiwa Wabunge hupata maelezo ya kina ya bajeti tangu hatua za awali na kinacholetwa Bungeni ni muhtasari tu wa maelezo ya kina ambayo nimeyaeleza hapo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu Serikali iwe na daftari la mali zake zote na Bunge lifahamishwe thamani ya mali za Serikali. Baada ya kupata mafanikio katika mfumo wa malipo *IFMs* , Wizara ya Fedha ilianza mchakato wa kuandaa mali za Serikali pamoja na kutathmini mali hizo. Lengo la Wizara ni hatimaye kujumuisha mizania ya Serikali yaani *Government Sheet* katika hesabu zake za kila mwaka. Hatua ya kwanza katika mchakato huo ilikuwa ni kuweka utaratibu wa kuorodhesha mali za Serikali katika daftari kadri zanavyonunuliwa. Hatua hii ilifuatwa na kutathmini mali katika Wizara nane kwa kutimia watalaam kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo ambacho kilishinda zabuni kwa ajili ya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili inayojumuisha Wizara nyingine nane inatagemea kukamilika mwezi Desemba, 2006. Aidha, Wizara nyingine saba zinatarajiwa kuwa zimefanya kazi hii kufikia Juni, 2007 na hivyo kufanya jumla ya Wizara 23 kuwa zimekamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu je, Serikali inafahamu faida na hasara za utekelezaji wa mashirika yake kwa mfano *TANESCO*, *TTCL*, Bima, Benki Kuu na kadhalika. Mashirika yote ya umma yalianzishwa kwa malengo maalum. Kwa hiyo, faida kubwa ya uwekezaji wa Serikali katika shirika lolote la umma ni kufikiwa kwa malengo ya kuanzishwa kwake. Pamoja na Msajili wa Hazina na Wizara ya sekta husika mashirika yote husimamiwa na Bodi za Wakurugenzi, Bodi hizo zinasimamia bajeti na utendaji wa mashirika hayo ikiwa ni pamoja na kuidhinisha matumizi. Mali zote zinazomilikiwa na shirika huingizwa katika kambi katika hesabu ambazo lazima zikaguliwe kwa mujibu wa sheria inayosimamia taaluma ya uhasibu. Aidha, taarifa za kila mwaka za mashirika yote huwasilishwa hapa Bungeni kwa taarifa na ushauri. Kwa namna hii Serikali hulifamisha Bunge na jamii kwa ujumla kuhusu utendaji wa mali za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata ilikuwa ni wananchi wapatiwe mikopo kupitia mabenki na taasisi nyingine za kifedha kwa masharti nafuu kutokana na fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni vyombo vinavyoanzishwa kwa malengo maalum ya kutunza akiba za wanachama wake ili wawe na kipato baada ya kuishiwa nguvu ya kufanya kazi.

Kwa hiyo, fedha zote zilizoko katika mifuko hii ni mali ya wanachama husika ambao wanahaki ya kuona kwamba fedha hizo zinaelekezwa na kupata faida kubwa iwezekanavyo. Uwekezaji mbovu unao athari ya moja kwa moja kwenye mafao ya wanachama husika wakati utakapowadia. Kwa sababu hiyo si sahihi kutaka fedha hizo zitumike kutoa mikopo kwa riba nafuu. Hata hivyo Serikali inafahamu kuwa mifuko ya Hifadhi ya Jamii ina fedha nyingi zinazoweza kuwekezwa kwa muda mrefu yaani *long term investiment*. Fedha hizi hutunzwa katika mabenki na kwa hiyo zinatumika kwa kiasi

fulani kutoa mikopo kwa wananchi. Hivi sasa Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu inashauriana na mifuko hiyo pamoja na mabenki ili kuwa na utaratibu utakaowezesha fedha hizi kutumiwa na mabenki kutoa mikopo ya muda mrefu pasipo kuathiri mapato ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu malipo ya watumishi wa Serikali walioko mbali na matawi ya benki. Hatua zinachukuliwa ili kuona uwezekano wa kuanzisha *Mobile Banks*. Tathimini inafanyika ili kujua idadi ya watumishi watakao hitaji huduma hiyo. Wizara, Halmashauri za Wilaya na benki zitashirikiana kujua idadi hiyo ili gharama za kutoa huduma za benki iweze kujulikana na taratibu ya kuanzisha huduma kwa *phases* ziweze kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia *National Microfinance Bank,* itafungua matawi mapya takribani 50, matano Dar es Salaam peke yake na sehemu mbalimbali hapa nchini pamoja na kuanzisha huduma ya malipo ya kadi ili kutoa huduma sehemu nyingine zaidi kwenye ofisi za mabenki.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyofuata ilihusu usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Wizara ya Fedha inatambua mchango mkubwa unaotolewa na sekta hii. Ili kuboresha zaidi hatua mojawapo itakayochukuliwa katika mwaka huu wa fedha ni pamoja na kutunga sheria ya udhibiti wa shughuli za Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii na pensheni na kuunda chombo kimoja cha kusimamia mifuko hiyo yaani *Pension Regulatory Authority.* Hatua hii itasaidia kukipa chombo hicho mamlaka ya kusimamia sera za uwekezaji katika mifuko hiyo na pia kushauri Serikali ni jinsi gani mifuko hiyo inaweza kutumia fedha za amana walizonazo kwa manufaa ya wanachama wake na wananchi kwa ujumla kama vile kutoa mikopo midogo midogo ya masharti nafuu, ujenzi wa nyumba za kupangisha na kuuza, na shughuli za biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilihusu Shirika la Bima la Taifa yaani *NIC* kama vile haliko hai, mbona halijitangazi na kwamba wateja wana wasiwasi na je, *PSRC* inarekebisha nini katika shirika hili? Shirika la Bima liko hai, linaendelea kuuza Bima, mwaka 2004 Shirika lilikuwa na asilimia 26 ya soko la Bima hapa nchini. Shirika linauza Bima kwa kutumia mawakala, madalali na wafanyakazi wake. *PSRC* inashughulikia taratibu zitazoliwezesha Serikali kubinafsisha biashara za *NIC* yaani biashara za bima ya maisha na bima za kawaida. Mchakato huu bado haujakamilika. Utakapokamilika Bunge lako Tukufu litaarifiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu Mamlaka ya Mapato na kwamba kuna usumbufu katika utoaji wa mizigo bandarini. Kumekuwa na malalamiko kuhusu usumbufu katika utoaji wa mizigo hasa katika bandari ya Dar es Salaam. Kwa kutambua tatizo hilo Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na *World Customs Organization* ilifanya utafiti uliojulikana kama *time release study* ili kubaini maeneo yanayosababisha ucheleweshaji, utafiti huo ulipendekeza pamoja na mambo mengine kutoa elimu kwa Wakala wa Forodha na kupeleka kadhia forodha kabla ya mizigo kufika.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato ilikutana na wadau wote na kuweka mikakati ya kuhakikisha ucheleweshaji huo unapungua au unatoweka kabisa. Taarifa ya

utekelezaji ilitolewa mnamo mwezi Machi, 2006 inaonyesha kwamba ucheleweshaji umepungua kwa kiwango kikubwa. Waagizaji wa mizigo wanashauriwa kufuata kikamilifu taratibu za forodha ikiwa ni pamoja na kuwahi kupeleka kadhia na kuwasilisha ankara zilizo sahihi ili kuongeza kasi ya utoaji wa mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu tatizo la mafuta ya ndege ya kwamba yanatumiwa kama mafuta ya taa. Ni kweli kwamba mafuta ya ndege hayana tofauti kubwa na mafuta ya taa. Hadi sasa kuna makampuni manne yanayoagiza mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani na yanayopelekwa nchi jirani yaani *transit*. Mamlaka ya Mapato itawasijili wote wanaoagiza *Jet A-1* ikiwa ni pamoja na kubainisha kiasi ambacho kila muagizaji ataingiza nchini. Kiasi hicho kitatokana na mikataba kati ya watumiaji wa hapa nchini na watumiaji na waagizaji wa nchi jirani. Kiasi hicho pia ndicho pekee kitakachosamehewa kodi. Kiasi chochote kitakachozidi kitalipiwa kodi kwa viwango vile vile vinavyotozwa kwenye mafuta ya taa. *(Makofi)*

Kuhusu uwekaji wa rangi na kutambulisha mafuta yaani *fuel marking,* utaratibu huu inasemekana kuwa haufai kwa mafuta ya ndege na kwa hiyo, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* na *EWURA* yataangalia utaratibu ambao utawezesha kudhibiti hayo badala ya kuweka alama.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa ambalo lilizungumzwa hata kabla ya kuwasilisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri inahusu kero ambazo wastaafu wanapata. Waheshimiwa Wabunge waliochangia bajeti ya Wizara Fedha wameonyesha kukerwa na matatizo mbalimbali yanayowapata wastaafu. Matatizo ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na yafuatayo, la kwanza ,ucheleweshaji wa kulipa mafao ya pensheni au mirathi kwa wastaafu au warithi, kima cha chini cha pensheni hakikidhi mahitaji ya wastaafu hivyo kuomba kuongezwa na mapunjo na kuomba malipo ya pensheni yalipwe kwa miezi miwili, miwili au mitatu badala ya utaratibu wa sasa wa miezi sita, sita.

Mheshimiwa Spika, pia malipo ya mafao kwa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashiriki iliyovunjika ambayo hawajalipwa mafao yao kuomba walipwe, ucheleweshaji wa malipo ya mafao ya wastaafu mara nyingi husababishwa na waajiri wenyewe kushindwa kutekeleza wajibu wao wa kuwasilisha majalada ya wastaafu Hazina miezi mitatu kabla ya mtumishi hajastaafu yakiwa na kumbukumbu zote zinazohitajika. Ili kupunguza au kuondoa ucheleweshaji wa malipo ya mafao ya wastaafu, waajiri wanaombwa kuwasilisha Hazina majalada ya watumishi wanaostaafu miezi mitatu kabla ya watumishi kustaafu yakiwa na kumbukumbu zote na ziwe sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa malipo ya mirathi, ucheleweshaji wa malipo huchangiwa kwa kiasi kikubwa na warithi wenyewe. Mara nyingi huchukua muda mrefu kukaa vikao vya kuteua msimamizi au wasimamizi wa mirathi kutokana na kutokuwa na makubaliano kati ya wanandugu. Aidha, tatizo la nyaraka pungufu pia huchangia ucheleweshaji wa kufanya malipo.

Kuhusu kima cha chini cha pensheni kuongezwa, Serikali inalishughulikia suala hili. Kikwazo kikubwa cha kuongeza kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu kama ilivyo kwa kima cha chini cha mishahara watumishi wa Serikali ni kutokana na ufunyi wa vyanzo vya mapato ya Serikali. Nia ya Serikali ni kuwalipa wastaafu kiwango cha pensheni kinachoridhisha lakini nia hiyo huathiriwa na uwezo mdogo wa Serikali kimapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wastaafu ambao kwa bahati mbaya huwa wamepunjwa mafao yao wakati wa ukokotoaji na hivyo kulipwa pungufu ya stahili zao hulipwa haki zao mara tu inapobainika kuwa wamepunjwa. Ni haki ya mstaafu kulipwa mapunjo yake yote ili mradi mapunjo hayo yawe ni halali na ya kweli. Kwa hivi sasa wastaafu wanaostahili kulipwa pensheni zao za kila mwezi hulipwa pensheni zao miezi sita, sita. Hata hivyo baadhi ya wastaafu wenyewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiomba malipo ya pensheni yalipwe kwa kipindi cha miezi miwili miwili au miezi mitatu badala ya utaratibu wa sasa Wizara ya Fedha imepokea mapendekezo hayo na itayafanyia kazi..

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika. Wizara yangu ilipokea jumla ya majalada 44,807 kutoka kwenye Taasisi zote zilizohusika. Kati ya idadi hiyo ya majalada, ni majalada 35,036 ndiyo yaliyokuwa na nyaraka kamilifu zilizowezesha ukokotoaji wa mafao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wastaafu wote 35,036 fedha zao zilipelekwa benki tayari kwa malipo lakini wastaafu 26,841 ndiyo waliofika benki na kulipwa mafao yao. Wastaafu 8,195 hadi sasa bado hawajajitokeza kuchukua mafao yao na juhudi za kuwapata wastaafu hao zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waheshimiwa Wabunge kama mnawafahamu muwaeleze ili waweze kwenda kwenye benki zinazohusika wakapate mafao yao. Aidha, malipo kwa wastaafu ambao hawajalipwa yanaendelea kupokelewa na kufanyiwa kazi kadri inavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya umma. Wizara inatambua tatizo hilo na imeandaa mkakati wa kuitatua kama ifuatavyo:-

Moja, kujenga uwezo wa mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma. Kusimamia utekelezaji wa sheria. Taratibu za kuajiri wafanyakazi wa mamlaka zimekamilika wafanyakazi 30 kati ya 51 wanategemea kuanza kazi mwezi ujao.

Pili, kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam wa ununuzi Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Vile vile mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kujenga uwezo wa wataalam wa ununuzi nchini umeandaliwa na utaanza kutekelezwa.

Tatu, utaratibu wa kusimamia shughuli za ununuzi wa umma umeandaliwa na utaanza kutumika mwaka huu wa fedha. Chini ya utaratibu huu kila taasisi itatakiwa kutuma taarifa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kuanzia mpango wa

ununuzi wa mwaka wa taasisi. Taarifa zote kuhusu mwenendo wa zabuni hadi kuingia mkataba na utekelezaji wa mikataba yenyewe. Taarifa hizi zitakuwa zimekaguliwa mara kwa mara kuhakikisha usahihi wake. Utaratibu huu utaiwezesha mamlaka kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa sheria katika taasisi moja moja kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pia, kuanzisha kada ya maafisa wa ununuzi ili kuchukua nafasi ya kada ya maafisa ugavi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo naomba nimwachie mwenzangu na mtoa hoja mwenyewe wakamilishe hoja nyingine ambazo zimejitokeza. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi niseme naunga mkono hoja asilimia mia moja. Afadhali niendelee na hoja ile ya ununuzi kuhusu kuanzisha utaratibu wa zabuni kwa njia ya mtandao yaani *Electronic Procurements*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Umma kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya Serikali inaangalia jinsi ya kutumia utaratibu huo wa *Electronic Procurements* kwa ajili ya bidhaa zinazotumiwa na taasisi za Serikali yaani *common use items*. Lengo ni kuondoa utaratibu wa sasa ambapo Bohari Kuu ya Serikali inanunua bidhaa hizo na kuzihifadhi kwenye maghala yao kwa ajili kuuza kwa idara mbalimbali za Serikali. Hata hivyo wakati utaratibu huu unaangalia kuna mambo muhimu yanatakiwa kuangaliwa kwa kina zaidi.

Kwanza kukubalika kwa *electronic signature* katika kufanya biashara hapa nchini ili ushiriki wa kampuni za kizalendo katika zabuni za Serikali ambazo ujuzi wao na matumizi yao ya mtandao ni mdogo.

Pili, kusambaa kwa mtandao kwenye ofisi za umma na uwezo wa watendaji kutumia mtandao. Kwa sasa Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma inaandaa mfumo wa upashanaji habari za ununuzi nchini yaani *Management Information System* ambao utatumika kupeana taarifa mbalimbali za ununuzi kati ya taasisi za umma na mamlaka. Tayari mamlaka inaitumia tovuti yake kuweka taarifa muhimu za zabuni ikiwa ni pamoja na matangazo ya zabuni za taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nitazidi kufafanua kidogo kwa hoja ambayo mikakati ya kupunguza matatizo ya pensheni ya wastaafu. Wizara yangu inakiri kwamba kuna matatizo ambayo yanaendelea kuathiri malipo ya wastaafu. Kutokana na kukubali kero zilizopo Wizara inaendelea kuchukua hatua matatizo hayo katika muda wa kati na muda mrefu. Katika muda wa kati Wizara imeendelea kuelemisha umma na wastaafu ili wajue taratibu za kufuata na nyaraka zinazohitajika ili kuhakikisha malipo ya mafao yao. Pia kupunguza usumbufu ambao wanapata wastaafu na warithi. Aidha, kuhimiza uhusiano mzuri kati ya waajiri na mahakama kwani malipo ya mirathi hulipwa katika mahakama walipofunguliwa mirathi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa malipo ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki malipo haya yanaendelea kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri aliyenitangulia kwa kushughulikia hoja ya mtu mmoja mmoja ambaye madai yake yanakubalika. Katika mpango wa muda mrefu Serikali imeanza kuangalia viwango vya pensheni ambavyo viko chini.

Aidha, Serikali imeendelea kushughulikia viwango vya pensheni kulingana na mapato ya Serikali. Vile vile Serikali inaamua kuongeza kima cha mshahara hatua ambayo itaongeza kiasi cha malipo ya wastaafu. Pamoja na hayo tunatarajia kuhamishia shughuli nyingine katika mifuko ya pensheni kama vile *PPF*, *GEPF*, *PSPF* na *NSSF* kwa lengo ya kuifanya Hazina ishughulikie zaidi masuala ya udhibiti yaani *regulatory and supervision*. Kuweka kumbukumbu za wastaafu kwenye kompyuta, kuwa na mtandao pensheni na kuweka huduma ya Ofisa Pensheni kwenye Hazina ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya kupanga muda wa kutosha kwa Kamati za Bunge za Kisekta kujadili Bajeti za Wizara. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya kuwasilisha Bajeti ya Wazira ya Fedha alirudia kauli yake aliyoitia mwezi Juni kwamba Kamati za Bunge zipewe muda wa kutosha kushiriki katika uchambuzi wa Bajeti. Lakini nikumbushe kwamba Bunge kwa kupitia Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge limeshirikishwa katika mchakato wa maandalizi ya Bajeti ya Serikali. Wizara inaahidi kuangalia njia bora zaidi ya ushiriki wa Bunge katika mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa *public expenditure review* ambao ni muhimu sana katika uandaaji wa Bajeti ya Serikali kutokana na uwazi wake na ushirikishwaji wa wadau wote. Washiriki wa *public expenditure review* ni pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Serikali, wahisani, wasomi na makundi mbalimbali ya kijamii. Wizara ya Fedha itachukua hatua za kuimarisha ushiriki wa Bunge katika utaratibu huu kwa kushirikisha pamoja na Wenyeviti wao, Makatibu wa Kamati za Kudumu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nashauri Waheshimiwa Wabunge wajihusishe hasa na kushauri ili kulipa Bunge nguvu ya kuidhinisha na kusimamia bajeti ya Serikali badala ya kujihusisha katika kutayarisha bajeti.

Kulikuwa na hoja juu ya Idara ya Ukaguzi wa Hesabu iongezewe uwezo ili ukaguzi ufanyike kwa wakati kwani ripoti za ukaguzi inasaidia sana endapo zitatoka mapema.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa ripoti za ukaguzi zikitolewa mapema zinasaidia sana katika *oversight function*. Idara katika mwaka uliopita imewezeshwa vya kutosha ndiyo sababu *reports* za ukaguzi zimetolewa mapema ndani ya muda unaokubalika kisheria. Pia kutokana na uwezeshaji huo na juhudi za *management reports* za ukaguzi zimetafsiriwa kwa Kiswahili. Kulikuwa na hoja kwamba Idara iwe na watumishi wenye sifa kwa kazi wanazozifanya. Idara inazizingatia kikamilifu ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwa kuendesha mafunzo kwa watumishi wake pamoja kuajiri watumishi wapya

wenye sifa. Idara itajitahidi kuboresha maslahi ya watumishi wake ili wasiondoke baada ya kupata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya waajiri wa sekta binafsi hawaongezi mishahara ya wafanyakazi wao baada ya Serikali kuongeza mishahara ya watumishi wake na pia hawafuatilii ulipaji kodi wa wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Spika, waajiri wote nchini wanawajibika kutekeleza sheria ya kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wao. Kima hicho hutangazwa na Waziri anayesimamia kazi na ajira baada ya kushauriana na wadau hawa, vyama vya wafanyakazi na waajiri. Wakati huo huo Serikali kama muajiri hupanga mishahara kwa watumishi wake kwa kuzingatia tija na uwezo wa bajeti yake. Waajiri wa sekta binafsi hawahitajiki kufuata mishahara ya Serikali. Aidha, Wizara ya Fedha haitoi maelekezo ya viwango vya mishahara kwa sekta binafsi, kazi ya kuhakikisha kodi ya wafanyakazi inayokusanywa hufanywa na *TRA,* lakini tutashukuru kupata taarifa zote za waajiri wanaovunja sheria. *(Makofi)*

Kulikuwa na hoja juu ya mgogoro wa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa nini Serikali haitekelezi uamuzi wa mahakama kuhusu kesi namba 95 ya mwaka 2003 hususan malipo kwa vigezo vya *real value* kifungu cha 11, asilimia 7.0 *compound interest* kifungu cha 12.

Mheshimiwa Spika ni kweli kwamba kesi ya madai namba 95 ya mwaka 2003 iliyofunguliwa na wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa niaba ya wenzao wapatao 17,946. Kesi hiyo ilimalizika kwa makubaliano nje ya mahakama baada ya ya kusainiwa *deed of settlement* baina ya walalamikaji na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Serikali na baadaye kuandikishwa Mahakama Kuu kwa mujibu wa taratibu za sheria. Aidha, chini ya kifungu namba moja cha makubaliano hayo walalamikaji waliokuwa wa Jumuiya Afrika Mashariki walikubali kusamehe vigezo vya malipo vilivyoainishwa chini ya kifungu cha 11 na 12 cha hukumu hususan malipo kwa kutumia vigezo vya *real value* na *7.0 percent compound interest.* Kwa kuwa makubaliano hayo yaliandikishwa Mahakama Kuu kwa mujibu wa sheria ni dhahiri kwamba Serikali inazingatia maamuzi ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya mtiririko wa fedha za matumizi ya kawaida kwenda kwa Halmashauri. Mtiririko wa fedha za Matumizi ya Kawaida, *OC* toka Hazina kwenda Halmashauri hutolewa kulinga na makusanyo ya mwezi hadi mwezi. Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ilikuwa na kiasi cha shilingi 1,954,507,200/= kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zilizotelewa kwa kipindi hicho zilikuwa shilingi 1,574,729,700/= na hivyo kuwepo pengo la shilingi 383,777,500/=. Hali hii haikujitokeza kwenye Halmashauri ya Bukombe peke yake, bali kwa Wizara, Idara na Mikoa yote. Hii ilitokana na Wizara, Idara na Mikoa yote kuchangia mahitaji ya ziada na yaliyotokana na ukame hasa kununua chakula na kugharimia uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barua alizozitaja nitazifuatilia na kujua ni kwa nini hazikujibiwa na hatua zinazostahili kuchukuliwa. Hata hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge ahakikishe kwamba Mweka Hazina wa Bukombe anafika Hazina ili kutafuta na kubaini chanzo cha upungufu huo katika fedha za mishahara. Kama kuna mishahara yoyote ambayo haijalipwa tangu Aprili na Mei, 2004 katika Halmashauri ya Bukombe, Mkurugenzi alipaswa kufuatilia na kujua tatizo ni nini. Wizara yangu itashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kufuatilia suala hili na ikithibitika kwamba kuna upungufu uliotajwa, fedha hizo zitalipwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya ucheleweshaji wa fedha za maendeleo kwenda Halmashauri za Wilaya. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha za maendeleo kwa Halmashauri zote zilitumwa robo ya pili ya mwaka 2005/2006 yaani mwezi wa Novemba, 2005 ikiwemo Halmashauri ya Kondoa. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Halmashauri ya Kondoa ilitengewa fedha za maendeleo jumla ya 74, 770,600/= kwa mgawanyo ufuatao, Maji Vijijini 41,270,600/=, Zahanati na Vituo vya Afya 28,500,000/= na *Participatory Rural Appraisal* 5,000,000/=. Jumla zote zinakuwa 74,770,600/=.

Mheshimiwa Spika, kulingana na mgawanyo wa fedha zilizotumwa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, 41,270,600/= zilikuwa ni kwa ajili ya maji vijijini na zilipokelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa mwezi Novemba, 2006. Hazina kwa upande wake ilitegemea fedha hizo zitatumika kwa kuzingatia vipaumbele katika Wilaya ya Kondoa na kugharimia maendeleo ya Mradi wa Maji wa Mto Moko. Kama mradi huo ni mmojawapo wa vipaumbele vya Wilaya hiyo, ni dhahiri kwamba Halmashauri ilipata fedha na siyo kwamba fedha hazikutolewa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa miradi inayotekelezwa na Wizara za Kisekta, Wizara ya Fedha hutoa fedha kulingana na miradi iliyowasilishwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Wizara zilizopewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni pamoja na Wizara ya Maji. Hivyo, Halmashauri kutopewa fedha kutoka Wizara husika inaashiria kwamba mradi huo haukuwepo katika mipango yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja juu ya malimbikizo ya madeni ya walimu, Mheshimiwa Mbunge amekiri kwamba yapo malimbikizo ofisini kwake. Tunamshauri awasilishe madai hayo TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na yale yatakayothibitika kwamba ni ya nani yatalipwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba watumishi wanaopata ulemavu wakati wakiwa kazini husaidiwaje. Kwa mfano, huko Bukombe mtumishi mmoja alipoteza uwezo wa kuona na baadaye alistaafishwa kwa ugonjwa. Kwa mujibu wa kanuni 110, 111 na 112 za Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Mtumishi wa Umma anapoumia au kufa kwa ajili ya ajali inayotokana na utendaji wa kazi ya umma anapata fidia ya ulemavu huo au ndugu zake hulipwa fidia kwa kifo kinachotokana na ajali ya kikazi. Ni wajibu wa mwajiri na mtumishi husika kuiarifu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu ajali na ulemavu wa mtumishi husika

akieleza mazingira yaliyosababisha ajali. Katibu Mkuu wa Utumishi ndiyo mwenye mamlaka ya kuunda Kamati za uchunguzi wa ajali na ikidhihirika kuwa si kutokana na uzembe wa mtumishi huyo, basi Katibu Mkuu Kiongozi hushauriwa kuidhinisha fidia ya kati ya 1,000,000/= hadi 10,000,000/= kutegemea na ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja aliyotoa Mheshimiwa Mbunge, kama nusu saa tu hivi nyuma, kwamba wastaafu wa Dodoma wamepuuzwa. Hilo nasema sidhani kama limepuuzwa. Siku walipokuja ofisini kwetu nimeonana nao, nimezungumza nao, nikawapa ahadi niende kwanza Dar es Salaam nikatafute tatizo ni nini na nitawajulisha nitakaporudi. Siku niliyoahidi nilirudi nikakaa nao tena, nikazungumza nikawaambia, matatizo yenu ni kwamba, kulikuwa kuna marekebisho kwa sababu kuna fedha zenu ambazo mtalipwa kuanzia Julai, 2004, mpaka hivi leo zinaongezwa ndiyo maana mmechelewa kupata hizo fedha mwisho wa mwezi wa Juni, lakini, tarehe 25 Julai fedha hizo zitakuwa zimeshapelekwa *NMB* na nyote mfike huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sijapata lalamiko tena kutoka kwa wastaafu hao na kwa hivyo nachukulia kwamba jambo hilo limemalizika. Basi sijui hao waliokuja ni wapi, lakini waliokuja nilikutana nao na tukaafikiana na hawajarudi tena kusema kwamba yale niliyowaahidi hayakutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya pili tena nasema naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa namwomba mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kuja kufanya majumuisho ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, unazo dakika 55.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Mheshimiwa Anna Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini na Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge ambao ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa kuongoza mjadala wa bajeti wa mwaka 2006/2007 kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Aidha, napenda nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuwasilisha kwa ufasaha maoni ya Kamati yake. Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo kuhusu masuala ya fedha Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Wawi, kwa maoni na ushauri wao juu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi kwa kweli wamechangia mjadala huu ama kwa kuzungumza ama kwa kuandika na hata sasa hivi tulikuwa tunaendelea kupata makaratasi yale ambayo walikuwa wanachangia kwa maandishi. Lakini wengine pia

tumezungumza hapo nje na wametoa maoni yao na napenda kuwaeleza kwamba kwa kweli michango yao imekuwa ni mizuri sana katika utekelezaji wa bajeti hii, lakini pia katika bajeti zijazo tutaweza kuzingatia na kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, napenda niwataje Waheshimiwa Wabunge, lakini sijui kama muda huu utachukuliwa kwenye muda wangu au vipi!

**SPIKA:** Huwa tunauondoa huo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Nashukuru sana.

**SPIKA:** Kengele inasimama wakati huo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwataje waliozungumza Bungeni ambao ni wafuatao, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani upande wa Fedha na Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, pia naye ni Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ambao walichangia kwa maandishi ni wafuatao, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Natumai wote nimewataja, lakini kama kuna wengine ambao sikuwataja basi mtaniletea vikaratasi na naomba radhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nijibu hoja mbalimbali zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge husika pamoja na kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Naibu Mawaziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kulikuwa na hoja ni nani wamiliki wa kampuni ya MEREMETA. Napenda kueleza yafuatayo kwamba, MEREMETA ni kampuni ya ubia kati ya Serikali na kampuni ya *Trinex Propriety* iliyoanzishwa mwaka 1997 chini ya Wizara ya Ulinzi kwa madhumuni ya kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo. Serikali kwa kupitia Msajili wa Hazina na *Trinex*

*Propriety* zinamiliki asilimia 50 ya hisa kila moja na Benki Kuu ya Tanzania kwa kweli haikuwa na hisa yoyote katika MEREMETA.

Mheshimiwa Spika, awali MEREMETA ilitarajia kununua dhahabu inayofikia kilo 300 kwa mwezi. Lengo hilo kwa kweli halikufikiwa kwani iliweza kununua kilo 40 tu kwa mwezi. Kushindwa huko kulitokana na uduni wa vifaa vilivyotumiwa na wachimbaji wadogo wadogo na pia ushindani wa biashara kati ya MEREMETA na wanunuzi wengine binafsi walioweza kulipa asilimia 20 zaidi ya bei waliyokuwa wanalipa MEREMETA kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 MEREMETA iliamua kuingia katika uchimbaji mkubwa na ilianzisha mgodi wa Buhemba. Baada ya hatua hiyo, kampuni ikakabiliwa na matatizo ya kifedha na pia matatizo ya kimenejimenti. Shughuli zote za ununuzi wa dhahabu zikasimama na Serikali ikabidi iingilie kati kumalizia mgodi huo wa Buhemba. Mgodi sasa hivi unafanya kazi, lakini kwa kiwango ambacho tunaweza kusema kwamba kisichoridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo hayo, Serikali sasa hivi imeunda timu ya kuchambua matatizo ya MEREMETA na kupendekeza namna ya ama kuinusuru au vinginevyo. Kwa hiyo, kwa sasa hivi hali ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa juu ya *Mwananchi Gold Refinery Pilot Project*. Napenda kusema yafuatayo, hii ni kampuni yenye wabia kadhaa ikiwemo Benki Kuu yenye lengo la kuanzisha karakana ya kusafisha dhahabu *(gold refinery)* hapa nchini. Chanzo cha mradi huu ni kuibuka kwa Tanzania kama mojawapo ya wazalishaji wakubwa wa dhahabu katika Afrika ambapo kulileta mawazo ya kwamba pengine Serikali ianzishe kiwanda cha kusafishia dhahabu *(gold refinery)*. Kati ya mwaka 2000 na 2003 yalifanyika mawasiliano Serikalini ya kuangalia uwezekano wa kuanzisha kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kuangalia uwezekano huo, fedha zilizotajwa ni pamoja na kuongeza thamani ya madini, kutoa ajira kiwandani na pia nje ya kiwanda kwa wachimbaji wadogo wadogo na kukuza ufundi wa kutengeneza vito *(jewellery)*. Iwapo kiwanda kinamilikiwa na Benki Kuu dhahabu ilionekana inaweza kusafishwa mpaka kuwa *gold bullion* ambayo inatumika kama fedha za kigeni katika malipo ya Kimataifa kama vile Dola za Kimarekani na *Pound Sterling* ya Uingereza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na manufaa hayo, Serikali iliagiza Benki Kuu iongoze katika kufanya utafiti wa kuanzisha kiwanda cha kusafisha dhahabu. Baada ya utafiti, Serikali iliamua Benki Kuu na *NBC* waanze utekelezaji wa mradi huu. Kiwanda kilikuwa kinafikiriwa kingekuwa kikubwa chenye uwezo wa kusafisha na kutoa dhahabu safi kati ya tani 40 hadi 60 kwa mwaka, ndiyo ilivyofikiriwa itakuwa hivyo. Gharama za kujenga kiwanda cha namna hiyo ilikadiriwa kuwa kati ya Dola za Kimarekani 15,000,000 mpaka 25,000,000 na kwa kuzingatia sababu nyingine muhimu tatu ambazo napenda kuzitaja.

Kwanza kabisa utaalam mkubwa ambao unahitajika kuendeshea mradi kama huo, uwezo wa baadhi ya wabia wa sasa kuchangia fedha za kutosha na hoja ya kupata uzoefu wa kutosha kuanzia uwezo wa namna ya kujipatia dhahabu hadi kufikia utaalam wa kuiuzia dhahabu safi katika masoko ya Kimataifa. Uamuzi kwa maana hiyo ulifikiwa na kuahirisha ujenzi wa kiwanda kikubwa, hivyo ikashauriwa kuwe na kiwanda cha majaribio yaani kama *Pilot Project.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi huo, mradi wa *Mwananchi Gold Company Limited* sasa hivi ni mradi wa majaribio yaani *Pilot Project.* Mtaji wake ni Dola za Kimarekani 600,000 na mitambo kutoka Italia iliyomo kiwandani ina thamani ya Dola za Kimarekani 850,000. Uwezo wa kiwanda hiki ni kusafisha dhahabu kiasi cha kilo tatu kwa siku, sawa na tani moja tu kwa mwaka mzima. Kiwanda kina wafanyakazi wanane, yaani Mkurugenzi Mtendaji, Mhasibu, Wakemia watatu, Msaidizi wa Ofisi yaani *Secretary,* dereva pamoja na mhudumu.Kampuni inayoendesha *Pilot Project* iliandikishwa kwa jina la *Mwananchi Gold Company Limited* mwaka 2004 na inamilikiwa na Benki Kuu kwa asilimia 20, *NBC* kwa asilimia 15, *Mwananchi Trust* kwa asilimia 45 na *MASE* mbia anayeleta teknolojia wa Italia asilimia 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu inajihusisha na mradi huu kwa sababu dhahabu ni *foreign exchange* na shughuli za kununua na kuuza *gold bullion* ni kazi muhimu ya Benki Kuu zote duniani. Vile vile *gold refineries* nyingi duniani zinamilikiwa na Benki Kuu. Kwa mfano, baadhi ya Benki Kuu zinazomiliki *gold refineries* ni pamoja na Benki Kuu ya Zimbabwe, Afrika Kusini, Austria, England, Switzerland, Russia, China, Philippines, Korea, India na Argentina.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya usimamizi na udhibiti wa fedha za Serikali. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwamba Wizara yangu imedhamiria kwa dhati kabisa kutekeleza ushauri wa Kamati yake wa kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Serikali zilizotengwa kwenye bajeti. Tayari hatua kadhaa zimeishachukuliwa ikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kuimarisha mtiririko wa taarifa za matumizi kati ya Hazina na Wizara, Idara, Mkoa pamoja na Halmashauri ili taarifa kutoka kwa watumiaji ziwe msingi wa kuidhinisha fedha.

(ii) Kitengo cha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha, yaani *Expenditure Tracking Unit* kimeimarishwa kwa kuongezewa idadi ya Maafisa. Aidha, kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2006/2007 kitengo hiki kitafanya kazi moja tu ya kufuatilia matumizi na kutoa taarifa zinazohitajika kwa mwaka mzima. Idara nyingine za Hazina kama *Technical Unit* na *Audit* zitaendelea na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Serikali lakini zikizingatia zaidi kwenye thamani ya matumizi yaani *value for money.*

Mheshimiwa Spika, samahani, katika Waheshimiwa Wabunge waliochangia pia Mheshimiwa Ameir Ali Ameir wa Jimbo la Fuoni alichangia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Benki Kuu, ni kwa nini kumekuwa na ongezeko kubwa la gharama za ujenzi wa Benki Kuu. Napenda kujibu kama ifuatavyo, kama nilivyoeleza tarehe 3 Aprili, 2006 wakati wa majumuisho ya Muswada wa Benki Kuu ya Tanzania, 2006 katika Bunge lako Tukufu, ujenzi wa Makao Makuu ya Benki Kuu unahusu majengo matano yaani *South Tower, North Tower, Conference Centre, East Block* ambalo ni jengo la *parking* na *North Block.* Zaidi ya majengo haya matano kuna mradi wa *basement* ambako zipo *strong rooms.* Gharama za ujenzi huo ni Shilingi bilioni 184.

Aidha, kumekuwa na ongezeko la gharama kutoka makadirio ya awali ya shilingi bilioni 112 mpaka shilingi bilioni 184 kutokana na matatizo ya udongo kuwa na hali ya mchanga mchanga na wingi wa maji mita chache tu chini ya ardhi na sehemu zote ambako zimejengwa *strong rooms.* Mambo haya yalikuwa hayakutegemewa kwamba yatakuwa hivyo. Pia, umuhimu mpya wa kuimarisha zaidi usalama kutokana na mabadiliko ya *exchange rate* kutoka Dola ambayo ilikuwa shilingi 950/= kwa dola moja mpaka *exchange rate* ya sasa ambayo ni zaidi ya shilingi 1,280/= kwa dola moja. Sababu hizi zote zimesababisha gharama za ujenzi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama za usalama na mawasiliano, itakumbukwa kwamba katika maelezo yangu ya kikao kilichopita nilieleza jinsi ambavyo sura ya mradi huu ilivyobadilika kwa kuzingatia zaidi usalama. Hali ya ujambazi na kupora mabenki imeongezeka sana na majambazi nao wanatumia teknolojia ya kisasa kufanya uhalifu. Usalama huu unajumuisha pia *strong rooms* ambazo zimeimarishwa zaidi katika majengo mapya ili siku za baadaye ziweze kuhifadhi fedha za Kitanzania, fedha za kigeni na hata dhahabu. Aidha, mtazamo wa usalama wa Benki Kuu katika dunia nzima umebadilika sana baada ya matukio ya Septemba 11, 2001 kuongezeka. Kutokana na hali hii, Benki Kuu imelazimika itekeleze *Integrated Security System* kwa majengo mapya ya Makao Makuu pamoja na matawi yote manne yaliyopo Zanzibar, Mwanza, Mbeya na Arusha.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu pia unawezesha mawasiliano kati ya Makao Makuu na matawi yake yote kufanyika kwa wakati mmoja. Mfumo huu utakuwa ni wa aina yake hapa nchini kwani kumbukumbu za matawi ya Benki Kuu yanaweza kuhifadhiwa Makao Makuu na pia yale ya Makao Makuu yakaweza pia kuhifadhiwa kwenye tawi lolote. Hivyo, gharama za usalama na pia mawasiliano kwa majengo mapya na matawi yote zitafikia dola za Marekani milioni 44.5.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi Serikali imeona ni jambo jema kujenga kitu kizuri ambacho kitadumu kwa kuangalia pia nchi nyingine wanavyofanya na pia kutokana na maelezo hayo, hakuna haja kama ilivyopendekezwa kwa kweli kuunda Kamati ya Bunge kufuatilia suala hili. Tunakubaliana na mapendekezo ambayo yalitolewa na Kamati ya Fedha kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika Benki Kuu pia kulikuwa na suala ambalo lilizungumzwa asubuhi hii kuhusu nani aliidhinisha mradi. Napenda kusema kwamba, mradi huu umeidhinishwa na Serikali na katika suala la kuleta Bungeni napenda kusema kwamba, hatuna kawaida ya kuleta Bungeni miradi ya Mashirika ya Umma isipokuwa

taarifa za mahesabu za mashirika zilizokaguliwa. Nimeona niongezee hili kwa sababu ya mchango ambao ulitokea asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine wa asubuhi hii kuhusu Benki Kuu labda ningeeleza pia kulikuwa na suala kwamba, je; tawi la Benki Kuu linaweza kujengwa hapa Dodoma? Ningependa kusema kwamba, kwa wakati huu kwa kweli matawi ya Benki Kuu mengi yanajengwa katika miji ya biashara. Kwa maana hiyo ni Dar es Salaam kwa Tanzania, lakini hata ukichukua India unakuta kwamba haikujengwa New Delhi, imejengwa Mumbai au Bombay. Lakini pia hata Brazil imejengwa Rio de Janeiro na sio Brasilia. Kwa hiyo, napenda kusema kwa wakati huu kwa kweli hakuna utaratibu wa kujenga tawi la Benki Kuu, lakini kazi ambayo inafanywa ya Benki Kuu inafanywa na *CRDB* kwa maana kwamba ina mkataba wa *state custody* na benki ya *CRDB.*

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya sarafu chakavu. Kama tulivyoeleza ni kwamba, baada ya kujadiliana na Mabenki ya Biashara tumekuwa na maelewano mazuri. Hivi karibuni hasa kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2005, sarafu mpya zimeanza kuongezeka katika mzunguko na hata hivyo sarafu chakavu katika miji midogo na vijiji bado kweli kabisa ni tatizo kubwa, nakubali. Lakini Benki Kuu ikishirikiana na Mabenki ya Biashara na Taasisi nyingine itaendelea kutafuta utaratibu mzuri zaidi wa kubadili sarafu chakavu kwa sarafu mpya. Kwa wananchi ambao wako Dar es Salaam au karibu na matawi ya benki kule Arusha, Mbeya, Mwanza na Zanzibar wanaweza kubadili sarafu chakavu kwa urahisi katika kaunta za matawi hayo. Kwa hiyo, suala hili bado tunalifuatilia kwa sababu bado ni tatizo hasa upande wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kwamba, je, *PPF* inaweza kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba za bei nafuu Mbinga kama ilivyowekeza kula Kiseke Mwanza? Napenda kusema kwamba, *PPF* ni kweli imeanza ujenzi wa nyumba za bei nafuu Mwanza na ingependa kuwekeza nchi nzima ili iweze kukidhi mahitaji ya wananchi na wanachama wake, lakini uwezo wake wa kifedha kwa kweli ni mdogo. Hata hivyo, tungependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge, nafikiri ni Mbunge wa Mbinga kama sikosei, awasiliane na *PPF* juu ya nia yake hiyo ya kuitaka *PPF* iwekeze kwenye ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwenye Wilaya yake na uwezekano wa kupata viwanja ili Mbinga nayo pia iwekwe kwenye orodha ya maeneo ya kufanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni la matumizi ya shilingi 1,000,000,000/= kila Mkoa kwa ajili ya Mfuko wa Uwezeshaji kwamba hayana idhini ya Bunge. Alipowasilisha bajeti ya ofisi yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitangaza mpango wa Serikali ambapo kila Mkoa Tanzania Bara ungepata shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi na kuongeza ajira. Aidha, hivi majuzi Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ametangaza kuwa kiasi hicho kimeongezewa maradufu na kufikia shilingi 21,000,000,000/=.

Hatua hiyo ya Serikali ni ya kutia faraja na ninamuomba Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed aungane na Watanzania wengine kutambua hatua hiyo kama uthibitisho na kutekeleza ahadi yake kuboresha maisha ya kila Mtanzania kama yeye

mwenyewe anavyosema. Wananchi wamepongeza mpango huu kwa matumaini makubwa na Serikali imedhamiria kutekeleza kwa uangalifu ili kupata manufaa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni juu ya *TISCAN* kwamba wanachelewesha mizigo ili kupata mapato na pia Maafisa wa Mamlaka ya Mapato huongeza thamani ya bidhaa iliyowekwa na *TISCAN*. *TISCAN* ni mawakala wa Mamlaka ya Mapato katika ukaguzi wa mizigo iingiayo nchini ambao huainisha thamani halisi ya bidhaa kwa ajili ya kukokotoa kodi stahili. Kampuni hii hulipwa kwa kutegemea thamani ya mzigo na kwa maana hiyo kucheleweshwa kwa mzigo hakuwezi kuongeza mapato ya kampuni kwani mapato yake hayategemei idadi ya siku mzigo ulivyokaa bandarini, inategemea mzigo ulivyopitishwa kwenye *TISCAN*.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kwamba mara nyingi ucheleweshaji wa mzigo hutokana aidha na waagizaji kutowasilisha nyaraka kamilifu au kuchelewa kuwasilisha nyaraka hizo. Wanangojea mpaka mzigo umefika ndiyo wanawasilisha. Lakini unaweza ku-*log in* kabla mzigo haujafika nchini Tanzania. Kamishna wa Forodha ndiye mwenye jukumu na mamlaka yote ya usimamiaji wa sheria ya forodha, *TISCAN* ni wapendekezaji wa bei kulingana na mtandao walionao kwenye nchi ambao mzigo huo unatoka. Kwa hiyo, inapotokea kuwa Kamishna ana taarifa za ziada kuhusu thamani ya bidhaa huwezi kubadilisha thamani iliyowekwa na *TISCAN* kulingana na jedwali la nne la Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki. Hali hii hutokea hata pale ambapo *TISCAN* wameweka thamani kubwa na Kamishna ana taarifa za ziada kuwa thamani hiyo ni kubwa na hivyo kuipunguza. Kwa hiyo, tumeliona kwa kweli tatizo hilo na ni kweli tatizo hilo lipo na tumeamua kwamba mamlaka ya mapato inatayarisha hifadhi ya takwimu *(database)* ili kuweza kuwa na thamani moja tu kuondoa tofauti ambazo zinajitokeza, kwa sababu kama mlivyosema, ukienda *TISCAN* unaambiwa labda *TRA*. Kwa hiyo, hilo kweli ni tatizo na tunalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, swali lingine lilikuwa ni Mamlaka ya Mapato itajenga lini jengo la ofisi ya Wilaya Mpwapwa? Ujenzi wa majengo ya Ofisi za Mamlaka ya Mapato ni mojawapo ya mambo yaliyopewa kipaumbele katika mpango mkuu wa miaka mitano *(cooperate plan)* na katika kutekeleza malengo iliyojiwekea, Mamlaka imeishajenga majengo ya Ofisi za Mikoa na vituo vya forodha zaidi vilivyopo mipakani. Aidha, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Mamlaka ina mpango madhubuti wa kujenga majengo ya Ofisi za Wilaya katika Wilaya ambazo hazina majengo hayo ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni juu ya mfumo wa utoaji leseni ya udereva kwa kutumia kompyuta *(computerized drivers licence) na* tumepata hii kwa maandishi.

Mheshimiaw Spika, ni kweli, *TRA* iliingia mkataba na kampuni hii ya *Face Technologies* na napenda kusema kwamba, ni kweli kuwa Mamlaka ya Mapato ilisaini mkataba na kampuni ya *Face Technologies* ya Afrika Kusini kwa ajili ya kuanzisha Mfumo Mpya wa Utoaji wa Leseni za Udereva kwa Kutumia Mtandao wa Kompyuta

*(Computerized Driving Licence System).* Katika mradi huu kuna makubaliano kwamba *Face Technologies* atajenga mfumo huo kwa gharama zake na atajirudishia fedha aliyowekeza katika kipindi cha miaka mitatu baada ya kukusanya ada ya leseni ya shilingi 24,000/= kwa kila leseni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kampuni hii ndiyo iliyojenga mradi wa usajili wa magari kwa kutumia Mfumo wa Mtandao wa Kompyuta *(Computerized Motor Vehicle Registration System).* Mradi huu ulitekelezwa kwa ufanisi mkubwa ukiacha mapungufu machache ambayo yalijitokeza. Kampuni ya *Face Technologies* iliishaelezwa matatizo haya na mtandao uliisharekebishwa ipasavyo.

Mheshimiaw Spika, kwa *experience* ambayo wamepata ya Kenya na Uganda, *TRA* imeweza kurekebisha masuala hayo. Aidha, mfumo mpya wa utoaji leseni za udereva kwa kutumia mtandao wa kompyuta nao pia utaunganishwa pamoja na ule wa uandikishaji wa magari ambao tayari unafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa thamani ya mradi itakuwa Dola za Kimarekani milioni 6.2, Serikali ilihakikisha kuwa mambo ya msingi yanayohusu mradi huu yamezingatiwa ipasavyo ndani ya mkataba. Aidha, mamlaka iliunda Kamati maalum ya kuweza kusimamia utekelezaji wa mradi ambayo inaundwa na Uongozi wa Juu ya Mamlaka ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Vile vile kuna Kamati za Ufundi na pia Kamati za Usimamizi wa Utekelezaji ambazo zinahakiki na kusimamia ubora wa vifaa vinavyoingizwa nchini na kampuni husika kwa ajili ya mradi kama ilivyokubalika katika Mkataba.

Aidha, Kamati hiyo itahakikisha kwamba kampuni hii itatoa kadi zenye ubora unaostahili. Pia, ili kusimamia mradi kikamilifu, mamlaka imehakikisha kuwa wadau wote wanashirikishwa ipasavyo katika kujenga na kumiliki mradi huu.

Mheshimiwa Spika, wadau hawa wanajumuisha Watumishi wa Mamlaka, Wizara ya Usalama wa Raia, Umoja wa Madereva, Wamiliki wa Vyombo vya Usafiri na kadhalika. Kampuni ya *Face Technologies* itawajibika chini ya mkataba kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Mamlaka ya Jeshi la Polisi ili kuwawezesha waweze kushiriki kikamilifu katika kuendesha mradi na pia kujenga uwezo wa kuendesha shughuli za mradi baada ya kampuni hiyo kumaliza mkataba wake.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine juu ya uimarishaji wa usimamizi wa fedha za umma. Napenda kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuhusu uimarishaji wa usimamizi wa fedha za umma. *(Makofi)*

Katika hotuba yangu ya bajeti ya hapo tarehe 15 Juni, 2006 nilieleza nia ya mkakati wa Wizara yangu kuhusu uimarishaji wa kitengo cha ukaguzi wa miradi. Kitengo hiki kitafuatilia matumizi hadi ngazi ya Halmashauri za Wilaya kama nilivyoeleza awali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waheshimiwa Wabunge, kupewa taarifa ya fedha mnazotumiwa kwenye Halmashauri napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila mwisho wa robo mwaka tunatoa matangazo kwenye magazeti na kwenye tovuti ya Wizara kuhusu fedha zote tulizotuma katika robo husika. Halmashauri zimeagizwa kubandika kwenye mbao za matangazo taarifa za fedha zilizopokelewa kila mwezi mara zinapotumwa toka hazina. Kama Halmashauri hazifanyi hivyo ni upungufu katika kutekeleza maagizo.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwakumbusha watendaji kufanya hivyo mara wanapopokea fedha kutoka Hazina. Kuhusu utaratibu wa kutoa adhabu kwa Halmashauri tunakiri kabisa kama mlivyoelewa Waheshimiwa Wabunge, kwamba kuwapa adhabu Halmashauri nzima pengine si sahihi kwani unawanyima wananchi haki yao. Hivyo basi Wizara yangu italishughulikia suala hili haraka iwezekanavyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuweza kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, suala la adhabu kwa Halmashauri zinazoshindwa kutoa hesabu safi kutokana na uzembe wa watendaji wake sasa ambao wanahamishwa badala ya kuadhibiwa na pia kuongeza uwezo kwa Halmashauri, kwa upande wa wahasibu napenda kusema kwamba kuhusu adhabu kwa wahasibu wazembe au wabadhilifu kanuni 35 (2) (b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 Wakurugenzi wa Halmashauri ndio wenye mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wao wakiwemo wahasibu wazembe. Hata hivyo katika ajira zilizofanyika mwezi Julai mwaka huu Wizara yangu imewapangia kazi wahasibu na wakaguzi wa ndani 596 katika Halmashauri mbalimbali. Hii ni hatua ya kuiwezesha Halmashauri kuwa na wahasibu au wakaguzi wa ndani wenye taaluma na hivyo kuongeza uwezo katika utendaji wao na pia utendaji wa Halmashauri hizi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine juu ya utekelezaji wa kazi za tume ya pamoja ya fedha *GFC*. Tume ya pamoja ya *GFC* ni ya sasa ya Muungano ambayo imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 77 na kama nilivyoeleza, Sheria ya Tume ya pamoja ya fedha sura 140 ndiyo ilianzisha Tume hiyo, ambayo ilianza kazi tarehe 3 Juni, 2003. Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ni kwamba *consultant* ambaye alikuwa anaangalia masuala haya yote ya Muungano amefanya uchambuzi wa kitaalam na kwamba ripoti hii imeshapelekwa kwenye Tume tunategemea kwamba itakapofika mwisho wa mwezi Agosti taarifa hii italetwa Serikalini na kuifanyia kazi. Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwamba kwa kweli tutalifuatilia suala hili vizuri na asiwe na wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya usahihi wa madeni ya nje na makampuni binafsi. Takwimu za madeni ya nje ambayo yanadhibitiwa kwa karibu sana na Benki Kuu ni yale ya Serikali, Mashirika ya Umma na madeni ambayo yamedhaminiwa na Serikali hayo yanadhibitiwa kwa kutumia *Commonwealth Secretariat*, *Dept Recording and Management System.* Baada ya kuondoa sheria ya kudhibiti fedha za kigeni (*Exchange Control)* mwaka 1992 ufuatiliaji wa mikopo ya nje

ya sekta binafsi ulizingatia takwimu za benki za biashara tu zilizoonyesha vyanzo vya mapato vya malipo. Ufuatiliaji huu wa madeni ya nje ya sekta binafsi ulionyesha kasoro nyingi kwani madeni yaliyotokana na uagizaji wa bidhaa na huduma mbalimbali moja kwa moja haukujumuishwa.

Kwa hiyo, kwa upande wa *Private Sector Externally Dept* kinachofanyika kwa sababu ni kwamba kila mwekezaji binafsi anaingia deni anapaswa kuandikisha deni hilo Benki Kuu kwa ajili ya kupata takwimu tu. Kutokana na upungufu huu benki ikishirikiana na *TIC* na *NBS* wanafanya *survey* kwa hivi sasa ya makampuni yaliyo na madeni nje ya nchi. Matokeo ya *survey* hii yatatoa picha halisi kuhusu takwimu halisi ya deni la taifa la nje ikiwa ni pamoja na deni la sekta binafsi. Matokeo ya utafiti huu yatatoa majibu ya masuala mengi ambayo yaliulizwa hasa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na naomba kama atataka taarifa zaidi basi Benki Kuu itakuwa tayari kuwasiliana naye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tofauti ya takwimu zilizomo kwenye *Tanzania Investment Report on Foreign Private Investment* 2004 Benki Kuu inamuomba tena Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kuwasiliana nao ili apate maelezo ya kina.

Hoja nyingine ilikuwa kwa nini thamani ya shilingi inaendelea kuporomoka kwa kipindi cha muda mrefu sasa? Ni kweli kwamba kwa kipindi karibu miezi 9 kuanzia Agosti 2006 thamani ya shilingi yetu imekuwa ikipomoromoka kwa wastani wa asilimia 1.1 kwa mwezi. Hali hii imesababishwa hasa na mahitaji makubwa sana ya fedha za kigeni kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na chakula (matokeo ya ukame) wakati huo huo mauzo yetu ya nje yamepungua sana katika mwaka huu wa fedha ulioishia mwezi Juni, 2006. Katika miaka minne iliyopita Tanzania ilitumia wastani wa dola za Kimarekani milioni 400 kwa mwaka kuagiza mafuta kutoka nje ikilinganishwa na matumizi ya dola bilioni 1.1 kwa mwaka 2005/2006.

Wakati huo huo mauzo yetu nje yaliongezeka kwa asilimia 7.2 kwa mwaka 2005/2006 ikilinganishwa na ongezeko la wastani 27 kwa miaka minne ya nyuma. Ongezeko hilo kubwa la mahitaji ya fedha za kigeni kuliko mauzo yetu nje yaliilazimu Benki Kuu kuuza dola nyingi katika soko kuliko katika miaka minne iliyopita. Hali hii iliyojitokeza mwaka huu ya *access demand* ya fedha za kigeni, tofauti na miaka ya nyuma ndiyo hasa iliyosababisha thamani ya shilingi kushuka katika kipindi cha karibu miezi kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine kubwa zinazoweza kusababisha kushuka kwa thamani ya shilingi yetu kama tulivyowahi kueleza mara nyingi huko nyuma ni nakisi kubwa katika urali wa biashara *(trade deficit)* na mfumko wa bei ulio juu kuliko nchi tunazofanya nazo biashara. Kama tulivyowahi kueleza mara nyingi njia pekee ya kuhakikisha uimara wa shilingi yetu ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje ya nchi ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni ili kukidhi uagizaji wa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza sera zinazolenga kuongeza mauzo nje ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika sekta hiyo, ili kuimarisha thamani ya fedha zetu. Aidha, Serikali inaendeleza juhudi za kupunguza mfumko wa bei ili ulingane na ule wa wenzetu tunaofanya nao biashara.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuliomba Bunge lako tukufu kuwahamasisha Watanzania, kupenda kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini ili kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni na kuagiza bidhaa za walaji *(consumer goods)*. Kwa mwaka ulioishia mwezi Juni mwaka huu Dola za Kimarekani milioni 800 zilitumika kuagiza *consumer goods* fedha hizi zingeweza kupungua mara dufu kama Watanzania wangeamua kutumia bidhaa zinazozalishwa humu nchini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni malipo kwa kampuni ya ukaguzi kwa shughuli za uzalishaji wa madini ya dhahabu *Alex Toured*. Tarehe 14 Juni, 2003 Benki Kuu ya Tanzania iliingia mkataba na kampuni ya *Alex Toured Aseaz Government Cooperation* ya Marekani kwa kukagua shughuli za makampuni ya dhahabu kwa lengo la kuhakiki mtaji, uzalishaji na uuzaji wa dhahabu nje ya nchi*, Investment Production* na *Export of Bonds*.

Madhumuni ya Serikali katika kufanya zoezi hili na kukagua na uzalishaji wa dhahabu ni kulinda maslahi ya nchi kwa kuhakikisha yafuatayo: Kwanza, kampuni za madini zinalipa kodi zinazostahili, pili, mchango wa dhahabu katika uchumi wa taifa unaonekana, tatu, *program* za ukaguzi ililenga katika maeneo matatu matano yafuatayo, ukaguzi wa kiasi na thamani ya dhahabu inayozalishwa na inayouzwa nje. Hatua hii itaiwezesha Serikali kujua kiasi cha mauzo ya dhahabu nje na pia kuhakikisha aina nyingine za madini yaliyochanganyika na dhahabu kaika udongo mmoja kwa mfano shaba na fedha. Pili, ukaguzi wa mitaji iliyowekezwa na Makampuni kama viko sahihi ili visije kuwa vinapunguza faida na kupunguza viwango vya kodi inavyotakiwa kulipwa na makampuni haya.

Tatu, ukaguzi wa gharama za mitaji wa shughuli za uzalishaji na kutathimini kama mapunguzo yaani *deductions* yanaendana na zile gharama zinazostahili kupunguzwa kwa sababu hawa wanapata *deductions* sisi kama hatujajua inakuwa ni vigumu wanaweza kusema zaidi na sisi kwa maana hiyo tukapata kodi pungufu. Hizi zisipoangaliwa kwa makini hupunguza kiwango cha kodi ambayo ingetozwa kwenye faida. Nne, ukaguzi wa bajeti na matumizi kwa ajili ya kufidia gharama za uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchimbaji pamoja na shughuli nyingine za madini, pia kuhakiki kama makampuni yanatimiza matakwa ya mikataba katika eneo hili la uhifadhi wa mazingira. Tano, kuhakiki usahihi wa mrahaba uliolipwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawalipa *SEGDC* ada ya asilimia 1.9 ya thamani ya dhahabu inayouzwa nje na ambayo imekaguliwa. Kumekuwa na hoja kwamba malipo haya yanaonekana kuwa makubwa hasa ukizingatia kwamba mrahaba ni asilimia 3 utafiti umebainishwa kwamba gharama ya asilimia 1.9 ya thamani ya dhahabu iliyokaguliwa na iliyouzwa nje ni *standard charge* ya duniani kwa hivi sasa. Mifano kadhaa ya nchi zenye *program* kama hii ni kama ifuatavyo: Ghana inalipa asilimia 2, Zimbabwe inalipa asilimia 1.9, Chile inalipa asilimia 2, Peru inalipa asilimia 1.8.

Mheshimiwa Spika, Mali iko kwenye mazungumzo na sasa hivi na kampuni na italipa asilimia 2 na Tanzania inalipa asilimia 1.9. Aidha, nchi zote hizi zinatoza mrahaba asilimia 3. Kulikuwa na suala hili la riba kubwa ya mabenki labda ningesema kwamba tumefanya mkutano na mabenki yote kulizungumzia suala hili la riba kubwa na katika *deposit* katika mikopo na riba ndogo katika upande wa *deposits*. Mabenki yameunda kamati yanalifanyia kazi suala hili na tumekubaliana kwamba itakapofika mwisho wa mwezi wa Oktoba, basi wataweza kutoa taarifa yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda tena kurudia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wote kwa mawazo yao na kwa kweli tunathamini sana mawazo yote na tutayafanyia kazi kwa hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kufikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 22 – Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 - *Administration and General* .. ... ... ... ... 282,235,337,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 – Mhasibu Mkuu Wa Serikali**

Kifungu 3001 - *Public Debt Management* . ... ... ... ... ... ... . 1,252,815,600/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na jambo dogo tu si kubwa *vote* 23 programu 3001 kifungu cha 250200 nilitaka kujua tu kiasi kilichotengwa fedha kwa wastaafu sasa hivi ni kiasi gani? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tafadhali urudie umesema kwa sauti ya chini sana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita Waziri alitueleza fedha ambazo alitenga kwa ajili ya hawa wastaafu *East African Community* na ziko katika fungu hili la *Accountant General* nilitaka anieleze safari hii zimetengwa kiasi gani maana sioni katika kifungu hiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona mngebadilishana na Mheshimiwa Mustafa Mkulo. Mheshimiwa Waziri ungechukua *microphone* ile ya kiti cha tatu pale.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama tulivyoeleza kwamba kwanza kabisa ziliwekwa shilingi bilioni 50 na ikabidi ziongezwe ikafikisha shilingi bilioni 117. Lakini kama tulivyoeleza kwamba wastaafu wameanza kulipwa na bado kuna wastaafu ambao hawakufika na kuna fedha ambazo karibu bilioni 8 ambazo bado wastaafu hawakufika na tulisema kwamba kwa kweli bado tunawatafuta ili waweze kulipwa na tutashughulikia mmoja mmoja mpaka wamalizike.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 - *Expenditure Management* ... ... ... ... ... ... ... 3,566,666,000/=
Kifungu 3003 - *Financial Management* ... ... ... ... ... ... ... 72,603,602,800/=
Kifungu 3004 – *Systems and Internal Audit*... ... ... ... ... ... 6,758,756,500/=
Kifungu 3005 - *Sub Treasury Arusha* … … ... ... ... ... ... ... ... 203,415,000/=
Kifungu 3006 – *Sub Treasury Coast* … … ... ... ... ... ... ... ... ... 189,846,000/=
Kifungu 3007 - *Sub Treasury Dodoma* … … ... ... ... ... ... ... ... 217,593,000/=
Kifungu 3008 – *Sub Treasury Iringa* … …... ... ... ... ... ... ... 202,361,000/=
Kifungu 3009 - *Sub Treasury Kagera* … .. .. ... ... ... ... ... ... ... 249,242,500/=
Kifungu 3010 – *Sub Treasury Kigoma* … …... ... ... ... ... ... ... 203,229,700/=
Kifungu 3011- *Sub Treasury Kilimanjaro*.... ... ... ... ... ... ... ...188,073,700/=
Kifungu 3012 - *Sub Treasury Lindi* .. ... ... ... ... ... ... ... ... ...204,520,000/=
Kifungu 3013- *Sub Treasury Mara* … .. ... ... ... ... ... ... ... ... ... 194,856,000/=
Kifungu 3014- *Sub Treasury Mbeya* . ... ... ... ... ... ... ... ... ... 209,590,000/=
Kifungu 3015 - *Sub Treasury Morogoro* ... ... ... ... ... ... ... ... 215,270,000/=
Kifungu 3016 - *Sub Treasury Mtwara*. ... ... ... ... ... ... ... ... ... 200,825,000/=
Kifungu 3017 - *Sub Treasury Mwanza* . ... ... ... ... ... ... ... ... ..191,220,000/=
Kifungu 3018 - *Sub Treasury Rukwa* … ... ... ... ... ... ... ... ... . 217,280,000/= Kifungu 3019 - *Sub Treasury Ruvuma* ... ... ... ... ... ... ... ... ..200,210,000/=
Kifungu 3020 - *Sub Treasury Shinyanga* ... ... ... ... ... ... ... 199,385,200/=
Kifungu 3021 - *Sub Treasury Singida* … … ... ... ... ... ... ... ... 209,200,000/=
Kifungu 3022 - *Sub Treasury Tabora* … ... ... ... ... ... ... ... ...208,220,000/=
Kifungu 3023 - *Sub Treasury Tanga* … ... ... ... ... ... ... ... ... 193,708,000/=
Kifungu 3024 - *Sub Treasury Manyara* … ... ... ... ... ... ... ... ... 313,701,000/=
Kifungu 7001 - *Pension and Gratuity* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 411,910,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and General*.. ... ... ... ... ... 9,027,732,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... 10,804,387,700/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* 50 *program* 10 *sub vote* 1001 *vote* ndogo 250100 mshahara wa Waziri, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa maelezo fasaha aliyoyatoa nina mambo kama manne ningeomba tuyaseme ili tutoe ufafanuzi na hasa yanayohusu Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema jana kwenye hotuba yangu kwamba kitendo cha kuongeza matumizi ya Serikali nje ya bajeti ambayo tumeipitisha ndani ya Bunge ni kitendo cha kuvunja Katiba. Kama Bunge lako kama ambavyo tunakula kiapo asubuhi cha kulinda katiba ni vizuri hilo tukaliweka wazi. Sasa mimi nafikiri Serikali haijatafuta *mechanism* ya kumuondoa Rais katika tendo la kuvunja katiba na kulifanya Bunge livunje Katiba. Serikali inaruhusiwa kuja Bungeni ikaleta *Supplementary Budget* kwa lile ambalo wanaona lina umuhimu wake. Kwa sababu tuna Kikao cha Bunge mwezi Oktoba Serikali ingeweza kufanya hilo. Kwa wakati huu Serikali ina uwezo wa kukopa fedha Benki Kuu au benki yoyote nyingine ili ikatekeleza malengo yake na huku iki-*protect* kuvunja kwa kuvunjwa kwa Katiba. Kwa hiyo, sisi hatupingani na *program* hata kidogo tunaiafiki *program* 100% na tungeomba programu hiyo itekelezwa vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, suala la Rais ama Bunge kuvunja Katiba ni zito sana hebu lifafanue kwanza nilione ili nione mtiririko wa mawazo kwa sababu ni jambo zito sana unalolisema.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ukurasa 114 wa Katiba kifungu 136 unasema kwamba fedha zinazotolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya matumizi zitakuwa kwa mujibu wa masharti yafuatayo:-

Fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa yanayotokana na fedha zilizomo katika mfuko mkuu wa hazina wa Serikali iwe imepitiwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria hii. Sasa Katiba hii kifungu cha 63 (c) kinataka Bunge hili kuidhinisha .....

**MWENYEKITI:** Utaje ibara umetaja tu ukurasa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ibara ya 63 (c).

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Sasa anasema na sisi tayari tulishapitisha kwenye bajeti hii fungu la Waziri Mkuu milioni 500 kwa kila Mkoa. Sasa imekuja kauli ya kuongeza *another* milioni 500 kwa kila Mkoa. Sasa nasema mimi sahihi, sasa imekuja kauli ya kuongeza another milioni 500 kila Mkoa. Sasa nasema mimi sahihi lakini kuongeza nje ya bajeti ambayo ilishakuwa *proved* na Bunge ni kosa.

Kwa hiyo, nasema naishauri Serikali ile *idea* nzuri tu iende kwa utaratibu ule ule wa Kibunge kwamba ongezeko lolote lazima liidhinishwe na Bunge hili. Sasa mimi ningependa Serikali ifanye utaratibu kwa sababu Oktoba tunakuja tena hapa na kwa sababu tunayo mabenki hivi sasa yanaweza kwenda kukopa Serikali ingefanya ili ikalihalilisha Bunge kufanya maamuzi sahihi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Hapana hujathibitisha hoja yako. Ongezeko la Bajeti, ingekuwa Mheshimiwa Rais ametaja milioni 500 halafu imefanya Bajeti hii yote siyo hapa kwenye fungu fulani liongezeke hiyo ndio tatizo. Lakini ndani ya Bajeti ile ambayo tumeipitisha kutoa hapa na kupeleka huku na hivi hivi huzingatia mahitaji maalum hiyo ndiyo nadhani Serikali wamefanya kwamba hizi milioni 500 siyo kwamba ni hela zilikuwa za siri hazieleweki zimekuja kuongeza bajeti tuliyopitisha. Ni kwamba ni dhahiri kuna miradi fulani au shughuli fulani ambazo zitapunguzwa ili kuwezesha jambo hili ambalo Serikali imeliona muhimu iweze kutekelezeka. Ushahidi wako ungekuwa ni kwamba kama bajeti ni trilioni 4, bilioni 200 sasa Rais kaongeza tena bilioni 500 kutoka mahali hatuzielewi. Lakini mimi nadhani ile jumla iko pale pale kwa hiyo, hakuna uvunjwaji wa katiba. Labda uthibitishe hilo sasa. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nathibitisha. Kila Wizara iliyoletwa katika Kamati ilikuwa imetaja vifungu na *amount* ambayo itapitishwa na halafu katika Bunge hili ikaletwa vifungu vya jumla jumla na katika vifungu vyote hivyo kila kifungu kimeelezwa matumizi yake ni kiasi gani. Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mfuko huu walitenga milioni 500.

Kwa hiyo, mapato ya Serikali yalitegemea kutumika kwa hizo milioni 500 sasa kama kuna mapato mengine ya ziada ambayo hayakupitishwa na Bunge hili then unaweza kusema hilo fungu limebadilika, vinginevyo kutakuwa na *reallocation* ya kukata mradi fulani ili kuziingiza mahali fulani hiyo ni *stage* nyingine kabisa.

Lakini kwa Bunge limepokea Mapato na Matumizi ya Serikali na ndiyo tuliyoyapitisha siku ile ya Bajeti. Sasa badiliko hili litaathiri mapato hayo na mipango hiyo iliyopangwa hapo mapema kwamba *reallocation* inayofanywa. Kwa hiyo, kuna miradi ambayo inaweza kukosa ambayo ilishapitisha katika Bunge hili. Sasa tungeelezwa mradi gani unakatwa ili fedha hizo ziende kwenye mradi huu ulikusudiwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo nasema lazima kuwe na *clause* inayoonyesha kwamba kuna mapungu mapato fulani ambayo Bunge hili hayakupitisha hatuyajui kwa sababu Bajeti iliyokuja hapa ina *deficit* asilimia 39. Sasa unaponiambia kwamba kuna fedha za ziada wakati bajeti yenyewe tayari ilikuwa na *deficit* hayo ni mashaka makubwa sana. Tungepata ufafanuzi zaidi kwa hili kwanza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ila ukitazama *(Order Paper)* orodha ya shughuli utaona kuna hatua nyingine zinachukulia na Serikali pamoja na *reallocation* na matumizi ya ziada n.k. labda Waziri wa Fedha, yaani ikiwa jumla haikubadilisha ile trilioni 4. tuliyopitisha haiwezekani kusema kuna uvunjaji wa Katiba. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo yako ya ufafanuzi. Kwanza kabisa, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Serikali katika hii, haivunji Katiba hata kidogo na kwamba, katika utaratibu wa matumizi ya Serikali, upo utaratibu kama ulivyoeleza Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba, kuna masuala ya *contingence,* kuna *re-allocation,* kuna taasisi za fedha, kuna *supplimentary* kwa mfano, tulipopata matatizo ya njaa, hatukuweza kurudi hapa Bungeni, lakini ilibidi kwa kweli fedha zitumike. Jambo hili ni zuri kwa wananchi, wamelifurahia. Tusije tukawarudisha nyuma wananchi katika suala hili. Tunataka kuondoa umaskini, lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ndugu yangu, kwa kweli kabisa taratibu zote zimefuatwa. Nataka kukuhakikishia kwamba, taratibu zote zimefuatwa, hakuna uvunjaji wa Katiba yoyote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Pengine Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, naomba ukae tafadhali, ungesubiri *Appropriation Bill,* kwa sababu hiyo ndiyo hatima yake, tutaoneshsa nini kinapita.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** La pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo nasema nimshukuru Mheshimiwa Waziri ni suala la MAREMETA kwamba, ametoa taarifa sahihi. Hapo nyuma Mawaziri, walikuwa wamejibu katika Bunge hili kwamba, kampuni hii imefilisika, lakini leo tumepata jibu tofauti. Naomba tu Serikali na Mawaziri wale waliosema ile kauli ya mwanzo, waweze kufuta ile kauli ya kwanza kwamba, hii kampuni haikufilisika kutokana na kauli aliyoitoa Mheshimiwa Waziri, hivi sasa.

**MWENYEKITI:** Uzifafanue hizo kauli kwanza, ile unayosema ifutwe ikoje na hii ya sasa ikoje.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Kauli ya kwanza, iliyotolewa na Mawaziri hasa Mawaziri wa Nishati na Madini walisema kwamba, kampuni ile imefilisika na sasa hivi iko katika *stage* ya ufilisi. Kauli iliyotolewa sasa hivi na Waziri ni kwamba, Serikali baada ya kufanya *investment* kwenye huu mradi huu wa kwanza 1997, baadaye ikafanya tena 2000, ikaona kwamba, kuna hasara fulani imepatikana lakini sasa hivi wanajaribu kurekebisha mradi huu na kwamba, Serikali bado inaendelea kufanya mchakato wa huo mradi wenyewe. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba, mradi umefilisika na hata kiwango cha uzalishaji kimeelezwa na Mheshimiwa Waziri hivi sasa.

Kwa hiyo, nasema kuna kauli mbili, moja ya kweli na kuna moja si ya kweli. Sasa ni ipi iliyokuwa ya kweli ili ile moja ifutwe, ambayo si ya kweli. Hilo lilikuwa la pili na la tatu, kuhusu *VAT* ni suala la *value for money,* tunakubali kabisa majengo yamejengwa vizuri na kadhalika, bado tuna wasi wasi wa *value for money* katika *Central Bank Investment.* Sasa hili ninaweza kukubaliana tu na Mheshimiwa Waziri, kama atakubali shauri hili liende kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, baada ya kuunda Kamati nzima ya Bunge. Mimi hilo sitakuwa na tatizo nalo, kwa sababu mimi mwenyewe niko kwenye Kamati hiyo.

Kuhusu *Alex Tower,* nakubaliana kabisa na Waziri lakini bado vile vile ninasema kuna suala la *value for money,* atuahidi kwamba, katika Bunge atatuletea thamani ya matumizi, yaani tathmini iliyofanywa na hiyo Kampuni ili kujua hizo fedha zilizotumika kwa ajili hiyo kweli zina *value* inayostahiki. Kusema tu kwamba, nchi fulani wanalipa na kadhalika, haijasaidia kitu. Muhimu ni kwamba, je, hizo dola milioni 35 zilizotolewa kweli hiyo kazi iliyofanyika ina *value* sahihi na Watanzania wanakubaliana nayo na Bunge hili linakubali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba mimi kupata ufafanuzi wa haya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani kuna hili la MEREMETA, ambalo linahitaji ufafanuzi, hasa ikiwa wakati wa Nishati walisema imefilisika. La *BoT*, naona huja hata ya kuendelea. Waheshimiwa Kamati ya Fedha na Uchumi, ina haki ya kuendelea kutaka *facts.* Kwa hiyo, hakuna haja ya kutafuta *commitment* ya Serikali, hii ni kazi yenu tu ya kawaida, labda hamuitekelezi tu vizuri. Halafu na huduma za huyu mthamini *1.9 percent.*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa maelezo aliyoyatoa na kwamba, kwa kweli nafikiri hakuna siri ya kazi ambayo imefanyika na inaendelea kufanyika. Kwa hiyo, tutakuwa tayari kutoa taarifa yoyote juu ya shughuli ambayo inayofanyika na Kampuni hii.

Niseme kwamba, wameanza kufanya kazi nzuri katika sehemu nyingine kwamba, kuna mapato ambayo tulikuwa hatupati hasa hasa yale ya *corporate tax,* ambayo yanatokana na *capital allowance* ambayo kampuni inaweka.

Kwa hiyo, baada ya kuona kwamba, baadhi ya kampuni hizi kwa kweli zilikuwa pengine haziko wazi sana, imerudisha asilimia 15, ambayo walikuwa wanapata. Walikuwa wanapata *a hundred and fifteen percent allowance* Serikali sasa imerudisha ile asilimia 15 na kwamba, Serikali imeanza kupata mapato kutokana na kampuni hii ya *Alex Tower.* Kwa hiyo, ni suala ambalo liko wazi na tutakuwa tayari kulitolea taarifa kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MWENYEKITI:** Suala la MEREMETA, Waziri hujalitolea taarifa, inaelekea kuna tofauti au mlikubaliana sawa sawa.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza maswali mawili kwa nia ya kupata ufafanuzi. *Vote* 50, Programu ya 10, *Sub-Vote* 1001, Kasma ya 250100.

Naomba nipate ufafanuzi kwa mambo mawili. Jana nilipokuwa nachangia nilikuwa nazungumzia pesa ambazo zilitengwa na Serikali ama Bunge lako Tukufu, kwa ajili ya kuhudumia mtaro wa Ntomoko katika Wilaya ya Kondoa. Naona Mheshimiwa Waziri, hakunielewa, majibu aliyotoa ni tofauti kabisa na hoja yangu. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, pesa za maji vijijini zilitolewa shilingi milioni 40 sawa, lakini siyo hizo ninazohoji.

Ninazohoji ni pesa ambazo huwa zinatengwa kupitia Wizara ya Maji. Mwaka 2005 zilitengwa shilingi milioni 30, Waziri Mkuu anaelewa sana jambo hili. Mngem-*consult* angewaeleza, mpate jibu sahihi. Hizo pesa shilingi milioni 30 hazijatolewa na Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Maji mwaka 2005/2006, ndiyo ninazohoji na nilipozungumza na Katibu Mkuu, nafikiri alinielewa. Kwa hiyo, naomba jibu, kama hazikutolewa, tunaomba pesa hizo zitolewe. Shida iliyoko ya maji katika mtaro wa Ntomoko sasa hivi ni hatari. Hiyo pesa inatolewa si mradi ni za uendeshaji wa kawaida tu, kupitia kwa miradi mikubwa ile kila mwaka kupitia Wizara ya Maji, huwa tunapewa pesa hizo, zinatengwa na mwaka 2005 zilitengwa.

Sasa kuniambia kwamba, tumetuma shilingi milioni 41 si sahihi, kwa sababu sizo ninazohoji, ni za kawaida tu za mradi ule. Mimi naomba mtupe hizo pesa, ama mtoe maelezo kama mmekwishawapa Wizara ya Maji, wamekwisha nithibitishia Wizara ya Maji kwamba, hawajapewa hizo pesa. Kama mmewapa, mnithibitishie niende nikawafuatilie kule. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo nilichangia jana ni kuhusu pensheni ya Wastaafu. Bunge lako Tukufu, lilipitisha Sheria ya Fedha mwaka 2004, ninayo hapa hiyo Sheria, imetamka katika marekebisho ya baadhi ya sheria ambazo tumerekebisha ni hiyo ya Pensheni ya Wastaafu. Naomba ruhusa yako, nisome kidogo lile eneo la Pensheni. *Amendment of the public Service Retirement Benefits Act 1999.* Sasa kipengele ama sehemu ya 39 ya Muswada huo wa Fedha wa mwaka 2004 unasema hivi: *"The principal Act is ammended by repealing Section 82 and replacing for the following provision:* Moja, ana-*amend* hiyo 82, *any person who at or during his retirement period, opted out of lump sum payment, shall as from the first day of July, 2004, be deemed to have not opted out and his name shall be registered in the pay roll of pensioners."*

Kipengele cha pili, inasema hivi: "*A person whom the provisions of the sub-section one apply, shall be entitled to payment of pension in the following manner:* Moja, *75,000 shillings for a person who retired at a rank of a senior officer.* Mbili, *45,000 shillings for a person who retired at a rank of officer."*

**MWENYEKITI:** Kamilisha ukiendelea hivyo kengele ikiita utakuwa wala hujadai ufafanuzi. Una dakika moja na nusu sasa.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** *Okay, 21,600* hicho ndiyo wanachodai. Malipo haya ndiyo wanayodai *pensioners,* sasa kama Sheria hii hatujaibadilisha, tutekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri, fedha za mtaro wa Ntomoko hutolewa kila mwaka, mwaka huu hazipo na hiyo pensheni sijui akina nani hawalipwi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za maji, namwomba Mheshimiwa Paschal C. Degera, baadaye aje tuoanane tupate ufafanuzi maalum. Lakini kama nilivyosema kwamba, pesa za sekta huwa tunazipeleka kwenye Halmashauri za Maji, ikiwa za kilimo na nyinginezo. Sasa kama kuna hizi *special,* labda tukae pamoja tulizungumze, tutazame matatizo yako wapi?

Kuhusu la wastaafu, kama alivyotangaza Mheshimiwa Waziri Mkuu, wale wote wenye matatizo ya wastaafu na mirathi, watuletee kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wameshatuletea hapa. Kama anayo *specific case,* tafadhali tu-*deal* nayo *case* kwa *case on case basis*. Kama nilivyosema, nilikutana na Wastaafu mimi hapa Dodoma, tukajadili matatizo yao, tukapeana ahadi baada ya wiki tukutane, tumekutana nao lilikuwa kundi kubwa tu hawapungui kiasi 100 mpaka 120 hivi. Tukakubaliana na baada ya hapo sikupata malalamiko mengine tena. Wako mmoja mmoja waliokuwa na tatizo fulani fulani kuhusu hii pensheni zao. Hiyo sheria haijabadilika, lakini tafadhali hebu tuletee hiyo kesi hasa tuweze kuitatua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paschal C. Degera, ninavyomwelewa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Serikali, keti basi kwanza, ni kwamba, fedha za Ntomoko namna unavyozungumza wewe, inawezekana ni masuala ya utaratibu wa mafungu. Amekukaribisha mkakae pamoja ili tatizo hilo litatuliwe.

La pili, hawa *pensioners* kama wapo, bado ziada ya wale ambao ameshughulika nao Waziri binafsi, basi apatiwe orodha au waletwe kwake ili ufumbuzi upatikane. Nilikuwa nadhani kwa ufafanuzi huo, mambo yamekaa vizuri tu. Endelea.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa ufafanuzi huo wa kwako na wa Waziri. Hilo la Ntomoko, mimi nitashirikiana nao tuweze kulitatua. Hili la viwango vya pensheni, nilikuwa naomba tu aseme kwamba, viwango hivi ndiyo vinalipwa sasa ama ni tofauti? Hicho ndicho ninachotaka kujua. Hiyo ya kusema kwamba, alete watu ambao hawajafanyiwa utaratibu, nitalifanya. Lakini viwango tunavyolipa sasa ndiyo ninachotaka kujua. Ahsante Mwenyekiti.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Paschal C. Degera, anasema kwamba, kama sheria inasema hivi, kwa sababu kuna suala katika sheria hiyo hiyo ambayo inazungumzia juu ya wastaafu kulipwa, badala ya kulipwa kwa miezi sita, labda kulipwa mwezi mmoja na kadhalika na hilo nalo pia linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, sisi siku zote tunafuata sheria, kwa hiyo, kama sheria ni hivyo, tutaiangalia ili kuangalia ni jinsi gani utekelezaji wake utakuwa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niko kwenye *vote* ya 50, Programu Na. 10 na *Sub-Vote* 1001, kile kifungu kidogo cha 250100 – Mshahara wa Waziri.

Kwa kuwa tu ni utaratibu na siyo maana yetu ya kufanya hivyo, miongoni mwa vigezo ambavyo Halmashauri zetu zimekuwa zikitumia kwa kuwasiliana na Wizara katika suala zima la kuongeza ruzuku, kufidia ruzuku ya mapato kwenye Halmashauri

zetu ilikuwa ni muundo mzima wa Bajeti ndani ya Halmashauri na vyanzo vya mapato ndani ya Halmashauri yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwandikia Mheshimiwa Waziri, lakini pia nimechangia kwa maandishi, tatizo kubwa sana tunalopambana nalo kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Songea, bajeti yetu kila mwaka inajumuisha pia na chanzo kikubwa cha mapato kutoka katika zao la mahindi, ushuru wa zao la mahindi. Lakini sasa hivi zao hili la mahindi limekuwa likinunuliwa moja kwa moja na kitengo cha hifadhi ya chakula kwa takriban miaka mitatu mpaka sasa. Hivyo basi, *Council* imekuwa ikipoteza mapato ya takriban shilingi milioni 47 kila mwaka, kwa sababu Kitengo cha Hifadhi ya Chakula, kinaponunua kama Serikali, hatukitozi ushuru wowote ule.

Nimekuwa kwa kweli nikiomba sana, je, Wizara kwa kuwa hicho ni kigezo kimojawapo kinachozingatiwa kuongeza ruzuku ya uendeshaji kwenye Halmashauri; ni lini basi Wizara itafidia pengo hilo ambalo linatumika na Serikali kwa manufaa pia ya nchi nzima ya Tanzania, lakini linapoteza mapato kwenye *Council* yetu na sisi tuko tayari kulisha nchi lakini huku tunashindwa kuendesha Halmashauri yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu maelezo, je, wako tayari sasa Wizara kuisaidia Halmashauri fidia hiyo kuanza kuiongeza kwenye ruzuku ile ya Serikali Kuu ili Halmashauri iweze kuendelea kujiendesha, vinginevyo tunaendelea kuwa na madeni na matatizo makubwa sana ya uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**WAZIRI WA FEDHA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Jana nilikuwa nasema kwamba, mdogo wangu Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, lazima atasimama katika kifungu hiki na ni kweli kwamba, alifanikiwa na tukazungumza na niseme kwamba, kwa uhakika tunalifanyia kazi suala hili. Kwa hiyo, naomba kumridhisha kwamba, hili suala tunalifanyia kazi na hata jana usiku, nilipokuwa na wataalam wangu, tulilizungumza suala hilo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... Sh. 5,195,265,400/=
Kif. 1004 – *Legal Services* ... ... ..... Sh. 294,510,800/=
Kif. 1005 – *Information, Education and Communication* .... ..... .... ..... ...... ..... Sh. 998,820,400/=
Kif. 2001 – *Government Budget* ... ... .... Sh. 38,540,330,600/=
Kif. 2002 – *Policy and Research* ... .... ..... Sh. 80,758,736,300/=
Kif. 2003 – *Treasury Registrar* ... ..... ...... Sh. 6,670,969,700/=
Kif. 4001 – *External Finance* ... ..... ..... Sh. 4,614,898,700/=
Kif. 5001 – *Stock Verification* ... .... .... Sh. 4,927,329,600/=

Kif. 6001 – *Computer Services* ... .... ... Sh. 2,392,553,900/=
Kif. 6002 – *Tax Revenue Appeals Board* ... Sh. 884,908,200/=
Kif. 6003 – *Technical Audit Unit* ... ..... ....Sh. 458,120,800/=
Kif. 6004 – *Tax Revenue Appeals Tribunal* ... Sh. 610,137,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3003 – *Financial Management* ... ...... ....... Sh. 6,153,861,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu – 45 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kif. 1001 – *Administration and General* .... ...... Sh.2,541,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

Kif. 1001 – *Administration and General* .... ...... Sh. 3,027,244,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* .... ...... ...... Sh. 913,498,300/=
Kif. 2001 – *Government Budget* ...... ...... ...... Sh. 1,230,872,000/=
Kif. 2002 – *Policy and Research* ..... . ..... ...... Sh. 18,929,430,000/=
Kif. 2003 – *Treasury Registrar* ..... ..... ..... .... Sh. 6,183,604,700/=
Kif. 4001 – *External Finance* ..... ...... ...... ...... Sh. 2,122,583,000/=
Kif. 6001 – *Computer Services* ..... ..... ...... ..... Sh. 1,357,607,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2006/2007, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha

bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu, liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nakumbusha tena kwamba, Kamati Tendaji ya *CPA Tanzania Branch,* hiki ni kingine, wanataka kukutana na mimi sasa. Kwa hiyo, tutaonana mara baada ya kusitisha shughuli hizi.

Kuna Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakiandika kwangu kuulizia mwelekeo wa Bunge shughuli zake kwisha, Mkutano huu wa nne ni lini? Napenda kutangaza tu kwamba, ni kesho kabla ya saa saba. Tutaanza na maswali kama kawaida, halafu kwa sababu jioni hii tunapitia hii Miswada mbalimbali ya Sheria za Fedha, maana nadhani tutaweza kuimaliza. Lakini hata ikisalia, kwa maana kuna utata hapa na pale, hautaweza kuwa mgumu wa kutushinda kuweza kukamilisha kesho tutakapoanza tena baada ya maswali na maswali ni macheche kesho.

Kwa hiyo, pengine saa 3.30 tutamalizia shughuli zilizosalia, kama kuna Azimio la kupitishwa na kadhalika, hayo yote yatakamilika, nitatoa taarifa fupi ya shughuli zilizofanyika kabla ya kumwita mtoa hoja kuahirisha Mkutano mzima, ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, natazamia pengine saa tano au saa sita, tutakuwa tumekamilisha shughuli zetu. Hii ni taarifa ili mjiandae kwa wale wanaopanga kwenda majimboni na wale ambao tumewapangia safari za nje, waweze kujiandaa.

Baada ya matangazo hayo, sasa nalisitisha shughuli za Bunge kabla ya wakati hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.25 Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

## MISWAADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2006 *(The Appropriation Bill, 2006)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ABDISALAAM I. KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba, Miswada ya Sheria kwa kutumia shilingi 4,562,801,509,500/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, itakayotekelezwa na Serikali, kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, hotuba ya bajeti ya mwaka 2006/2007, iliainisha shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi 4,562,801,509,500/= kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida, shilingi 2,828,334,901,400/=; Matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi 1,734,466,608,100/=; Jumla ni shilingi 4,562,801,509,500/=.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, limekwisha jadili na kupitisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri, wakati walipowasilisha makadirio ya Wizara zao, hivyo basi, madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe matumizi ya Serikali ya mwaka 2006/2007, ya jumla ya shilingi 4,562,801,509,500/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo, iliyokubaliwa na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Kwa kawaida, Muswada huu huwa hauna wachangiaji, kwa sababu unakubali kile ambacho tayari tunacho, kwa hiyo, namwomba Katibu atupeleke katika hatua inayofuata.

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2006 *(The Appropriation Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ABDISALAAM I. KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2006 *(The Appropriation Bill, 2006)* na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo, naomba Muswada huu sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kutangaza kuwa, Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa mwaka 2006/2007, umeshapitishwa na Bunge.

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2006**
***(The Finance Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2006, yaani *Finance Bill, 2006,* pamoja na marekebisho yake, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya fedha na uchumi, chini ya Uenyekiti wa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tutazingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati, tutayafanyia kazi ipasavyo. Aidha, kwa mara nyingine, napenda kutoa tena shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote, ambao walichangia katika hotuba ya bajeti. Tumezingatia kwa dhati, michango yenu ambayo imesaidia sana kuboresha Muswada huu, vilevile nawashukuru pia wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara, sekta binafsi, wakulima na wananchi kwa ujumla, ambao kwa nyakati tofauti, wametoa ushauri wao, ambao kwa kiwango kikubwa tumeuzingatia.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Muswada wa Sheria ya Fedha, yaani *The Finance Bill, 2006* ni utekelezaji kisheria kwa hatua kadhaa, kwenye mfumo wa kodi na ada mbalimbali, kama nilivyowasilisha Bungeni katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2006/2007 na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho, sheria 12 zinazohusu fedha, kodi na ushuru, kwa lengo la kuweka, kurekebisha au kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali. Sheria hizo ni zifuatazo: Sheria ya Bodi ya Korosho Tanzania sura namba 203; Sheria ya ushuru wa bidhaa sura namba 147; Sheria ya michezo ya kubahatisha ya mwaka 2003; Sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004; Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa sura namba 290; Sheria ya madini sura namba 123; Sheria ya ushuru wa barabara na mafuta

sura namba 220; Sheria ya ushuru wa *stamp* sura namba 189; Sheria ya uwekezaji sura namba 38; Sheria ya mamlaka ya mapato Tanzania sura namba 399; Sheria ya Bodi ya Rufaa za kodi sura namba 408; na Sheria ya kodi ya ongezeko la thamani sura namba 148.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 13, sehemu ya kwanza inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada wenyewe. Sehemu ya pili inapendekeza kurekebisha Sheria ya Bodi ya Korosho Tanzania sura namba 203 katika kifungu cha kumi kwa kuongeza kifungu kipya cha 10(a), kwanza, kuongeza kiwango cha ushuru unaokusanywa hivi sasa kutoka asilimia 8.5 ya bei ya korosho ghafi, *F or B value* hadi asilimia 10.

Pili, kuhamishia madaraka ya kukusanya ushuru wa korosho ghafi, inayosafirishwa nje ya nchi kwa Mamlaka ya Mapato *TRA.* Kwa hivi sasa ushuru huu unakusanywa na Bodi ya Korosho Tanzania.

Aidha, mapendekezo haya yana lengo la kuharakisha ukusanyaji na uwajibikaji, ambapo ushuru huu utagawanywa kwa utaratibu ufuatao, asilimia 6.5 ya thamani ya korosho ghafi sawa na asilimia 65 ya ushuru utakaokusanywa, itapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya zinazozalisha korosho, kwa uwiano utakaotolewa na Bodi ya Korosho. Asilimia 3.5 ya thamani ya korosho ghafi, sawa na asilimia 35 ya ushuru utakaokusanywa, utapelekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina kama mapato ya Serikali.

Aidha, kama Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alivyobainisha, wakati akiwasilisha makadirio ya matumizi ya Wizara yake, kuanzia mwaka huu wa fedha 2006/2007, Serikali imetenga fedha, yaani ruzuku kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa bodi zote za mazao, ikiwemo Bodi ya Korosho Tanzania na gharama za utafiti wa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Tatu, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147, katika kifungu 124 na jedwali la nne, katika marekebisho hayo inapendekezwa yafuatayo:-

(a) Kurekebisha kifungu cha 124 cha sheria hiyo, kwa kuongeza kifungu kidogo cha 1(a), kinachoweka sharti kwa bidhaaa zinazouzwa nje ya nchi, kuandikwa maneno kwa kuuzwa nje ya nchi tu au *for export only,* ili kuzuia bidhaa hizo kuuzwa hapa nchini bila kulipiwa kodi.

(b) Katika kifungu kidogo cha pili, kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa, kwenye huduma za mawasiliano ya simu za mkononi, yaani *mobile phone air time,* kutoka asilimia tano hadi saba ili kuongeza mapato ya kodi kutoka kwenye chanzo hiki.

(c) Kuongeza kifungu kidogo cha 5(a), kinachoweka ushuru wa bidhaa wa kiwango cha asilimia 20 kwa magari madogo machakavu, yatakayoagizwa kutoka nje ya nchi, yenye umri wa miaka 10 au zaidi. Aidha, magari yatakayohusika ni yale yaliyoainishwa

katika *tariff codes 8702.10.198702.90.19* na *tariff code* zote zilizoko chini ya *tariff heading 48703.*

(d) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa, kwenye mafuta ya taa kutoka shilingi 122 kwa lita hadi shilingi 52 kwa lita. Hatua hii itasaidia kuhamasisha wananchi, kutumia mafuta ya taa badala ya mkaa au kuni na hivyo, kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba ya bajeti, hatua hii inaweza kuongeza tatizo la ukwepaji wa kodi, kwa kuchanganya mafuta ya taa na mafuta mengi ya petroli, yaani *fuel adulteration.* Kwa hiyo, Serikali itaimarisha udhibiti katika biashara ya mafuta kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EURA)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).*

(a) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa, kwenye bidhaa mbalimbali zisizo za petroli kama vile tumbaku, sigara, vinywaji baridi, bia, uvinyo na vinywaji vikali, kwa asilimia saba sawa na kiwango cha mfumko wa bei.

(b) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa, mafuta ya petroli, kama ifuatavyo, ili kulinda mapato ya Serikali hasa kufuatia kuondolewa *VAT* katika bidhaa za mafuta ya petroli. Petroli kutoka shilingi 146 kwa lita hadi shilingi 315 kwa lita, Dieseli kutoka shilingi 127 kwa lita hadi shilingi 292 kwa lita, mafuta mazito ya mitambo kutoka shilingi 13.50 kwa lita hadi shilingi 109 kwa lita, Dieseli ya kuendeshea mitambo ya viwandani kutoka shilingi 201 kwa lita hadi shilingi 366 kwa lita, kuondoa ushuru wa shilingi 114 kwa lita uliopo sasa kwenye gesi ya kupikia.

(a) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa mifuko ya *plastic* inayoruhusiwa, kutoka asilimia 15 hadi asilimia 120 ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

(b) Kufanya marekebisho yenye lengo la kuainisha *tariff codes* za magari madogo, kwenye sheria hii ili zilingane na *tariff codes* zilizoaiinishwa ndani ya utaratibu wa ushuru wa forodha katika Afrika Mashariki, yaani *common external tariffs,* chini ya itifaki ya umoja wa forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Aidha, marekebisho haya ni pamoja na kufuta *tariff codes 4702.10.20* na *tariff codes 8702.90.20*, zilizoainishwa chini ya *tariff heading 87.02* na badala yake kuweka *tariff codes 87.02.10.19* na *tariff code 8702.90.19.*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha ishirini kifungu kidogo cha tatu, kuweka muda maalum wa miaka mitano wa uhai wa leseni ya kuendesha bahati nasibu ya taifa. Kifungu hiki kama kilivyo, hivi sasa hakina ukomo wa leseni hii

(b) Kurekebisha kifungu cha 31(2) na jedwali la pili kwa kubadilisha utaratibu wa kutoza kodi ya michezo ya kubahatisha, ambapo badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza kodi kwa kigezo cha vifaa vya kuchezea michezo hii, kodi hiyo itozwe kwa kiwango cha

asilimia 13 ya mapato yote yatokanayo na michezo ya kubahatisha. Kifungu cha 31, vifungu vidogo vya nne, tano, saba na nane, kuipa bodi ya michezo ya kubahatisha kwa niaba ya mamlaka ya mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha tatu kama kilivyorekebishwa, kufuta tafsiri ya maneno makazi, yaani *residents* au mkazi *resident* na kuacha tafsiri ya maneno haya kama yalivyo kwenye sheria ya sasa. Aidha, marekebisho haya yalikusudiwa kuweka tafsiri mpya ya makampuni na watalaam wa kigeni, yanayotoa huduma za kitaalam katika sekta ya madini, kwa madhumuni ya kodi ya zuio.

(b) Kifungu cha saba kuongeza kifungu kidogo kipya cha nne na tano ili kubadilisha utaratibu wa kutoza kodi ya mapato ya hitimisho la ajira, isipokuwa pensheni, ambayo haitozwi kodi ili mapato atakayolipwa msataafu, yaweze kugawanywa katika kipindi cha miaka sita ya mwisho au kipindi halisi cha ajira, ndiyo yatumike kukokotoa kodi badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza kodi mapato hayo kwa mkupuo, kama vile ni mapato ya mwaka mmoja. Hatua hii ina lengo la kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi wanapostaafu.

(c) Kuongeza kifungu vidogo vya tatu na nne, chini ya kifungu cha 16, ili kutoa unafuu kwa kodi ya mapato, kwa waajiriwa wanaochangia mfuko kutokana na mapato yao ya ajira kama ilivyo sasa kwa wafanyabiashara. Wachangiaji watapaswa kujaza fomu za marejesho ili kudai nafuu hii ya kodi.

(d) Kufuta kifungu kidogo kipya cha tatu cha kifungu cha 83 kinachopendekeza marekebisho ya viwango vya kodi ya zuio, yaani *withholding tax*, kwa wataalam na makampuni ya kigeni yanayotoa huduma za kitaalam, yaani *technically services* katika sekta ya madini. Aidha, pamoja na kufutwa kwa kifungu hiki, mapendekezo haya yaliyotolewa na Kamati ya Fedha na Uchumi, kimsingi Serikali imeyapokea na itayafanyia kazi, kwa kuzingatia kwamba, marekebisho ya kiwango cha kodi ya zuio kwa makampuni ya kigeni na wataalam, ni miongoni mwa masuala yanayojadiliwa na Kamati iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais, kupitia mikataba ya madini. Hivyo, ni vyema Kamati hii iachiwe ikamilishe kazi yake na iishauri Serikali ipasavyo.

(e) Kifungu cha 86; kwanza, kuongeza kifungu kidogo cha pili, kutoa unafuu wa kodi ya mapato kwa mfumo wa uwekezaji katika vipande, yaani *unity trust*. Hivi sasa mfumo huu unatozwa kodi ya zuio ya asilimia kumi na baadaye mapato yake ya mwaka, yaani *total income*, hujumishwa na kutozwa kodi ya makampuni ya asilimia 30. Marekebisho haya, yanapendekeza kutoza kodi ya zuio ya asilimia ambayo itakuwa ndiyo kodi ya mwisho, yaani *final withholding tax* na kuondoa kodi ya makampuni *tax* ya asilimia 30, inayotozwa sasa. Lengo la hatua hii, ni kuhamasisha uwekezaji wa pamoja nchini. Pili, kufuta kifungu kidogo kipya cha (g), kufuatia kufutwa kwa kifungu cha 83(3), kutokana na sababu nilizoeleza hapo juu.

(f) Kifungu cha 94; kumpa mamlaka ya kisheria Kamishina wa Kodi ya Mapato, kukokotoa mapato ya ukomo wa ajira, yaani *terminally benefits,* yaliyogawanywa miaka mitano nyuma. Sheria kama ilivyo hivi sasa, inampa mamlaka kamishna kukokotoa mapato ya kodi yaliyogawanywa nyuma kwa muda wa miaka mitatu tu.

(g) Kifungu cha 96, kurekebisha ukomo wa kutoa makadirio ya mapato yanayopaswa kukatwa kodi, yaani *adjustment of assessment* ili kuwiana na pendekezo la kutoza kodi ya mapato ya hitimisho la ajira. Kugawanywa katika kipindi cha miaka sita ya mwisho au kipindi halisi cha ajira na hatimaye kumwezesha Kamishna wa Kodi ya Mapato, kutoa makadirio ya mapato ya ajira kwa muda wa miaka sita ya nyuma wakati wa kukokotoa mapato ya hitimisho la ajira.

(h) Kuongeza aya ndogo namba mbili katika jedwali la kwanza, chini ya aya namba 3(1), kwa kupunguza kodi ya mapato kwa makampuni mapya yatakayojisajili katika soko la mitaji la Dar es Salaam na kuuza angalau asilimia 35 ya hisa zao kwa wananchi ili kiwango cha kodi, kiwe asilimia 25 badala ya asilimia 30 kama ilivyo hivi sasa. Punguzo hili litakuwa la muda wa miaka mitatu, hatua hii ina lengo la kushawishi makampuni mengi ya binafsi, kusajiliwa katika soko la mtaji na kuongeza umiliki wa wananchi katika makampuni ya Tanzania.

(i) Jedwali la pili aya namba 1(f), kuongeza aya ndogo 1(f)(4), ili kutoa msamaha wa kodi ya mapato kwa Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, sehemu sita inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, kwenye jedwali la kwanza, aya ya 3(s), ili kufuta ada ya magari yanayotumia barabara za miji, yaani *city plying fees,* inayotozwa chini ya sheria hii. Hatua hii inakusudia kuondoa kero na kuboresha mazingira ya biashara.

Sehemu ya saba inahusu marekebisho ya Sheria ya Madini, ambayo kifungu cha 86(1)(b), kinarekebishwa ili kutoa msamaha wa mrabaha kwa wazalishaji wa chumvi, wanaotumia rasilimali zinazojirejesha, yaani *renewable resources* katika kusaidia kampeni ya kupambana na magonjwa yatokanayo na ukosefu wa madini joto mwilini. Sheria ilivyo sasa, wazalishaji chumvi, hutozwa mrabaha wa asilimia tatu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane, inapendekeza marekebisho katika jedwali la pili la Sheria ya Ushuru wa Barabara ili kuongeza ushuru wa barabara kutoka shilingi tisini kwa lita ya petroli na dieseli hadi shilingi 100 kwa lita. Hatua hii inakusudia kulinda mapato ya Mfuko wa Barabara, kwa kuzingatia ongezeko la gharama kwa matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa ni mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa *Stamp* ya kuhamishia kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, jukumu la kukusanya ushuru wa *stamp*, badala ya Katibu Mkuu wa Hazina, kama ilivyo kwenye sheria ya sasa.

Sehemu ya kumi inafanyia marekebisho sheria ya uwekezaji kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu 19(1), kuondoa msamaha wa kodi unaotolewa sasa kwa magari madogo ya binafsi, yaani *non utilities vehicles* kwa wawekezaji wote wenye vyeti vya uwekezaji vinavyotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC).* Aidha, wawekezaji wenye *certificate* zilizotolewa na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* kabla ya tarehe 1 Julai, 2006, hawatahusika na marekebisho haya. Hatua hii ina lengo la kuziba mwanya wa kukwepa kodi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

(b) Kufuta vifungu vidogo vya mbili na tatu vya kifungu cha 19 na kuweka kifungu kidogo kipya cha moja, ili kuweka sharti kwa Serikali, kutobadili mfumo wa kodi kwa wawekezaji mahili tu, yaani *strategic investors*. Kifungu hiki hivi sasa kinaweka sharti kwa Serikali kutobadili mfumo wa kodi kwa wawekezaji wa aina zote. Hatua hii ina lengo la kupunguza misamaha inayoikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 11 inahusu marekebisho katika jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato kwa kuongeza katika orodha, Sheria ya Bodi ya Korosho Tanzania Sura Na. 203 kuwa ni mojawapo ya sheria inayosimamiwa na mamlaka hii katika ukusanyaji wa ushuru wa mauzo ya korosho ghafi nje ya nchi.

Sehemu ya 12 inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Rufani za Kodi kwa kuongeza tafsiri ya neno *assessment* ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hii. Hivi sasa sheria haina tafsiri ya neno hilo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 13 na ya mwisho, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha 17(2), kupunguza ukomo wa muda wa kuomba marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kutoka miaka mitano hadi mitatu ili kuondoa mianya ya ukwepaji kodi.

(b) Kifungu cha 29 (3), huongeza kiwango cha adhabu kwa kosa la kutotoa Stakabadhi kutoka faini ya shilingi 200,000/= ya sasa hadi shilingi 500,000/=.

(c) Kifungu cha 45 Kuongeza kiwango cha adhabu kwa kosa la kushindwa kulipa kodi, kushindwa kuwasilisha fomu za marejesho ya kodi kwa wakati unaotakiwa kutoka faini ya shilingi 200,000/= hadi shilingi 500,000/= au kiasi cha mara mbili ya kodi husika, kutegemea kipi ni kikubwa.

(d) Kufunga kifungu cha 47(1) na kuweka kifungu kidogo kipya cha (1) ili kurekebisha kiwango cha adhabu kwa kosa la kukwepa kodi kwa njia ya udanganyifu. Chini ya marekebisho haya, mhusika atapaswa kwanza, kulipa kodi aliyokwepa kulipa. Pili, kulipa faini ya shilingi milioni mbili au mara mbili ya kodi iliyokwepwa, kutegemea kipi ni kikubwa au kifungo cha miaka miwili au faini na kifungo kwa pamoja. Hatua hii inakusudia kupunguza ukwepaji wa kodi. Jedwali la kwanza linalohusu *Zero Rated*

*Supplies,* aya namba 12 kuweka aya ndogo ya (d), ili kutenganisha dawa ya mbu ya kuchoma, yaani *Mosquito Coins* na vifaa vya usafi wa akina mama, yaani *Sanitary Pads* kwa kuwa bidhaa hizi hazina uhusiano katika matumizi.

(e) Jedwali la pili linalohusu *Exam Supplies and Imports*. Kwanza, kuongeza aya ndogo ya 1(7) inayotoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani, kwa Kahawa inayosindikwa nchini, kama ilivyo kwa Chai, ili kufufua uzalishaji wa mauzo ya Kahawa nje ya nchi.

Pili, kutenganisha dawa ya mbu ya kuchoma na vifaa vya usafi wa akina mama, yaani *Sanitary Pads,* kwa kuwa bidhaa hizi hazina uhusiano katika matumizi.

Tatu, kuorodhesha katika Msamaha wa Kodi ya Ongezeko, gesi ya kupikia ya *LPG* na Mitungi ya kuhifadhia gesi hii, ili kuhamasisha wananchi kutumia gesi badala ya kuni au mkaa kwa matumizi ya nyumbani na hatimaye kulinda mazingira.

Nne, kujumuisha katika msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani, Mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa, ili kupunguza mzigo wa ongezeko la bei ya mafuta hayo bila kuathiri mapato ya Serikali.

Tano, kurekebisha aya ya 16 kwa kufafanua kwamba, ada ya kukodi ndege, *Air Craft Leasing Fees* inayolipwa na Kampuni ya Ndege iliyosajiliwa hapa nchini, haitozwi kodi ya Ongezeko la Thamani, sawa na ilivyo kwa gharama ya kununua ndege. Lengo la msamaha huu ni kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni za Ndege za hapa nchini ili kuyaongezea ushindani.

(f) Jedwali la Tatu, kuongeza aya mpya ya 28 katika orodha hii, kujumuisha bidhaa zitakazo nunuliwa na Benki Kuu ya Tanzania na kutumika katika shughuli za Benki hii katika orodha ya msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba, mengi ya marekebisho ninayopendekeza, ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali, ambayo tayari yaliridhiwa na Bunge wakati wa kuhitimisha hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2006/2007.

Hivyo, naomba Bunge lako Tukufu, lipitishe Muswada huu ili kuhalalisha kisheria, Bajeti iliyokwisha pitishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ililtolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kwenye orodha yangu ninao wachangiaji watatu; Mheshimiwa Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa William H. Shellukindo na Mheshimiwa Juma A. Njwayo. Tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, kwa maoni ya Kamati, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI ):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, baada ya kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2006 *(The Finance Bill, 2006)*. Tunakusudia kupendekeza marekebisho katika Sheria mbalimbali, zinazohusu Fedha na kodi kwa madhumuni ya kutoza au kubadili viwango vya kodi na ushuru.

Kimsingi Kamati imekubaliana na mapendekezo ya marekebisho yote ya Muswada huo, ambayo ni utekelezaji wa kisheria wa mapendekezo ya Serikali, ambayo yaliridhiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 23 Juni, 2006, wakati ulipohitimisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge kifungu cha 70(2), kifungu kidogo pili, Toleo la mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Fedha wa mwaka 2006. Kama nilivyoeleza hapo juu, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati ilikubaliana kimsingi na maeneo yote ya marekebisho ya Sheria ya Muswada, yaliyowasilishwa Mbele ya Kamati na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Hata hivyo, Kamati katika Sheria ya Bodi ya Korosho, Sheria ya Uwekezaji na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, ilitoa maoni na mapendekezo ambayo Mheshimiwa Waziri, alikubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania, inafanya kazi ya kufanikisha jukumu lake la kusimamia ukusanyaji wa mapato. Katika miaka miwili ya fedha iliyopita; 2003/2004 na katika mwaka 2004/2005; Mamlaka ya Mapato, imeweza kukusanya zaidi ya malengo iliyowekea. Hayo ni mafanikio makubwa lakini bado changamoto kubwa ipo kwa *TRA*, kuongeza juhudi zaidi ya kukusanya mapato zaidi.

Mapato ya Serikali bado hayawiani na matumizi, hali inayosababisha kutegema misaada kutoka nje ya nchi ili kuziba pengo la bajeti. Pato la Taifa bado lipo chini na kazi zaidi inatakiwa kufanyika. Kamati inaunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais, alipotembelea *TRA* kuwa, waongeze juhudi za makusanyo ya mapato ili waweze kufikia wastani wa shilingi bilioni 200 kwa mwezi, ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Kwa kuwa, bajeti yetu hadi sasa ni tegemezi kwa asilimia 39, Kamati inaishauri Serikali, kuongeza juhudi ya kukusanya mapato yetu ya ndani. Hali hii itatusaidia kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha, unaotokana na mikopo na misaada kutoka kwa wahisani ili uendane na kiwango halisi cha uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali katika ukusanyaji wa mapato, Kamati bado ina wasiwasi na kuwepo kwa mianya ya kukwepa kulipa kodi, kunakofanywa na wawekezaji, wazalishaji mali na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Katika kipindi cha takriban miaka kumi iliyopita, Serikali imekuwa ikipoteza mamilioni ya fedha, kutokana ukwepaji wa kulipa kodi. Ni matumaini ya Kamati kwamba, mikakati ya kuwabana wakwepa kodi, itaongezewa nguvu. Aidha, Serikali iweke mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi na wadau mbalimbali, kujua umuhimu na uwajibikaji kwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali, kwa kuifanyia marekebisho Sheria ya Bodi ya Korosho Tanzania. Katika marekebisho hayo, Kamati ilikubaliana kimsingi na mapendekezo ya Serikali kwamba, madaraka ya kukusanya ushuru wa Korosho ghafi, inayosafirishwa nje ya nchi, ufanywe na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, katika kupunguza kuuza nje ya nchi Korosho ghafi, Serikali imeongeza kiwango cha ushuru unaokusanywa hivi sasa kutoka asilimia 8.5 ya bei ya Korosho hadi asilimia kumi, ambayo ushuru huo utagawanywa katika utaratibu ufuatao: Asilimia 6.5 ya makusanyo yote, itapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya zinazozalisha Korosho, asilimia 3.5 ya makusanyo, itapelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina kama Mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na uamuzi huo wa Serikali, kwani utasaidia kuongeza thamani ya Korosho yetu kwenye masoko ya nje ya nchi na hivyo kupata bei kubwa pamoja na kuziwezesha Halmashauri zinazolima Korosho, kufaidika na mapato yatakayotokana na mauzo ya Korosho hivyo, kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya petroli, kwa kuondoa kodi ya *VAT*. Kamati baada ya uchambuzi wa kina, imebaini kuwa, pamoja na kuondolewa na Kodi ya *VAT* katika Kodi ya Mafuta ya Petroli, bado Petroli inaendelea kupanda. Kamati baada ya kupatiwa ufafanuzi na kutafakari suala hili kwa kina, imebaini mambo yafuatayo:-

Lengo la Serikali la kuondoa Kodi ya *VAT* katika mafuta ilikuwa ni kufanya bei ya mafuta zisiendelee kupanda, pale bei hizo zinapopanda katika soko la dunia, kwa vile *VAT* ni kodi inayopanda kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko. Hivyo, badala yake, Serikali imeamua kutoa tozo la kodi kwa kiwango maalum, ambacho hakitabadilika hata kama bei ya mafuta ya Petroli Duniani itapanda, tofauti na ilivyokuwa *VAT* kwenye mafuta. *It is a Revenue Natural Tax Measure*.

Utaratibu huu wa *Tax Measures*, hauwezi kutoa haraka ya unafuu katika bei ya mafuta ya *Petrol* kwa walaji wa nchi, bali matokeo yake yataonekana baada ya muda. Baada ya kujadili kwa kina kuhusu hali hiyo, Kamati imeona kwamba, pamoja na nia njema ya Serikali ya kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi katika mafuta, kuwapatia unafuu watumiaji wa kawaida, ipo haja ya kurekebisha na na kuboresha mfumo wa Biashara ya Mafuta hapa nchini, ili kubaini njia ya kupunguza gharama ya Nishati hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa, wananchi waelimishwe kuwa, kuondolewa kwa kodi ya *VAT* peke yake katika mafuta ya petroli, hakutaweza kushusha bei kwa haraka kama ilivyotarajiwa, kwa kuwa mambo yanayochangia kupanda au kushuka kwa

bei ya mafuta na mengine, yapo nje ya uwezo wa Serikali yetu. Siyo kodi peke yake, ingawa utaratibu utadhibiti upandaji holela wa bei ya mafuta.

Kamati kupitia utaratibu wa Bunge, inapendekeza ikae na Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Wadau wote wa mafuta, haraka iwezekanavyo ili kwa pamoja, tufanye tathmini ya kina ya suala hili la kupanda mno kwa bei ya petroli na baada ya hapo, tuwasilishe maoni yetu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Uwekezaji, Kamati imebaini kuwa, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuwapatia wawekezaji misamaha ya kodi katika baadhi ya vifaa vya huduma wanazohitaji, baadhi ya misamaha hiyo imedidimiza uchumi wa Taifa letu au haina manufaa kwa umma wa Tanzania. Mathalani zipo bidhaa kama vile matunda na mbogamboga, ambazo zinalimwa hapa nchini, lakini jambo la kusikitisha, bidhaa hizo zimekuwa zikiagizwa na wawekezaji kutoka nchi za nje. Aidha, zipo kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania, lakini badala yake hata wapishi wanatoka nchi za nje. Kamati inaamini kuwa, ni muda muafaka sasa Serikali kufanya marekebisho katika kodi mbalimbali zinazohusiana na wawekezaji ili nchi yetu iweze kunufaika na wawekezaji.

Kamati ilibaini kuwa makampuni ya kigeni, hususan katika Sekta ya Madini, yamekuwa yakilipa kiwango kidogo cha kodi ya zuio *(Withholding Tax),* kuliko kile kinacholipwa sasa na makampuni yanayomilikiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri mfumo wa kodi hii, *Withholding Tax,* urekebishwe ili makampuni ya kigeni yalipe kiwango kikubwa zaidi ya kile kinacholipwa na makampuni ya Kitanzania ili kuyashawishi makampuni ya ndani kutumia zaidi huduma za kitaalam, yaani *Technical Service* kutoka kwa Makampuni ya Kitanzania na hivyo, kuongeza ajira kwa Watanzania na mapato ya Serikali kutoka kwenye chanzo hicho. Aidha, kwa kuwa hivi sasa kuna majadiliano yanaendelea katika Makampuni ya Madini na Serikali, kupitia Tume ya Rais ya Kurejea Mikataba ya Madini, Kamati inashauri hoja hii ijumlishwe kwenye mapitio ya Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii, kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Gavana wa Benki Kuu, Ndugu Daud Balali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa J. P. Mathias Mwanyika, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Gray Mgonja na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Ndugu Kitilya, kwa kutusaidia Kamati kufanikisha kujadili na kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu, kwa michango yao makini, ambayo kwa kiwango kikubwa, imesaidia kuboresha Muswada huu. Kama ilivyo ada, naomba niitumie nafasi hii, kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti na Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke,

Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo na Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa. Pia na Makatibu wetu ambao ni Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Hellen Mbeba, Katibu Msaidizi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kwa sababu ni mara ya kwanza, kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia tena kurudi Bungeni kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa wanawake wa Ukerewe, Ilemela, Nyamagana, Magu, Kwimba, Misungwi, Sengerema na Geita, walioniwezesha tena kwa kunipa kura nyingi sana mwaka 2005 na hatimaye kuja kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana watoto wangu watatu; Dorica Nyawazwa, Alex Nyawazwa na Naomi Nyawazwa. Walinisaidia sana katika kuniombea ili niweze kuchaguliwa tena mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA :** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa mara nyingine, kwa kunipa ruksa kwa niaba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kueleza maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2006, pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kusoma maoni ya Kambi ya Upinzani, naomba niwakumbushe watu wa Wizara ya Fedha kwamba, Muswada huu bado ni Muswada, haujawa Sheria, kwa hiyo, walivyoandika *The Finance Act, 2006*, wamekosea. Inawezekana yakawa ni makosa madogo tu ya uchapishaji, lakini kwa sababu kila Muswada ni lazima upitishwe kwanza na Bunge ndiyo uitwe *Act,* baada ya kuwa *assented* na *President*. Naomba makosa kama haya yasirudiwe na pia hata kwa Wizara nyingine, kwa Miswada mingine, ambayo italetwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni yetu kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2006, pamoja na marekebisho yake *(The Finance Bill, 2006),* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu Namba 45(3)(b)(c) na Namba 81(1), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada huu, ambayo inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Ushuru wa Bidhaa, Sura Namba 147 katika kifungu cha 124 na Jedwali la nne, kifungu kidogo cha pili, kinachohusu kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye Huduma za Mawasiliano ya Simu za Mkono, yaani *Mobile Phones Airtime,* kutoka asilimia tano hadi asilimia ili kuongeza Mapato ya Kodi kutoka kwenye chanzo hiki cha Mawasiliano ya Simu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tulishauri katika hotuba yetu ya Upinzani, kuhusu athari zitakazojitokeza kwa mwananchi wa kawaida, kwani tunapoongeza kodi kwa ajili ya *Airtime,* Makampuni ya Simu hayaathiriki, isipokuwa wanaoathirika ni wananchi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali, iliangalie hilo kwa sababu matumizi ya simu za mkononi si anasa, bali ni kitu cha lazima kwa sasa na ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba, uchumi wetu unakua.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* haina athari kwa mfanyabishara, kwa sababu kodi hii hupelekwa kwa mlaji wa mwisho hivyo, kuondoa ushuru huu katika mafuta ya petroli, haina maana kwamba, imempatia nafuu ya bei, mtumiaji wa mwisho, ambaye ni mwananchi wa kawaida. Aidha, suala kama hili la kuondoa kodi ya ongezeko la thamani, kwa wale wanaofanya biashara ya Kahawa hapa nchini, bado halijaweza kuonesha kwamba, linamnufaisha mkulima wa Kahawa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali, itueleze inapoondoa kodi hii inakuwa na lengo la kumnufaisha nani?

Mheshimiwa Spika, vilevile kupandishwa kwa ushuru wa petroli mpaka shilingi 315 kwa lita, ambayo ni sawasawa na ongezeko la asilimia 53, nalo pia Serikali inabidi kuliangalia, kwa sababu halitatui tatizo la bei ya petroli ambapo baada ya *VAT* kuondolewa, bado bei haijaonekana kushuka kama jinsi ambavyo imeelezwa na Msemaji wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kambi ya Upinzani, ilizungumzia suala zima la kuongeza ushuru wa bidhaa za *plasitic*. Tunatambua umuhimu wa kuhakikisha kwamba, tunalinda mazingira kwa kuhakikisha kwamba, bidhaa za *plastic* zinakuwa na bei kubwa ili wananchi waanche kutumia bidhaa hizo, lakini hata hivyo, tulikuwa tumeishauri Serikali, ifanye kitu hiki hatua kwa hatua, kwani kwa sasa matumizi makubwa kwa wananchi bado ni ya bidhaa za *plastic,* yaani mifuko ya *plastic* na hatujaweza kupata mifuko mbadala kwa wingi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaiomba Serikali, iongeze kodi hii hatua kwa hatua, badala ya kuongeza mara kutoka asilimia 15 mpaka asilimia 120.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada, inapendekeza marekebisho ya ongezeko la ushuru wa barabara kutoka shilingi 90 mpaka shilingi 100 kwa lita ya petroli na dizeli. Hii ina maana kuwa, kabla mfanyabiashara hajaweka gharama nyingine za uendeshaji na usafiri, tayari lita moja itakuwa imefikia shilingi 415. Tunauliza je, mwananchi au mnunuaji, anayetegemea vyombo vya usafiri katika shughuli za kila siku, atakuwa amepata unafuu gani katika suala hili?

Tunaitaka Serikali iangalie sana suala hili, kwani inaonesha kwamba, wanaopewa unafuu si wale wananchi ambao wanaathirika moja kwa moja, bali ni wafanyabiashara ambao wanapitisha kodi hizi moja kwa moja, kwa wananchi ambao ndiyo watumiaaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba, Muswada huu ni muhimu sana kuifanya Serikali ianze kuongeza mapato na kutumia fedha ambazo zinapatikana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, baada ya maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri atayatoa, kuhusiana na haya ambayo tumeyauliza, Kambi ya Upinzani Bungeni, itaunga mkono Muswada huu ili Serikali ianze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza awali, nina wachangiaji sasa wanne; Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Juma A. Njwayo na Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye. Nitawapa nafasi kwa mpangilio huohuo, nikianza na Mheshimiwa Paschal C. Degera.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Muswada huu wa fedha wa mwaka 2006.

Kabla ya yote, napenda nitumie nafasi ya kwanza kabisa, kumpongeza Waziri, kwa kuleta Muswada huu Bungeni ili tuweze kuujadili na kuupitisha.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuleta Muswada huu Bungeni hapa ni kutokana na hotuba ya Bajeti, ambayo Waziri aliitoa na alitoa mapendekezo mbalimbali na marekebisho mbalimbali ya kodi mbalimbali na Muswada huu ndiyo unakidhi mahitaji haya kwamba, sasa tutunge Sheria, ambayo itamuwezesha Waziri aweze kufanya kazi ya kukusanya mapato, kwa vile vyanzo ambavyo amependekeza vingine vipya na vile ambavyo amerekebisha. Kwa hiyo, ni Muswada muhimu na mimi nipo hapa, sipingi chochote isipokuwa nachangia kidogo tu.

Baada ya kusema maneno haya ya awali, naomba sasa nichangie maeneo mawili ya Muswada wenyewe, nianze na sehemu ya nane ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane ya Muswada, inapendekeza kodi ama ushuru uongezwe ule wa *road tour* katika bidhaa ya Petroli na Dizeli na kama Muswada ulivyosema ni kwamba, anatarajia ama anapendekeza kuongeza shilingi kumi kwa lita kutoka shilingi 90 ya sasa kwenda shilingi 100 kwa bidhaa zote mbili za Dizeli na Petroli.

Tunajua athari ya kuongeza mafuta, wote tunafahamu gharama za maisha zitaongezeka sana, siyo sana lakini kwa kiasi fulani, kwa sababu petroli na dizeli ni bidhaa ambazo zinatumiwa na kila mtu na katika shughuli zote za uzalishaji. Ukienda

kwenye kilimo, viwanda, bidhaa hii inatumika sana kwa hiyo, tunategemea kwamba, kwa kweli tunaongeza gharama ya maisha kwa kila Mtanzania, yule ambaye tuliahidi kwamba, tutaboresha maisha yake lakini sasa tunaendelea kuongeza bidhaa hii ni kwamba, itaathiri sana maisha ya Watanzania wote.

Lakini hiyo siyo hoja yangu, nilikuwa naikumbusha Serikali tu kwamba, kuongeza bidhaa hiyo maana yake ni kuongeza gharama ya Mtanzania ama Watanzania wote. Lakini hoja yangu niliyosimama hapa ni suala la mgawanyo wa mapato hayo, yanayopatikana katika Mfuko wa Barabara, hiyo ndiyo hoja yangu. Tunaelewa kwamba, tunaongeza kwa nia njema tu kwa sababu kilio cha barabara katika nchi hii ni kikubwa sana na ninafikiri ndicho Waziri amesema hapa kwamba, tunahitaji tupate mapato ya kutosha, kuweza kuongeza Mfuko wetu wa Barabara ili tuweze kufanya kazi ya kuboresha barabara nchi nzima.

Lengo hilo mimi nakubaliana nalo kabisa, naafiki kabisa ongezeko hili, lakini sasa ninachohoji ni kwamba, pamoja na lengo hilo zuri, lakini pia tuangalie na mgawanyo wa pesa zinazopatikana kupitia Mfuko huo. Mgawanyo wa sasa hivi kwa kweli hauridhishi, mimi naweza kusema na Wabunge wengi wamelalamikia sana mgawanyo wa Mfuko wa Barabara uliopo hivi sasa. Labda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, mgawanyo wa pesa zinazopitia Mfuko wa Barabara ni kama ufuatao:-

Wizara ya Miundombinu, inatengewa ama inachukua asilimia 70 na Wizara ya TAMISEMI kwa niaba ya Halmashauri zetu zote katika nchi yetu hii inapewa asilimia 30 tu. Mimi nafikiri tungependekeza tuongeze, ama uwiano huo nafikiri ungebadilishwa ili angalau TAMISEMI nayo ipate mgao mkubwa zaidi, sisemi utakuwa nusu kwa nusu, lakini angalau tuwaongezee sababu ninazo mbili: Moja, mtandao wa Barabara za TAMISEMI, kwa maana ya Halmshauri zetu ni mkubwa sana nchi nzima, kwa hiyo, lazima tuangalie uzito wa barabara na ukubwa na mtandao wa barabara katika Halmashauri zetu, kwa hiyo, tunahitaji fedha ili tuweze kuhudumia hizo barabara. Hizo barabara ndizo zinazowafikia wananchi wa kawaida, kwa hiyo, mimi ningependekeza kwamba, angalau watuongeze hiyo asilimia kutoka 30 iliyopo sasa ifike angalau 40, itatupa uwezo sisi Halmashauri kuweza kuhudumia barabara zetu ambazo ni muhimu sana kwa uzalishaji hasa kule vijijini. Kwa maana hiyo, mimi napendekeza Waziri aangalie uwiano wa mgao wa Mfuko wa Barabara kutoka ile ya awali ya asilimia 70 kwa ajili ya Wizara ya Miundombinu na ailimia 30 kwa TAMISEMI, ingeweza kuongezwa au kuweza kurekebishwa ili miundombinu ichukue asilimia 60 na TAMISEMI iweze kuchukua asilimia 40, ambayo itasaidia kuboresha barabara za vijijini.

Sababu ya pili, ambayo nimeona niitoe, kwa nini napendekeza hivyo ni kwamba, Wizara ya Miundombinu ina vyanzo vingi vya kupata pesa kwa ajili ya kutengeneza barabara zake. Pamoja na Mfuko huu, Wizara bado ina bajeti ya Serikali ambayo tumeipitisha, Wizara pia inapata misaada mbalimbali, ambayo pia inaingia kwenye Mfuko wa Wizara hiyo na Wizara pia inaweza kukopa kutoka nje.

Kwa hiyo, bado tuna vyanzo vingi, lakini ukiangalia *TAMISEMI* kwa maana ya Halmashauri zetu, chanzo ni hicho hicho, hatuna vyanzo vingine. Kwa hiyo, mimi ndiyo

maana nimependekeza kwamba angalau tungeweza kuangalia huo mgao ili kuweza kurekebishwa kwa faida ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo, naomba sasa nizungumzie pia Sehemu ya Sita ya Muswada. Katika Sehemu ya Sita ya Muswada wa Mheshimiwa Waziri, amependekeza kufuta kodi ama ada za magari yanayotumia barabara za Miji. Alipokuwa anabadilisha maeneo mengine alielezea vizuri sana kwa sababu gani ama sababu zipi zinamfanya aweze kufanya marekebisho hayo. Lakini kwa hili, hakutoa sababu ni kwa nini anataka kurekebisha ama kuondoa kodi hiyo. Ni kwa sababu tunashindwa kukusanya ama ni kero, ama ni kitu gani? Nataka kufahamu sababu za kuondoa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia mimi nafikiri nimshukuru tu na kumpongeza kwamba kuondoa hiyo kodi inaweza ikawa inapunguza kero na inawezekana ni gharama kubwa kukusanya kodi hiyo au ada hiyo, ndiyo maana labda amependekeza. Lakini ninachoomba hapa, ama ninachotaka kupendekeza ni kwamba, hicho ni chanzo kimojawapo cha Halmashauri husika cha kodi ama ada hiyo. Ni moja ya chanzo cha mapato. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha hajasema kwa zile Halmashauri ambazo zitapoteza chanzo hicho, Serikali Kuu ina mpango gani wa kufidia pengo hilo. Hiyo ndio hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nipate jibu kwa Halmashauri ambazo zitapoteza fedha kutokana na kufutwa kwa ada hiyo: Je, Serikali Kuu ina mpango wa kufidia? Hiyo ndio hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwa kifupi sana na ninaomba niunge mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kidogo Muswada huu muhimu wa Waziri wa Fedha. Kwanza, napenda kumpongeza sana kwa alivyouwasilisha, umeeleweka vizuri sana na baadhi yetu hautatupa taabu kuchangia.

Mheshimiwa Spika, eneo mojawapo ambalo nataka kuchangia ni katika ile Sehemu ya tatu ya Muswada. Kwanza, napenda kuipongeza sana Serikali kwamba, sasa magari yanayoingizwa nchini ni magari ambayo hayatutii hasara kwa kuweka ushuru maalum kwenye magari ambayo yana zaidi ya miaka 10 au kwa lugha ya mjini, mikweche.

Mheshimiwa Spika, pengine wananchi wa kawaida wanaweza wasilielewe hili suala la kuzuia magari yenye umri mkubwa kuingia hapa nchini. Kwenye nchi zilizoendelea huko, magari pamoja na matairi huziharibu kwa ajili ya Sheria za Mazingira zilivyo ni gharama zaidi kuliko kupaka rangi *engine* na likaonekana ni safi, halafu ulisafirishe kuja Tanzania na uliuze ni rahisi zaidi kuliko kutafuta mahali pa

kulitupa. Kwa hiyo, kama hatukufanya hivyo, nchi yetu itakuwa ni mahali pa kutupia magari mabovu.

Mheshimiwa Spika, nadhani mantiki hii ingelijulikana kwa wananchi kwamba hiyo ndiyo hali ilivyo. Haya magari mengi yanakuja kwa bei rahisi kabisa, ni gharama kwa mtu anayetumia kule, aliyeko Japan au Uingereza kuliharibu hilo gari, hakuna mahali pa kuliharibu hiyo gari. Kwa hiyo, ni lazima kulisafirisha kwenye meli na kuliuza kwa bei ndogo kuliko kutafuta mahali pa kuliharibu gari pamoja na tairi zake. Nadhani msingi huu ukijulikana, itatusaidia sana kuelewa kwamba hatutaki kuzuia watu ambao hawana uwezo, wasinunue magari hayo. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa hatua hizi za kuzuia uharibifu wa mazingira katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya Tatu katika lile jedwali la nne, kuna orodha pale ya Sigara. Sasa nataka tu tupate ufafanuzi kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na tulipotembelea viwanda vya kutengeneza Sigara hapa nchini, tuna viwanda viwili sasa. Tuna Kiwanda cha *TCC,* halafu tuna kiwanda cha *Master Mind*. Tulikuta pale kuna sigara zinazotengenezwa za urefu tofauti. Kuna sigara fupi, lakini sigara hizi fupi zinatozwa bei sawa na sigara ndefu.

Labda tungependa kupata maelezo kwa sababu wale wanalalamika na sisi kwa kweli tuliwasukuma waendelee kwa sababu ni wazalendo watupu wanaofanya kazi pale. Sasa ifike mahali tuweze kuweka taratibu ambazo zinatia hamasa wazalishaji wa hapa nchini badala ya kuwakatisha tamaa. Tofauti ile ya sigara ndefu na zile sigara fupi itazamwe hiyo, tusije tukawakatisha tamaa hawa. Wametumia akili kwa kweli kwamba ile *packet* ukiishika ni ndogo tu inaingia kwenye mfuko na wametuomba sisi kama Wabunge kwamba litazamwe hili.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana kwenye sehemu ile ya tano ya Muswada kutoa unafuu wa kodi kwa watu binafsi ambao watachangia Mfuko wa Elimu. Hii ni hatua nzuri sana kwa sababu nadhani ni Makampuni ndiyo yalikuwa yanachangia. Hii itasaidia sana hata wananchi wafanyabiashara wadogo kwa maana ya mtu binafsi kuweza kuchangia vizuri sana kwa sababu hapo kuna unafuu. Sasa hili litangazwe zaidi kwamba ukichangia katika Mfuko wa Elimu, kuna unafuu katika shughuli zako unazozifanya, utapunguziwa kodi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo mimi kwa kweli limenifurahisha sana ni hili la kuondoa ada za magari yanayopita katika barabara za Mijini. Ni biashara hii, lakini ina adha kubwa sana. Kwa sababu mwananchi anaweza kuwa na haraka , anakimbilia Benki amesahau kukata ada ile, anakuta gari lake limewekwa kwenye *breakdown* linaburuzwa. Unakuta katika kuburuzwa huko, wakati mwingine kunaziba na barabara nyingine, kufunga funga minyororo ile.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kukuta mahali kuna ugomvi katika Mtaa wa Mkwepu kati ya mkusanyaji ada halafu na Askari wetu, mmoja wa Jeshi la Wananchi. Alikuwa anakimbilia kazini na amekwenda pale Benki, anatoka Benki anakuta gari imewekwa kwenye *breakdown* linaburuzwa na huku anataka kwenda kufanya shughuli nyingine kule. Ilikuwa kazi siku hiyo! Sasa nadhani tupunguze hizi ghasia ghasia za

kukusanya watu Mijini kwa ajili ya kuangalia magari yanayoburuzwa. Kwa hiyo, sisi tunashukuru sana, mimi hasa kwamba kwa kweli hii ni moja ya sheria au taratibu ambazo zina adha kubwa sana. Kwa hiyo, ninaunga mkono sana hili kwa kweli tena lingeanza jana wala sio kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la kodi ya kahawa ambayo imesindikwa hapa nchini. Nilikuwa nataka kupata ufafanuzi: Je, chai inahusika nayo au labda iko katika sheria ya Chai? Kama haipo, tungetazama na mazao mengine. Kwa sababu hapa nchini tumesema tunataka kuongeza ajira, sasa ajira hizi zinaweza kuongezeka kwa kutumia mazao ya kilimo vikifunguliwa viwanda. Kwa mfano, kahawa, chai vilevile tunapata taabu sana na mimi ni mkulima mdogo wa chai. Tunapata taabu sana tunakwenda kwenye Mnada Mombasa.

Lakini tatizo ni kwamba, uwezo wa kuchakata chai na kuipa thamani na kuiweka kwenye vipaketi ambavyo vinakwenda moja kwa moja kwenye hoteli, bado nguvu hiyo ni ndogo na ni viwanda vichache.

Kwa hiyo, mimi ningeshukuru kama Serikali ingeweza kuhamasisha wakulima wa chai hawa wajenge viwanda vingi vya *blending* ili chai kwa kweli inayouzwa iwe ni ile ambayo ni *blended* tayari au imeshatengenezwa tayari kwenda kuuzwa rejareja au kwa jumla.

Tunavyo viwanda vichache sana hapa, nadhani kuna *TATEPA*, *Tanzania Tea Blenders* na wengine wadogo. Tunashukuru sana kwamba kile Kiwanda cha *Tanzania Tea Blenders* kilikuwa cha Serikali, kimebinafsishwa, lakini waliobinafsishwa wamefanya kazi nzuri sana na kimeongoza, kimepata vikombe, wakati wa Maonyesho ya Kimataifa Kiwanda kile kilishika nafasi mara mbili kwa ubora na vilevile kwa jinsi ambavyo wanafanya *packing* yao.

Kwa hiyo, tungelisukuma sana hili pamoja na ile ya Korosho kwamba tusipeleke sasa vitu ambavyo havijachakatwa, tunakula hasara kubwa sana. Vilevile, hata gharama ya kupeleka, maana yake unapeleka mzigo mzito sana wakati kama ingechakatwa hapa, basi thamani ingekuwa kubwa na nchi ingepata faida, zaidi na ajira vilevile ingeweza kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii. Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha vizuri Muswada wake. Aidha, naomba pia niwapongeze Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mapendekezo mbalimbali waliyoyatoa, ni mapendekezo ya busara kabisa kwenye Muswada huu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala yangu ni machache na nita-*base* kwenye *Part Two* ya Muswada huu hasa pale panapohusu *Amendment* ya mambo mbalimbali ya Bodi ya Korosho na yale yanayohusu korosho.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nataka kutoa pongezi kwa Serikali kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, niliona kulikuwa na matatizo kidogo ambayo niliyasemea sana. Sasa nataka kuipongeza Serikali kwamba Serikali yetu ni sikivu sana.

Muswada wa awali, wananchi wanaolima korosho walikuwa wanapewa asilimia tano ya *export levy,* lakini baada ya mijadala na kelele za hapa na pale tuliahidiwa kwamba wanakwenda kutafakari kama Serikali. Sasa leo naona asilimia 6.5 hapa. Nawapongeza sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa sababu yangu kubwa kwamba, hii asilimia 6.5 itakayokwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya inakwenda kuzalisha korosho ili iongeze uchumi wetu nchini. Kama mtakumbuka, wananchi kwamba karibu *dollar* milioni 800 kila mwaka zinaingizwa nchini kutokana na korosho. Kwa hiyo, hii inakwenda kuzalisha korosho. Nadhani hapa kuna mambo mengi mazuri yatakuja baadaye. Ndiyo maana nimesema ni vizuri nikaipongeza Serikali kwa kuwa sikivu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo na pia naomba niipongeze Serikali sasa kwa kuondoa hii *export levy* iliyokuwa inakusanywa na Bodi ya Korosho. Kulikuwa na matatizo mengi sana. Sisi ni wakulima wa korosho, tunayajua. Kwa hiyo, naamini sasa kwa kuwapa *TRA* watafanya vizuri. Lakini nitoe rai kwamba tusifanye makosa kule, msimu ukiisha hizo fedha zipelekwe kwa wananchi wale wakafanye mambo kwa haraka ya kujenga huduma za jamii na mambo mengine ya kiuchumi kwenye Wilaya husika za korosho.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na pongezi hizi ninazozitoa kwa Serikali, nataka kutoa wasiwasi wangu. Mimi siridhishwi na utendaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwenye suala la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mifano mingi. Mheshimiwa Waziri Mkuu jana ameona pale, watu wametengeneza utaratibu wa ugawaji wa mbegu na mbolea, lakini *sulphur* na pembejeo nyingine zinazohusu korosho zimesahauliwa na jibu la mkato pale lilikuwa linasema tunakuja baadaye. Hivi huko Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika hakuna *division of labour*? Hakuna mtu anayeshughulikia kahawa? Hakuna mtu anayeshughulikia korosho? Hakuna mtu anayeshughulikia mbolea? Kuna tatizo gani katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika? Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi naomba ulione hilo.

Mheshimiwa Spika, namtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu tarehe 8 Julai, 2006 tulikuwa wote Mtwara kukagua Mradi wa *Mnazi Bay.* Mimi nilifedheheka sana, Waziri Mkuu wangu anaonyeshwa mabango pale *sulphur, sulphur* haikuwa vizuri, tena Serikali ya kutukuka hii yenye ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya inaaibishwa, inakuwaje? Kwa kweli sikujisikia vizuri kabisa Waziri Mkuu ananyanyaswa pale mpaka aliamua kumpigia simu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika aje kule. Kwa nini bwana? Kuna tatizo gani? Mimi ninamwomba kama kiranja wa Serikali alione hilo.

Kuna haja ya kuweka utaratibu mwingine katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mambo kule yanakwenda legelege, hayafanani na mpango wetu wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama sikosei, mwanzoni mwa mwezi Agosti, mwaka huu, maana nimetaja hili la *sulphur* na pembejeo, sisi wakulima wa korosho na wadau mbalimbali tuliitwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Dar es Salaam kwenye Ukumbi wa Ofisi yake pale, tuliahidiwa kwamba tunapewa bilioni moja ili isaidie kupata pembejeo mbalimbali. Lakini cha kusikitisha, baada ya Waziri Mkuu niseme kumlazimisha Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwenda Mtwara, akajibu maswali ya wananchi, alipofika kule mimi nilimwona kwenye televisheni akisema kwamba hana namna, hakuna *the best alternative* anaweza kufanya ili watu wale wapate *sulphur* kule, wakati *sulphur* sasa ndiyo wakati wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa unapokuwa Serikali, halafu unawaambia wananchi kwamba hakuna cha kufanya, hivi wanafanyaje? Sisi wakulima wa korosho tujionaje? Kwamba korosho isizalishwe na nilitangulia kusema hapa kwamba zaidi ya *dollar* milioni 800 zinaingia nchini kutokana na korosho. Sasa unaposema huna namna, hivi tunafanyaje?

Kwa hiyo, korosho isizalishwe na sasa kuna *shortage* ya *sulphur* kule. Sasa kwa sababu liko hili suala, mimi naiomba Serikali itafute namna yoyote hata kwa kukopa mahali ili wakati wa msimu mambo yaende vizuri. Hali ni mbaya kule, tunapigiwa simu na hii ni dalili pengine mnataka tusirudi tena Bungeni mwaka 2010 Waheshimiwa Wabunge wa kule. Maana kwa Mtwara sera ni korosho, siasa ni korosho na ndiyo pekee inayoleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi Wilaya yangu ya Tandahimba ninayotoka mwaka 2000 ndiyo ilikuwa *full recognized* kuwa Wilaya. Tulikuwa hatuna hata Shule moja ya Sekondari. Lakini kwa sababu ya *giant* ya korosho, leo ninavyoongea mwaka 2006 tayari tuna Shule za Sekondari 12 na zinatokana na korosho hiyo. Sasa kama mnavyotuacha kama kuku asiyekuwa na mwenyewe, mimi sielewi, napata shida sana. Lakini tatizo langu mimi, najua Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hana matatizo, Waziri Mkuu wetu hana matatizo, lakini kuna matatizo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Tafadhali naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu utusaidie. Kuna matatizo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kuna haja ya kuleta jambo jipya pale tuone ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu kwa kweli ilikuwa ni hiyo, sikutaka leo niongee sana, lakini kwa kweli kama nilivyosema, mimi ni mkulima wa korosho na ninawawakilisha watu wa korosho hapa nakereka sana.

Mheshimiwa Spika, nimalize tu kwa kusema kwamba, msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Nawashukuru kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Njwayo, ujue Spika amekuachia tu, lakini hoja hii kwa kweli namna ulivyochangia, hakuna uhusiano wa moja kwa moja na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Lakini kwa kuwa korosho ni zao muhimu, basi tunaona bila shaka Serikali imesikia na wananchi wako wamesikia unavyowatetea.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwa kifupi sana katika Muswada huu wa Sheria ya Fedha. Ninaomba kuthibitisha kwamba, nitajielekeza sehemu moja tu ambayo ni Sehemu ya Kumi ya Muswada kipengele cha 31 na 32.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyoletwa yanahusu Sheria iliyopo sasa ya Uwekezaji na inapendekeza marekebisho mbalimbali hasa kuhusu *incentives* kwa wawekezaji waliopo, mimi nitazungumza mawazo yangu kuhusu suala la kuongeza mapato kwa kupanua mapato kupitia wigo wa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, suala hili linalizungumza mara ya pili leo, nilishawahi kulizungumza kama hoja huko nyuma katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Lakini leo kwa sababu ninataka nilizungumze kwa maana ya kusaidia Serikali katika maana ya uwezeshaji na uingizaji wa mapato, basi nafikiri hapa ndipo nitoe mawazo yangu ingawa hayataingia moja kwa moja katika majibu ya hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kupongeza sana kazi nzuri inayofanywa na *TIC* hapa nchini kwa maana ya kupanua wigo wake katika kukuza uchumi wa nchi hii katika uwekezaji. Pamoja na kwamba wanafanya kazi katika mazingira ya Bajeti finyu, lakini kazi wanayoifanya na juhudi wanayofanya kutuletea wawekezaji au kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ulikuwa katika sehemu hiyo na ulifanya kazi nzuri na mimi nilithibitisha. Hata huyo uliyemuachia kazi anafanya kazi nzuri kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ukiwa katika Ofisi hiyo, ulianzisha utaratibu wa kuanza sasa kupanua wigo wa Ofisi ya *TIC* na kupeleka katika Kanda, ninaelewa zoezi hili linakwenda vizuri ingawa kwa taratibu. Sasa tuna labda Vituo viwili au vitatu tu katika Kanda, lakini tunategemea kwamba Kanda zote zitapata vituo. *Challenge* ninayotaka kuitoa mimi hapa ni moja, kwamba, ni vizuri sasa Serikali ingekubali au ingeruhusu kupitia sheria kwamba Mikoa na yenyewe ipewe uwezo wa kisheria wa kufanya shughuli zake za uwekezaji ambazo zinahitaji fedha. Kusipokuwa na sheria, Mikoa haiwezi ikafanya yale ambayo inaweza kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, Mikoa iwe bunifu kwa kutumia *Local Incentives* wabunifu wa kutafuta maeneo ya uwekezaji wao wenyewe bila kungojea *Centre.* Watafanya nini? Kinachoweza kufanyika na ninaelewa wanatamani kufanya, ni kujaribu kutenga maeneo ya uwekezaji. Sasa huwezi kutenga eneo la uwekezaji ukaliacha hivyo kama pori.

Mheshimiwa Spika, lazima ujenge na kuandaa miundombinu, uandae barabara zinazokwenda kwenye maeneo hayo, uandae umeme, uandae vilevile maji ili mwekezaji yeyote wa ndani hasa akitaka kuwekeza, basi kuwepo na eneo la kuanzia kazi ambalo liko tayari kabisa kufanyiwa kazi. Sio mtu anakwenda porini na kuanza kufyeka misitu yeye, hapana. Mikoa ifanye hiyo kazi, halafu yule mwekezaji atakuja afidie. Anaweza kuja kufidia hiyo gharama ambayo Mikoa itakuwa imeshatumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana, sasa wakati umefika wa kuhamasisha hiyo, kwa sababu litakuwa limetujengea wigo wa mapato, lakini vilevile litakuwa ni njia ya kukuza uchumi katika Mikoa na vilevile uchumi wa wananchi katika Mikoa yao. Hatuwezi kwenda katika *speed* hii tuliyonayo ya kungoja wawekezaji wanaoletwa Kitaifa *through TIC*, itatuchukua miaka 20.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji ninaouzungumzia hapa ni ule uwekezaji mdogo mdogo. Wazo hili ninavyoliona mimi, linaweza kabisa likaoana na hoja nzuri ya *MKURABITA,* kwa maana kwamba, kama wananchi wataweza kuthamanishiwa mali zao, wakapimiwa, wakapewa mikopo, hawatasita kuanzisha viwanda vidogo vidogo ambavyo navyo pia vitaajiri hata kama watu watano watano tu, inatosha kabisa. Kwa sababu sisi tunataka katika kipindi hiki cha miaka mitano, tuwe tumejenga ajira kwa watu milioni moja.

Lakini kwa njia hii tutajenga ajira hata kwa zaidi ya watu milioni tatu. Tunaweza kabisa! Hakutakuwa na haja ya watu kuzurura Mijini na wapi kutafuta ajira, eti kuna ajira mahali fulani! Huko huko Mikoani tukishaandaa mazingira kama haya tutajenga ajira na tutakuza uchumi *and therefore,* hatutakuwa tunanyang'anyana haya mapato madogo ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninaomba sana hili lisichukue muda mrefu kulitafutia namna ya kuliwekea sheria ambayo itawezesha Mikoa yenyewe ifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, juzi, Mheshimiwa Rais alikuwa anazungumzia nafikiri katika Mkoa wa Mara, aliwaambia viongozi kwamba lazima wawe wabunifu, wao wenyewe wajenge mazingira ambayo wataweza kupata nafasi ya kuisaidia Serikali katika kukuza uchumi wa nchi hii. Sasa hii ni njia mojawapo ambayo inaweza ikasaidia kabisa.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilikuwa nazungumza na Balozi wa Indonesia, yeye aliniambia, katika Visiwa vilivyoko kule huwezi kumaliza kilometa mbili, tatu, utakuta viwanda vidogo vidogo vina watu watano, sita, wengine hata katika kaya yao wamejiajiri humo humo.

Mheshimiwa Spika, sasa tuige mifano kama hiyo, tuji-*centralize* kupeleka Mikoani, tunaweza tukasema hatuna *manpower,* lakini *manpower* iko kule. Kuna Sekretarieti, watagawana wenyewe wafanye hizi kazi ili mradi wenyewe wapate uwezo wa kuweza kufanya hizi kazi walizojiwekea kila Mkoa na kila Wilaya. Wana *priorities* zao, wanajua namna gani watakuza uchumi katika Mikoa au katika Wilaya zao. Basi watumie akili zao walizonazo kuweza kukuza maeneo hayo ili kuisaidia Serikali kuweza

kupata ajira, kuweza kukuza uchumi, kuweza kuiweka nchi hii iweze kuwanufaisha wananchi wakawa matajiri katika maeneo waliyoko.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu hoja katika Muswada huu wa Sheria ya Fedha 2006. Kabla sijaingia katika kujibu hoja hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua wale wote ambao wamechangia kwanza kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza kwanza ni Mheshimiwa Esther Nyawazwa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Msemaji Mkuu kwa upande wa Upinzani, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Cynthia Ngoye. Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Rostam Azizi na Mheshimiwa Mohammed Dewji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu kwa kweli wote waliozungumza, kimsingi wameunga mkono Muswada huu. Wametoa mawazo mbalimbali ambayo kwa kweli hata mengine yale ambayo labda pengine moja kwa moja hayalengi katika Muswada huu, lakini naweza kusema kwamba yatasaidia katika Wizara mbalimbali katika utekelezaji wa kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala zima la kuongeza jitihada za mapato upande wa *TRA* limezungumzwa. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hii ni ajenda namba moja kwa sababu tunaamini ni muhimu kabisa ili kuweza kutekeleza yale yote tuliyoyasema na kujenga uwezo pia wa uchumi. Uwezo wa kutotegemea sana Wahisani, suala hili ni la umuhimu mkubwa. Kwa hiyo, tutalitekeleza.

Mheshimiwa Spika, Suala la elimu nalo litaendelezwa kwa kupitia njia mbalimbali ikiwemo Redio. Lakini kama mnavyoelewa hata hivi majuzi kwa mara ya kwanza Wizara ya Fedha imeshiriki katika Maonesho ya Saba Saba na Nane Nane na ilikuwa nafasi nzuri sana ya kuelimisha wananchi katika masuala ya kodi.

Mheshimiwa Spika, suala la Kodi ya Zuio na Makampuni ya nje nashukuru kwamba Kamati ya Fedha na baadhi ya waliozungumza imeona kwamba ni bora tungoje suala hili lishughulikiwe na Kamati ile ambayo iliundwa na Mheshimiwa Rais kwa sababu hili ni mojawapo ambalo lipo katika maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, hili nalo nasema kwamba kimsingi kama tulivyosema, Serikali tunakubali, lakini litaingia katika mapendekezo yale ya ujumla.

Suala la petroli na bei ya petroli, napenda kusema kwamba suala hili kwa kweli tunajua kwamba hivi sasa petroli inazidi kupanda huko nje na hasa hasa kutokana na vita. Nafikiri kwamba, kama ingekuwa hatukufanya marekebisho haya tuliyokuwa tumefanya, basi petroli ingepanda zaidi.

Manufaa kwa kweli ya mfumo huo ni kwa kodi zote sasa zinazingatia ujazo *(Volume Base)* na sio thamani, kwa sababu hakuna *VAT* lakini kutakuwa na *excise duty.* Kwa hiyo, kodi itabakia ile kwa kila lita hata kama bei zitabadilika, kwa sababu sio *percentage* ya *volume,* lakini ni kutegemeana na *excise duty* ambayo italipa. Tunategemea kwamba mabadiliko yataonekana, lakini la muhimu pia ni kwamba, mafuta ya taa bei imekuwa ya chini na tunajua kwamba wananchi wengi sana wenye kipato cha chini wanatumia mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia la *Plying Fees* ya magari katika Miji, nilisema kwamba, hili hasa zaidi ilikuwa Dar es Salaam ambazo ada hii ilikuwa inatozwa. Ni jambo ambalo tunasema kwamba ni la kuudhi. Mara nyingine na ndiyo maana tuliona kwamba ni heri kuliondoa na hata pale ambapo tuliomba kupata mapato kutoka *Dar es Salaam City,* ni kiasi gani ambapo wamekusanywa, basi mapato hayo hatukuonyeshwa na hayakupatikana kwa sababu nafikiri hawakusanyi fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasema kwamba, hili limeondolewa kwa sababu linaudhi. Lakini pia kama kodi hii kwa mfano kuna maeneo ambayo wanasema kwamba walikuwa wanakusanya na wakaweza kuhakiki kwamba ni kweli kuna fedha hizi ambazo zilikuwa zinakusanywa, basi Wizara ya Fedha itakuwa tayari kulipia fedha hizo. Lakini iliona kwa sasa iliondoe.

Mheshimiwa Spika, suala la kodi ya kahawa ambayo inasindikwa na ambayo imefanyiwa marekebisho ya *VAT* na suala ni kwamba: Je, kwa upande wa chai ni vipi? Napenda kusema kwamba chai ndio ambayo ilipata nafuu mwanzo kabisa miaka miwili iliyopita. Kwa hiyo, kwa kufanya kwa kahawa ni kufuata kile ambacho kilichofanywa kwa upande wa chai.

Mheshimiwa Spika, suala la uwiano wa mgao kwa Mfuko wa Barabara, niseme kwamba suala hili lipo ndani ya Sheria ya Mfuko wa Barabara na kwa maana hiyo, tumepokea maoni ya Mheshimiwa Degera na tutayafikisha kwa Waziri ambaye anasimamia Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni juu ya plastiki, kwamba, ongezeko la kodi ya plastiki ufanywe kwa utaratibu ili kupata bidhaa mbadala. Ni kwamba, labda lisingefanyika kwa sasa. Niseme kwamba suala hili la mifuko ya plasiki. Mifuko ile laini sana ya plastiki, suala hili kwa kweli sio mara ya kwanza kuzungumzwa Bungeni.

Suala hili limeanza kuzungumzwa Bungeni toka mwaka 2004 na wakati huo wadau wengi sana mwaka 2004 walipendekeza kupiga marufuku. Lakini Serikali ikatoa muda wa kupata bidhaa pamoja na mifuko mbadala ili wananchi kujiweka tayari. Kwa hiyo, suala hili kwa kweli Waheshimiwa Wabunge sio la sasa ni suala ambalo limekuwa limezungumzwa hata humu Bungeni toka mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya sigara fupi za *Master Mine* zitozwe kodi nafuu kuliko sigara ndefu. Kabla ya mwaka 2005, ushuru wa bidhaa kwenye sigara ulitegemea urefu ambapo sigara yenye urefu wa milimita 70 zilitozwa

ushuru zaidi ya zile zenye urefu pungufu wa huo. Urefu wa sigara ulichukuliwa kama kigezo cha ubora na thamani ya sigara husika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 tulianza kutengeneza sigara zenye milimita 65 hadi 68 ambazo zina ubora na bei sawa sawa kama zile zenye urefu wa milimita 70. Kwa kuendelea kutumia utaratibu wa zamani upungufu wa milimita moja, ningepelekea Serikali kupoteza mapato zaidi ya shilingi 3,000 kwa kila sigara 1,000. Utaratibu wa sasa unalenga kuzingatia hasa hasa ubora wa sigara kwa misingi ya kuwa na kichungi kwa maana ya *filter* au kutokuwa na kichungi. Kwa hiyo, hii ni hatua ambayo inalenga kulinda mapato ya Serikali kuziba mwanya uliojitokeza katika utaratibu wa ule wa zamani.

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia kwamba, Waheshimiwa Wabunge wameliona suala hili la magari kutozwa asilimia 20 zaidi na kama alivyoeleza Mheshimiwa Shellukindo, ni kwamba, kwa kweli magari ya zamani pengine ni gharama zaidi. Lakini nataka kuweka wazi kwamba, magari haya ni magari madogo na hayahusishi magari yale ya mizigo. Kwa hiyo, yale ya mizigo yatakuwa hayahusishwi na asilimia 20 ya juu ambayo tunayozungumza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nirudie tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Namwona Mheshimiwa Mercy amekalia kiti cha Kiongozi wa Upinzani, sijui anaelewa uzito huo au? Ahsante sana.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2006

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 32

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 44

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kueleza jambo ambalo nafikiri Katibu hakulifanyia utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 12...

**MWENYEKITI:** Tuangalie ulitakiwa kufanya nini Mheshimiwa? Kwa sababu tulikofika sasa ni kifungu cha 44.

**MHE PASCHAL C. DEGERA:** Ni kwamba kuna marekebisho yamefanyika. Huu Muswada hauna kifungu cha 44, unaishia kifungu cha 43. Ndiyo maana nilitaka kukurejesha wapi wamefanya marekebisho ili tuweze kufanya hayo.

**MWENYEKITI:** Wewe uliyonayo ni ipi? Maana yake marekebisho yamekwishawasilishwa hapa.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Katika *amendments,* kifungu, ama sehemu ya 16 iliondolewa yote. Kwa hiyo, zilizobaki ni 43, sio 44.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa inabidi usome Muswada na mabadiliko, ndio unapata jibu. Sasa wewe unasoma Muswada tu naona.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Hapana, nimesoma mabadiliko, ndiyo nasema kwamba mabadiliko yamefanywa vifungu vimepungua vimekuwa ni 43 badala ya 44.

**MWENYEKITI:** Sawa hakuna ubaya wowote. Mabadiliko ni dhahiri yanabadilisha Muswada wenyewe ndiyo maana sasa tunasoma 43. Ulikuwa na maana Katibu alisoma 44?

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sawasawa nimekuelewa. Hilo ni kosa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana. Anavyozungumza Mheshimiwa Mbunge ni sahihi. Kwa sababu marekebisho tuliyonayo hapa yanazungumzia kwamba kifungu cha mwisho ni 42, ndiyo kifungu cha mwisho.

**MWENYEKITI:** Kilichokuwa 44 sasa ni 43.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo. Hapa 44 kinakuwa ni 42

**MWENYEKITI:** Inakuwa 42!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ooh, lakini *schedule of amendment* inasema ni 16 – 43. Nilikuwa nadhani iliyotoka ni moja tu ili zibaki sasa 43.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kulikuwa na nyingine ambayo tulitawanya baadaye.

**MWENYEKITI:** Aah, ipo na nyingine tena! Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Degera. Naona ni mwangalifu sana katika haya. Kwa kuwa hakuna lolote kubwa linalobadilika, kwa mabadiliko hayo, tunachokipata hasa ni mtiririko mpya wa vile vifungu. Basi, sioni kwamba kuna tatizo kubwa hapo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2006**
***(The Finance Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2006 yaani *(The Finance Act 2006)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2006 Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**Azimio la Kumwezesha Waziriwa Fedha Kufuta au Kusamehe Madai au Hasara ambazo Hazilipiki Zitokanazo na Upotevu wa fedha za Vifaa vya Serikali kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2005**
***(The Public Finance Act Cap 348)***

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Madai au Hasara ambazo Hazilipiki Zitokanazo na Upotevu wa Fedha za Vifaa vya Serikali kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2005 kwa mujibu wa Sheria za Usimamizi wa Umma sura Na. 548. *(The Public Finance Act Cap 348)*.

Aidha, Azimio hili lilijadiliwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali katika Kikao chake cha tarehe 8 Agosti, 2006 kilichofanyika hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa maoni yao mazuri yenye lengo la kuboresha udhibiti na uimarishaji wa usimamizi wa mali na vifaa vya Serikali kwa lengo la kupunguza au kuepuka upotevu wa mali wa vifaa vya Serikali. Aidha, ushauri wao kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na Serikali katika kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Azimio ninalowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, ninakusudia kufuta na kusamehe madeni hasara na potevu ambazo hazilipiki kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2005.

Aidha, hasara na potevu hizi zinajumuisha chache zilizotokea miaka ya 1990 na nyingine zilikuwa ni za kati ya miaka ya kuanzia Julai, 2000 mpaka Juni 2004. Hasara za potevu hizi zimefanyiwa uchambuzi kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hasara husika zinagawanyika katika sehemu kuu tatu. Aidha, mradi huu una lengo la kuainisha kwa uwazi zaidi hasara hizo ili Waheshimiwa Wabunge waanze kuzielewa vizuri na hatimaye kufikia uamuzi ulio sahihi. Hasara hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Zile zinazohusu potevu za fedha, vifaa na malipo batili ya kiasi cha Sh. 1,710,022,920.47.

(b) Zile zinazohusu mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa ya kiasi cha Sh. 44,973,497,057.80.

Mheshimiwa Spika, jumla ya potevu yote ni Sh. 46,683,519,978.27 ambapo maelezo yake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hasara zinazohusu potevu za fedha, vifaa na malipo batili Sh. 1,710,022,920.47 zinahusisha chache zilizotokea kipindi cha miaka ya 1990 na nyingi zikiwa ni kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2000 hadi mwezi Juni, 2004 ambazo zimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo wizi wa makusanyo ya mapato uliosababishwa na watumishi wasio waaminifu kwa kudokoa na kupeleka fedha Benki zikiwa pungufu na majambazi kupora mishahara ya watumishi hasa Walimu. Hali hii sasa imepungua baada ya Serikali kuanza kupitisha mishahara ya watumishi Benki.

Aidha, sababu nyingine za upotevu ni pamoja na wizi wa mali, vifaa na uzembe *(negligence)* ambapo vifaa huachwa bila ya kuangaliwa na mwishowe kuharibika hasa kwa vifaa vilivyopo katika Bohari ya Serikali, vifaa vilivyoko katika Bohari hupitwa na wakati hivyo kutofaa kwa matumizi, na malipo batili yaliyofanyika bila ya Serikali kunufaika na huduma yoyote ambayo kwa lugha nyingine tunaita *negative expenditure*.

Mheshimiwa Spika, pengine nikupe mfano ulio hai ili kuwapa picha halisi Waheshimiwa Wabunge ya malipo batili yaliyofanyika bila Serikali kunufaika na huduma yoyote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 1998/1999 Serikali iliwahi kufanya malipo kwa Kampuni ya *K.J. Motors* na kiasi cha Sh.147,024,000/= kwa ununuzi wa magari matatu aina ya *Tipper* kwa ajili ya Idara ya Ujenzi kupitia Ofisi ya Mhandisi wa Ujenzi wa Mkoa wa Morogoro yalikuwa na thamani ya Sh. 131,250,000/=. Vile vile ununuzi wa pikipiki tano kwa thamani ya Sh. 15,774,000/= kwa ajili ya matumizi ya Idara ya Nyuki iliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 5 Novemba, 1999 Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ujenzi kupitia kwa Mhandisi wa Ujenzi wa Mkoa wa Morogoro zilipokea barua kutoka Kampuni ya *Price Water House Coopers* ikiwajulisha kwamba Kampuni ya *K.J. Motors* imefilisika na kwamba *Price Water House Coopers* ndiyo walioteuliwa kuwa wafilisi. Barua hiyo ilieleza kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii haikuwemo katika orodha ya wadai muhimu na hivyo isingeweza kurudishiwa fedha yoyote.

Aidha, Kampuni ya *Price Water House Coopers* ilitoa taarifa kwa Mhandisi wa Ujenzi wa Mkoa Morogoro kwamba magari waliyolipia hayakuwemo katika orodha ya mali za Kampuni ya *K.J. Motors* na hivyo yasingeweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Polisi ilifanya juhudi kubwa ili kuweza kurudisha fedha hizi, lakini ilishindikana. Wizara ya Ujenzi ilifungua kesi ya madai Na.263 ya mwaka 2001 dhidi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya *K.J. Motors,* kesi hiyo ilipaswa kuanza kusikilizwa tarehe 22 Machi, 2006. Lakini iliahirishwa hadi tarehe 3 Agosti, 2006 kwa kuwa mmoja wa Wakurugenzi wa Kampuni ya *K. J. Motors* alifariki dunia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi, uwezekano wa kupatikana fedha hizi ni mdogo sana na kwa kuwa suala hili limesababisha hoja za Wakaguzi kuanzia mwaka wa fedha 2001/2002, Serikali iliwasilisha mapendekezo ya kufutwa kwa hasara hii ili kusafisha kumbukumbu za vitabu vya hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kufutwa kwa hasara hii, hakumaanishi kwamba Serikali imewasamehe wadeni hawa, bali itaendelea kufuatilia kupitia taratibu za kisheria ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kesi iliyofunguliwa na Wizara ya Ujenzi Mahakamani inaendelea hadi hukumu itakapotolewa.

Mheshimiwa Spika, pili, hasara nyingine zilizoombewa kufutwa ni Sh. 44, 973,457,057.80 zinazotoka na mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa.

Mapato yaliyoshindikana kukusanywa yametokana na sababu mbalimbali zikiwemo kufilisika kwa walipa kodi, gharama za ukusanyaji maduhuli makubwa kuliko kiasi kilichotarajiwa kukusanywa, maamuzi mbalimbali ya Mahakama yanayoizuia

Serikali kukusanya maduhuri dhidi ya wadaiwa na baadhi ya walipa kodi kutokujulikana walipo baada ya kuhamisha au kufunga shughuli zao kutokana na kukosa wafadhili kama vile vyama vya hiari au Asasi zisizokuwa za kiserikali yaani, *NGO's*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000/2001, hadi mwaka 2004/2005, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA)* imekuwa inayadai kodi ya mapato Mashirika makubwa matatu ambayo ni *TAZARA*, Posta na *TANESCO*, jumla ya Sh.13, 037,182,702/=. Mashirika haya yameshindwa kulipa fedha hizo kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mfano, Reli ya *TAZARA*, biashara kwa Shirika hili imeshuka sana kutokana na kukabiliwa na gharama kubwa za uendeshaji zilizosababishwa na uchakavu wa miundombinu yake. Aidha, *TAZARA* imekabiliwa na ushindani mkubwa wa kibiashara katika njia mbadala za usafirishaji na hasa usafiri wa barabara ambao unajiimarisha siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta hivi sasa liko katika hatua za kufanyiwa marekebisho kimfumo na kimuundo. Hivyo, mojawapo ya hatua hizo ni kuhamishiwa Serikalini madeni yote yasiyolipika. Nadhani Mheshimiwa Mohammed Missanga atakubaliana nasi kwa hilo.

Kwa Shirika la *TANESCO*, Shirika hili limewasilisha Serikalini maombi ya msamaha wa faini au adhabu iliyotozwa katika kipindi cha mwaka 2001 hadi mwaka 2002 kutokana na kushindwa kulipa kodi ya mapato ya ajira, yaani *payee* kwa wakati. *TANESCO* imeomba kufutiwa adhabu hiyo kwa sababu mapato ya Shirika hayatoshi kulipia adhabu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mkakati wa Serikali wa kuimarisha Vyama vya Ushirika nchini katika muundo wa kisasa zaidi kupitia mpango mpya wa kuboresha, yaani *The Cooperative Reform and Modernization Programme,* Serikali imechukua jukumu la kufuta madeni ya vyama hivyo kwa *NBC Holdings*, Serikali za Mitaa, Taasisi nyingine kadhaa za Serikali na Bodi za Mazao ambayo jumla yake ni Sh. 15,013,073,960/=.

Aidha, ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma umechangia kwa kiasi kikubwa pia kwa Serikali kushindwa kukusanya mapato yanayodaiwa wawekezaji wanaonunua Mashirika yanayobinafsishwa hawakubali kurithi madeni ya mashirika waliyoyanunua. Hivyo, Serikali hulazimika kufuta madeni ya mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaweka juhudi katika kusimamia kikamilifu sheria ya fedha za umma, sura Na. 348 kwa lengo la kupunguza na hatimaye kuepuka hasara za namna hii. Sheria hii inabainisha pamoja na mambo mengine jinsi ya kushughulikia potevu, hasara za Serikali na inawajibisha Maofisa Wahasibu katika kuhasibu hasara na potevu hizo kwa sababu wao ndio wasimamizi wakuu wa mapato na matumizi ya fedha hizo.

Aidha, kanuni za adhabu na tozo za sheria ya fedha za umma, sura hiyo hiyo Na. 348 ya *Public Finance Penalties* and *Charges Regulations* ya 2005, zinaainisha adhabu

kwa Maafisa Wahasibu watakaoshindwa kusimamia matumizi ya fedha za umma na kukiuka taratibu za usimamizi wa fedha hizo. Ni matarajio ya Serikali kwamba, Maafisa Wahasibu watazingatia taratibu za usimamizi wa fedha za umma ili hasara za namna hii zitoweke.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kufuta hasara na kusamehe madai ambayo hayalipiki ya kiasi cha Sh. 46,683,519,978.27 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali ambalo limeambatanishwa pamoja na Azimio hili na ambalo limewasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge ili kutoa picha halisi. Kufutwa kwa hasara hizi kutasaidia kupungua kwa kiasi kikubwa hoja za ukaguzi mwaka hadi mwaka na kutoa picha iliyo sahihi ya vitabu vya hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la kufuta na kusamehe madai na hasara itokanayo na upotevu wa vifaa vya Serikali kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2005 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha tano cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma sura Na. 348 Waziri wa Fedha amepewa Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma, ikiwa ni pamoja na kugawa na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo baada ya kupata idhini ya Bunge;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa kifungu cha 43 (1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma sura hiyo hiyo ya 348, Bunge linaweza kuazimia kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi na kwa kuwa vitabu vya hesabu ya Serikali vimeonyesha kuwepo na upotevu wa fedha za Serikali pamoja na maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa;

NA KWA KUWA, kutokana na upotevu wa upungufu huo wa fedha, vifaa na maduhuli ya Serikali upo umuhimu wa kusawazisha kumbukumbu katika vitabu hivyo vya Serikali;

KWA HIYO BASI, kwa mujibu wa kifungu cha 43 (1) cha Sheria ya Usimamizi na Uthibiti wa Fedha za Umma, sura Na. 348, sasa Bunge hili katika Mkutano wake wa Nne linaazimia kumuidhinisha Waziri wa Fedha asamehe na kufuta upotevu wa fedha vifaa na malipo batili, maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa na kwa ajili hiyo kusawazisha kumbukumbu katika vitabu vya Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili Sh. 1,710,022,920.27;

(b) Mapato au Maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa Sh. 44,973,497,057/=.

Jumla Kuu ni Sh.46,683,519,978.27. Maelezo kuhusu upotevu huu, yapo kwenye makabrasha ambayo naamini Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali juu ya Azimio la kufuta upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 43, (5) (b), naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali juu ya Azimio linalotajwa hapo juu.

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Zakhia Meghji - Waziri wa Fedha, Manaibu wake Mheshimiwa Mustafa Mkulo na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Katibu Mkuu Grey Mgonjwa na Manaibu Katibu Wakuu Ndugu Ramadhan Kijja na Joyce Mapunjo pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa namna wanavyosimamia utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Sisi sote ni mashahidi kwamba Wizara ya Fedha imejitahidi kuboresha mambo mengi kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na wataalam wake kwa namna walivyoshiriki katika zoezi la kuchambua na kufanyia kazi upotevu huu. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yangu kwa kunichagua kuwa Makamu Mwenyekiti. Uchaguzi wao umeonyesha imani kubwa waliyonayo kwangu. Naomba nichukue fursa hii niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John Cheyo - Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Estherina Kilasi ambaye ndiyo mimi nasoma, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Zubeir Ali Mauld, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Fatma Fereji. Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Ponsiano Nyami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Azimio hili, ni sheria mpya ya fedha ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake ambapo ni jukumu la Maafisa Wahasibu kuhakikisha kuwa mapato na matumizi ya Serikali yanakusanywa na kutumiwa kama ilivyokusudiwa na

kuhakikisha kuwa hasara haitokei. Hasara hutokea kutokana na wizi, upotevu wa vifaa na kushindwa kukusanya mapato ya Serikali. Kama nilivyoeleza hapo juu, kuwa chimbuko la Azimio hili ni sheria mpya ya fedha inayotoa mamlaka ya kufuta upotevu wa fedha na mali ya Serikali ambapo kabla ya marekebisho ya sheria ya mwaka 2004 jukumu hili lilikuwa likitekelezwa na Waziri wa Fedha. Hivyo, kufuatia sheria mpya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo lenye jukumu hilo, Sheria inatamka kuwa taarifa ya hasara na potevu za Serikali zinaandaliwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali na kuwasilishwa mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali ambayo itachunguza na hatimaye kutoa mapendekezo ya kufuta na hatua nyingine za kuchukuliwa na Bunge la Jamhuli ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika hasara ya upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali. Waziri wa Fedha aliwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya hasara ya upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa jumla ya Sh. 47,582,540,088.5.

Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 iliyofanyiwa marekebisho ya mwaka 2004, kati ya kiasi hicho 1,710,022,926.47, ni hasara inayohusu upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili. Kiasi cha Sh. 44,937,497,057.80 ni hasara inayohusu mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa na kiasi cha Sh. 899,020,109.78, ni upotevu ambao unaendelea kufanyiwa kazi. Hasara inayohusu upotevu wa fedha, malipo batili ni Sh. 1,710,022,926.47.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa hasara na upotevu wa fedha vifaa na malipo batili ya Sh. 1,710,022,926.47. Kiasi kikubwa cha hasara hiyo kimetokana na sababu zifuatazo:-

(i) Wizi unaofanywa na watumishi wasio waaminifu kwa njia ya kudokoa maduhuli badala ya kupeleka Benki;

(ii) Wizi wa mishahara ya watumishi wa Serikali unaofanywa kwa njia ya ujambazi wa kupora au kuvunja stoo na kuiba vifaa;

(iii) Ubadhirifu wa watumishi kwa kula njama za kuhujumu fedha za Serikali;

(iv) Vifaa kupitwa na wakati na hivyo kutofaa kwa matumizi;

(v) Uzembe kama vile vifaa kuachwa bila kuangaliwa na mwisho wake kuharibika na hasa katika Bohari za Serikali; na

(vi) Malipo batili yaliyofanyika bila ya Serikali kunufaika na huduma yoyote au *nugatory expenditure*. Kama vile ilivyofanyika kwa watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Miundombinu kwa uzembe wa kuilipa kampuni ya *JK Motors* malipo ya Sh.147,024,000/= kwa ajili ya kununua magari na pikipiki wakijua kampuni hii ilikuwa katika mpango wa kufilisiwa,

hadi ilipoelezwa na mfilisi wa *Price Water House Coopers* kwamba magari na pikipiki visingeweza kupatikana kutokana na kufilisika kwa kampuni hiyo na kwamba fedha zilizolipwa hazitaweza kurudishwa.

Mheshimiwa Spika, upotevu uliosababishwa hususani kwa wizi na ubadhilifu umewasilishwa mbele ya Kamati na baada ya Serikali kupitia, Wizara na Idara na Mikoa husika kutoa taarifa Polisi na kushughulikiwa na hatima ya sera hiyo imejulikana. Kamati imeridhia kufuta upotevu wa kiasi cha Sh.1,710,022,920.47, unaohusu fedha, vifaa na malipo batili baada ya kufanya uchambuzi wa kina na kukuta kwamba watuhumiwa hawajapatikana kabisa na wengine wamefariki wakiwa bado wanadaiwa.

Mheshimiwa Spika, mapato na mduhuli yaliyoshindikana kukusanywa ya Sh. 44,473,497,057.80, Kamati iliridhika na hasara iliyohusu mapato na maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa kwa jumla ya Sh. 44,473,497,057.80. Kamati ilibaini kuwa hasara hiyo ilitokana na Serikali kushindwa kukusanya mapato hayo kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Kutokana na mapato ya makapuni au mashirika yaliyobinafishwa;

(ii) Gharama ya ukusanyaji kuwa kubwa kuliko kiasi kinachopatikana;

(iii) Madeni ambayo Serikali ilikuwa inadai mashirika ambayo yamefilisika.

(iv) Maamuzi mbalimbali ya Mahakama dhidi ya Serikali au dhidi ya wadau wanaodaiwa na Serikali.

(v) Baadhi ya wadaiwa kutokujulikana waliko baada ya kuhamisha au kufungu shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, katika kiasi hicho cha hasara, Sh. 44,973,397,057.80 kuna maeneo ambayo yamechangia kuongezeka kwake. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2000/2001 hadi 2003/2004, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, inadai kodi ya mapato ya Mashirika makubwa matatu, ambayo ni *TAZARA*, Shirika la Posta na *TANESCO*, jumla ya Sh. 13,037,182,702/=. Mashirika haya yameshindwa kulipa fedha hizo kutokana na sababu mbalimbali zifuatazo:-

Reli ya *TAZARA* kushuka kibiashara kutokana na kukabiliwa na gharama kubwa za uendeshaji zilizosababishwa na uchakavu wa baadhi ya miundombinu yake na ushindani wa kibiashara kwa njia mbadala za usafirishaji na hasa usafiri wa barabara ambao unajiimarisha siku hadi siku. Aidha, Shirika la *TANESCO* limeomba msamaha wa faini au adhabu walizotozwa katika kipindi cha mwaka 2000 mpaka 2001, hadi 2002, kwa kodi ya *payee* walioshindwa kulipa kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika viko mbioni kuimarishwa upya katika muundo wa kisasa zaidi kama mpango unasema *Cooperative Reform and Modernization Programme (CRMP)* na ili kuwezesha mpango huu kufanikiwa, Serikali imechukua

mzigo wa madeni yake ambayo kati ya hayo, Serikali imeazimia kuyalipa jumla ya Sh.15,013,073,960/= yamependekezwa kufutwa. Kati ya hayo yapo mashirika ambayo yalipatiwa mtaji na Serikali kutokana na misaada kutoka nje kwa makubaliano kwamba mashirika hayo yangeilipa Serikali. Kufilisika au kubinafishwa, kuvunjwa kwa mashirika hayo kunasababisha deni kutolipwa na hivyo kubaki hasara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya Serikali kwenye mashirika ya umma, Kamati imeridhika na hasara hiyo kufuatia sera ya ubinafsishaji ambayo madeni hayo yamekuwa ni mzigo wa Serikali hasa ukizingatia kuwa mwenye mashirika hayo ni Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Spika, upotevu unaoendelea kufanyiwa kazi, Sh. 899,020,109.78 ni hasara ambazo ziliwasilisha mbele ya Kamati kwa taarifa tu kama kanuni ya fedha inavyohitaji. Hasara hizo bado hazijafikia hatua za kuziombea kibali cha kufutwa kwa sababu bado ziko katika ngazi mbalimbali za kufanyiwa kazi. Mathalan kesi zilizopo Polisi na Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hasara au upotevu huo umekuwa ni chanzo kikubwa cha hoja za ukaguzi kwa Wizara na Idara za Serikali kwa muda mrefu baada ya uchambuzi wa kina, Kamati imeridhika kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu kufuta hasara na upotevu huo mwenye thamani ya Sh. 46,683,519,978.27 kama ifuatavyo:-

Upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili Sh. 1,710,022,920.47, mapato na maduhuli yaliyoshidikana kukusanywa Sh. 44,973,497,057.80/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeweka bayana kuwa kufuta upotevu huo maana yake ni kutaka kujipanga upya, kuhakikisha tunatunza vema fedha na vifaa vya Serikali na sio dhana ya kiweka vitabu sawa. Aidha wajumbe wamebaini kwamba upotevu mwingi unaruhusu maafisa wenye mahusiano ya karibu na wafanyabiashara. Matharani katika mwaka 1998/1999, malipo batili yaliyofanyika bila Serikali kunufaika na huduma yoyote kwa kampuni ya *KJ Motors* kwa ajili ya kununu magari na pikipiki huku wakifahamu kabisa wanafilisika. Hii inaonekana kwamba kuna safu ya watu wanaojipanga kwa kushirikiana katika kufanya malipo yasiyo ya halali katika matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upotevu huo, Kamati yako imetoa ushauri ufuatao:-

(i) Kamati imeagiza Serikali iwe na njia nyingine ya kufanya uchunguzi kuhusu fedha na mali za Serikali bila kuichia Mahakama peke yake;

(ii) Serikali ibuni utaratibu ambao hautaruhusu upotevu wa kiasi kikubwa cha fedha na mali za Serikali;

(iii) Katika uwasilishwaji wa upotevu wa fedha na vifaa, Serikali iweke bayana kama kuna kiwango ambacho kinaruhusiwa kitaalam kulingana na Bajeti ya mwaka husika, kwa maana iwekwe asilimia kwamba kwa mwaka ni asilimia ngapi ya hasara inatakiwa itokee;

(iv) Pale ambapo kampuni imefilisiwa, Wakurugenzi wawajibike moja kwa moja kwa kuwa ndiyo walikuwa wakiendesha makampuni husika;

(v) Kuwepo na udhamini binafsi wa Wakurugenzi *Personal Performance Guarantee for Directors*, kwa maana ya kwamba endepo makubaliano ya mikataba ya manunuzi hayatatekelezwa Mkurugenzi husika awajibike;

(vi) Serikali iimarishe uwekaji wa kumbukumbu zake, wawepo Wahasibu na Wakaguzi wa ndani wa kutosha na wenye taaluma katika kila Idara, Wizara na Wakala wa Serikali; na

(vii) Upotevu wowote unaohusu mwaka 2004/2005 utajadiliwa kwenye Kamati kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati ni kwamba, kuwepo kwa kipindi maalum cha Bunge kujadili Matumizi ya Bajeti iliyopita ili kuzuia matatizo ya mwaka unaoishia yasijitokeze katika mwaka unaofuata. Kwa maana hiyo, Bunge lisipitishe Bajeti ya Wizara yoyote mpaka ithibitishwe matumizi ya mwaka uliopita yalikuwa halali. Wajumbe wamebaini kuwa Maafisa Wahasibu hawawajibiki moja kwa moja katika hasara hizi.

Hivyo basi, upotevu wowote uwasilishwe mbele ya Kamati ili Afisa Mhasibu mhusika awajibike; Bunge lishirikishwe katika mchakato mazima wa *Public expenditure Review*; iwepo sheria kwa wale wote wanaoihujumu Serikali kutoruhusiwa kuanza biashara nyingine mpaka watakapotoa maelezo yanayoridhisha au kuilipa Serikali. Kwa maana hiyo, sheria ya ufilisi ifanyiwe rejea ya marekebisho.

Maafisa uhasibu wapewe pia maelekezo kuhusu upotevu na watoe taarifa inayohusu upotevu katika Idara, Wizara husika pamoja na hatua alizochukua wakati wa kuwasilisha mahesabu yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaliomba Bunge likubaliane na Maoni na Mapendekezo ya Kamati ili Bunge lako Tukufu likubali Azimio la kumwezesha Waziri wa Fedha kufuta madeni au hasara iliyotokana na upotevu wa fedha au mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa fedha. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE KABWE Z. ZITTO – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani

kuhusu Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Madeni au Hasara itokanayo na upotevu wa fedha au vifaa vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 43 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Udhibiti wa Fedha za Umma, Bunge kwa Mamlaka yake linaweza kuazimia kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, katika jumla ya fedha zote ambazo Waziri anaomba zisamehewe asilimia 96.34 ni fedha zinazotokana na Serikali kushindwa kukusanya maduhuli yake na kati ya fedha hizo, Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zake inaomba kusamehewa jumla ya Shilingi bilioni 29 na Wizara ya Kilimo kwa kupitia fedha ambazo zinasamehewa kwa Vyama vya Ushirika inasamehewa jumla ya Shilingi bilioni 15. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani, hii inaonyesha jinsi gani Serikali ipo legelege kukusanya maduhuli yake.

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zote ambazo Serikali inaomba zisamehewe, Shilingi bilioni 46, ni Bajeti ya Wizara mbili kwa miaka miwili. Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Bajeti ya Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ndiyo thamani ya pesa ambazo Serikali inaomba zisamehewe.

Mheshimiwa Spika, pesa hizi ni nyingi mno. Lakini katika fedha ambazo Serikali inaomba kusamehewa katika Wizara ya Kilimo, kwa kuweka kumbukumbu sawa, baadhi ya Vyama vya Ushirika ambavyo vilikuwa na madeni sugu na kufuatia Serikali kufanya juhudi za kuibua upya ushirika, kipindi hicho wakulima walilazimishwa kukatwa asilimia fulani ya mauzo ya mazao yao ili waweze kulipia madeni. Mfano wa hili ni Ushirika wa Wananchi wa Mkoa wa Kagera ambao walikuwa wanakatwa kahawa yao ili waweze kulipia madeni ya Vyama vyao vya Ushirika. Sasa nataka kufahamu, kwa kuwa Serikali imeamua kusamehe madeni yote ya Vyama vya Ushirika; Je, wakulima watarudishiwa fedha zao ambazo wameshakatwa?

Mheshimiwa Spika, kiasi cha Shilingi zipatazo bilioni 12 ni maduhuli yaliyoshindwa kukusanywa kutokana na kufilisika kwa mashirika binafsi. Tunaitaka Serikali kuleta orodha ya mashirika hayo na wamiliki wa mashirika hayo ambayo yalifilisika, kwani tunadhani kwamba huu unaweza kuwa ni ujanja wa watu hao hao kubadilisha majina ya kampuni, lakini kwa maana halisi bado ni wenyewe hao hao.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna kiasi cha Shilingi bilioni 3.237 kama hasara ya malimbikizo ya maduhuli ambayo yalikuwepo kabla Serikali kubinafsisha Mashirika ya Umma. Kambi ya Upinzani ina uhakika kwamba mashirika yanapobinafsishwa wale wanaonunua (wawekezaji) wanachukua mali zote zinazokuwa chini ya miliki ya mashirika hayo kama nyumba na kadhalika. Sasa, ni kwa nini mashirika hayo yasichukue na madeni ambayo mashirika yanayobinafsishwa yanakuwa nayo?

Mheshimiwa Spika, kwa hili, Kambi ya Upinzani haiko tayari kukubali Azimio hili kwa sababu tunapoteza pesa nyingi sana ambazo zingeweza kuleta maendeleo kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaomba kufuta madeni ya mashirika makubwa kama *TANESCO* na *TAZARA*. *TANESCO* inaomba kufutiwa Shilingi bilioni 4.46 ambayo ni maduhuli toka mwaka 2000 mpaka 2006.

Mheshimiwa Spika, hapa Kambi ya Upinzani inaona tutakuwa hatuwatendei haki Watanzania kwa Shirika hili kwa sababu karibu kila mwezi Shirika hili linapata ruzuku ya Serikali ya Shilingi bilioni tatu. Kama wanapatiwa ruzuku, ni kwa nini washindwe kulipa stahili zote za Serikali? Kuhusu deni la *TAZARA*, hii ni mamlaka inayomilikiwa na nchi mbili. Sasa tunataka kufahamishwa: Je, wenzetu wa Zambia nao watafuta madeni kwa *TAZARA*?

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa, kati ya pesa hizo zinazoombwa kufutwa ni pamoja na fedha wanazolipwa wanunuzi mbalimbali wa vifaa vya Serikali kama vile magari na pikipiki, lakini wakashindwa kuwasilisha vifaa hivyo Serikalini kama mkataba wa zabuni unavyowataka wafanye hivyo. Mfano ni malipo ya *K.J. Motors* ya Shilingi milioni 131.

Huyu mmiliki wa *K.J. Motors* yuko wapi? Je, ana Kampuni nyingine inayofanya kazi hiyo hiyo aliyokuwa anaifanya kabla? Kwa kuwa kesi bado iko Mahakamani, kuna haraka gani kwa Serikali kusamehe pesa hizi? Tunaiomba Serikali katika pesa hizi isizisamehe mpaka kesi itakapokwisha ili tuweze kujua matokeo ya kesi ni nini.

Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani kabla ya kukubaliana na Azimio hili, tunataka Serikali isubiri kwanza mpaka tutakapoweza kukusanya hizo pesa.

Mheshimiwa Spika, pia Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuweka njia nzuri za kutunza mali ya umma ili kuepuka upotevu mkubwa kama hivi leo tunavyotaka kutoa Azimio la kusamehe pesa kama hizi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilidokeza mwanzo, ni sheria inampa mamlaka Waziri wa Fedha kutoa Azimio la kufuta madeni na sisi tunaitambua sheria hiyo, lakini tumetoa maangalizo ambayo tunaomba Serikali itupatie majibu na vinginevyo hatutakubaliana na Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Ninayo majina ya wachangiaji watatu, nadhani tunaweza kuanza na mmoja ili kupunguza kazi ya kesho. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Napenda kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake kwa hii hoja ambayo imeletwa kwa sababu mimi binafsi naiona ni ya msingi na kwa sababu nimekuwa ni mmojawapo ambaye nilikuwa nikiona mzigo ambao unakabili mashirika hayo ikiwemo *TANESCO* ambayo nimekuwa nikiifanyia kazi na kufahamu hali halisi ya mazingira waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, ni kwa vile hatuwezi kujua kwa uharaka jinsi ambavyo Serikali inajitahidi hasa katika kuleta ufanisi kwa niaba ya Watanzania wote. Mara nyingi sana Kambi ya Upinzani nimekuwa nikiisikia ikizungumzia suala la *TANESCO* kuhusiana na kupewa ruzuku. Lakini tukirudi nyuma, kwa mfano katika suala la ukame, suala hili tumelishuhudia na Serikali iliweza kutoa ruzuku ya kununua chakula kutokana na ukame. Ndiyo hivyo pia ambavyo Shirika la *TANESCO* limekuwa likipata matatizo kama hayo.

Mwaka 2000 kwa kumbukumbu zangu, ni katika miaka ambayo *TANESCO* ilipata hasara kuliko miaka mingine yote na ndiyo maana Serikali iliona haja kwa nini Serikali inaendelea kupata hasara. Ilifikia hata maamuzi ya kuona kwamba aidha Shirika libinafsishwe na hata wakafikia kuweka *Management* ya *Net Group* ili kuweza kunusuru hali ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, Shirika hili limekuwa likifanya kazi hata zile zisizolipa. Narudia kuzungumza sentensi hii. Shirika hili halifuati ile dhana ya kuwa *business is a separate entity* kiasi kwamba ifanye kazi zake kwa kufuata faida peke yake. Kuna wakati tunasema tunahitaji umeme uende katika Kijiji cha Mbika kule, inafikia ni lazima ipelekwe jenereta ya *Megawatt* moja na mafuta bei zake tunazijua na inabidi i-*operate* katika misingi hiyo.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka pia kulikuwa na tatizo katika *system* yetu kwa upande wa ulipaji wa *bills* zetu. Nakumbuka miaka ile ulikuwa hata huwezi kwenda kukata umeme kienyeji kienyeji. Katika hilo nasema, kulikuwa na mapungufu fulani kwa upande wa Serikali pamoja na mashirika yale ambayo yalikuwa kwa namna moja yameegemea upande wa Serikali, kiasi kwamba mpaka walipofika wale wenzetu wa *Net Group* ndipo tulipoanza kulipa madeni yetu. Hiyo pia ilisababisha shirika kufanya shughuli zake kwa hasara.

Kwa hiyo, kwa mtu yeyote yule unayefanya biashara na unayehitaji angalau uweze ku-*survive*, huwezi kusema nakwenda kulipa kodi wakati unajua utafunga biashara. Hiyo ndiyo hali ambayo iliikabili *TANESCO*. Kwa hiyo, naomba tuwe Wazalendo wa kuona ukweli. Nalizungumzia Shirika hili kwa niaba ya mashirika mengine ambayo yamepitia *process* hii. Tuwe wazalendo na tumeona faida ya kubinafsisha kutokana na matatizo yaliyopo. Tunashindwa nini kutambua madeni na matatizo yaliyokuwepo huko nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono katika yale matatizo ambayo yalisababishwa kiuzembe kama yapo. Kama yapo basi yachukuliwe hatua, lakini kwa yale ambayo yana msingi ndani yake naomba sana Kambi ya Upinzani tuunge mkono ili *account* zetu zikae vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo naliona kwa upande wa *bills* za *TANESCO* ni kwamba tuna-*charge* kodi kwa mfano kabla hata mteja hajalipa. Kwa hiyo, kunakuwa kuna mlundikano wa madeni ambayo bado hayajalipwa.

Nadhani kama tulivyoamua kufanya kazi kwa kasi mpya na ari mpya na kama tulivyoamua kuona kwamba zile *bills* kwa mfano zinazokuwa zinasumbua wateja pasipo sababu kwa sababu tu zinashindwa kufutiwa madeni yake mpaka ipatikane kibali cha Serikali, basi ni wakati muafaka na sisi sasa kuweza kuunga mkono ili tumalize hii kazi na tuanze kwa kasi mpya kama ambavyo tumeamua. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hakika muda uliosalia sasa hauwezeshi mchangiaji anayefuatia kuchangia, kwani ninao wawili. Hata huyo mmoja tu itakuwa haifai kwa sababu ni dakika tano, itakuwa ni kumharakisha na kumnyima haki yake. Tuna muda mzuri kesho na kwa hiyo, ningeomba kusema kwamba itabidi tuahirishe ili tuweze kuendelea kesho. Lakini kabla ya kufanya hivyo, ninalo tangazo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, leo katika mchezo wa mpira wa miguu kule Dar es Salaam timu ya Simba imeifunga timu ya Yanga kwa *penalty*. Timu ya Simba iliongoza kwa goli moja, baadaye katika dakika za majeruhi Yanga wakarejesha. Kwa hiyo, wakasawazisha, zikapigwa *penalty*, Simba wakapata *penalty* saba na Yanga wamepata *penalty* sita. Kwa hiyo, nasikitika kuwaharibia jioni watani zetu wale wa Yanga, lakini hiyo ndiyo hali halisi. Kama nilivyosema awali, kuna timu kubwa na kuna timu bora. Sasa leo usemi wa Spika nadhani umetimia. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya salaam hizo, naomba sasa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.38 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku yaJumatano,*
*Tarehe 16 Agosti, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*